

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 17 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA
MICHEZO:-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:-

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA (K.n.y. MHE. EDWARD LOWASSA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):-

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MHE. VINCENT J. NYERERE – MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaanza maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo kwa niaba yake Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Na. 207

Fedha za Matumizi ya Kawaida (OC) kwa Halmashauri

MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO) aliuliza:-

Kutokana na ufinyu wa Bajeti, Halmashauri nyingi zilipata fedha kidogo sana za OC katika mwaka wa fedha uliopita:-

(a) Je, ni Halmashauri ipi ilipata fedha nyingi zaidi na ni kiasi gani ikilinganishwa na Bajeti husika iliyopitishwa?

(b) Je, ni Halmashauri ipi ilipata fedha kidogo zaidi, na ni kiasi gani ikilinganishwa na Bajeti husika iliyopitishwa?

(c) Je, nini kifanyike kuondoa athari zilizojitokeza kutokana na ufinyu wa fedha hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upangaji wa Bajeti zikiwemo fedha za matumizi ya kawaida (OC) huzingatia idadi ya watu, ukubwa wa eneo, hali ya kipato (hali ya umaskini) pamoja na urefu wa barabara unaozunguka eneo la kutolea huduma. Aidha, kila Halmashauri inapanga Bajeti kwa kuzingatia ukomo wa Bajeti Kitaifa kwa mwaka (*ceiling*) pamoja na mahitaji ya Halmashauri kulingana na vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri iliyopata fedha nyingi zaidi ya matumizi ya kawaida kwa kulinganisha na makisio kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ni Halmashauri ya Wilaya

ya Mafia ambayo ilipata shilingi bilioni 1.01 ikilinganisha na makisio ya shilingi 938.7 sawa na asilimia 109.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri iliyopata fedha kidogo sana ni Halmashauri ya Wilaya ya Geita ambayo ilipata shilingi bilioni 2.5 ukilinganisha na shilingi bilioni 4.5 ambazo zilikuwa zimepangwa, hii ikiwa sawa sawa na asilimia 55.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada za makusudi za kupunguza athari ambazo zinatokana na ufinyu wa Bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Kurejesha ruzuku ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa yaani *General Purpus Grant (GPG)*.

(ii) Kuanzisha Kamati za kuboresha ukusanyaji wa mapato na kubaini vyanzo vipya vya mapato katika Serikali za Mitaa.

(iii) Kutambua na kubaini vianzio vya mapato yasiyo ya kodi kama vile michango ya wananchi, Taasisi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kuyaingiza katika mfumo wa mipango na Bajeti.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, lakini hakuna uwiano wa karibu kati ya Halmashauri ambazo zimepata fedha kwa wastani na zile ambazo zimekosa kwa kiasi kikubwa sana. Hii tofauti

inaleta vilevile matatizo katika ufanisi wa utendaji ndani ya Halmashauri.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu kuondoa tofauti hizi kati ya uwiano wa fedha zinazopelekwa katika Halmashauri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, labda hapa niweke vizuri ni mambo gani tunayazungumza hapa. Hapa hatuzungumzii Bajeti yote kwa ujumla kwa maana ya Maendeleo na ile ya mishahara, hapa tunazungumzia habari ya *OC* na *concern* ya Mheshimiwa Herbert Mntangi naiona hii aliyoizungumza ya uwiano. Sasa kilichoangaliwa hapa ili niweze kulisaidia Bunge hili Tukufu na tuweze kuelewana vizuri kwamba nini kinachozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo alichouliza hapa yeye alitaka kujua kama umebajeti umesema kwamba mimi fedha hizi ndizo ninazozomba.

Je, ni Halmashauri ipi ambayo inaonekana kwamba imepata zaidi ya kile ambacho ilikuwa imeomba na Halmashauri ambayo imeonekana kwa ulinganisho huo na hiyo ni kwa asilimia.

Kwa hiyo, ukisema uchukue mahesabu yenyewe Wilaya ambayo itaonekana inaongoza hapo itakuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni ndiyo itakuwa inaongoza na Wilaya ambayo itaonekana ipo chini sana ni hiyo hiyo Wilaya ya Mafia tuliyozungumza hapa.

Ukienda Mafia pale ukaingia pale kuna *Regional Consultative Committee* ambayo itakwenda kufanyika Kibaha pale hata kama ni *messenger* anakwenda lazima apande ndege hakuna kusema utatumia gari la Mkuu wa Wilaya. Hutaweza kwa sababu watawuka wataenda upande wa pili hiyo tu kwanza ni kigezo kimojawapo na wakifika upande wa pili lazima wafanye *arrangement* ya magari yatakayobeba *crude oil* yote. Kuna Bodi ya Barabara pale, kuna *Regional Consultative Committee* na Mikutano mengine na *Headquarters* zake zote zipo Kibaha.

Pili, hawa wenzetu wa Mafia ambao inaonekana fedha zimeongezwa hapa kwa sababu ya hiyo jiografia yao na Mheshimiwa Shah yupo hapa anasikia. Walikuwa na madai ya Walimu, walikuwa wanadaiwa pale shilingi milioni 28.9 nikatafuta *percentage* yake hii imewaongezea kwa kiasi gani ambazo zililipwa kwa kelele zilizopigwa pale ilikuwa ni *five percent*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *the bottom line is* hapa Halmashauri ndizo zinazopanga Bajeti, ndizo zinazoweka kipaumbele kama unaona maji ni kipaumbele utasema maji yatawekwa kulingana na kipaumbele. Lakini vyote hivi Mheshimiwa Mbunge vinakuwa na *ceiling*. Kwa hiyo, hii ndiyo hali halisi iliyojitokeza pale.

SPIKA. Ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Mhagama swali la nyongeza.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, hili tatizo la *OC* kutofika kwa wakati kwenye Halmashauri zetu ama kufika kidogo kumetengeneza tatizo kubwa la Madiwani

kutokukaa vikao vyao vya Kikatiba kwa muda unaotakiwa na wakati mwingine Madiwani wamekuwa wakikaa kwa kukopwa na hivyo kusababisha usimamiaji wa Halmashauri kufanya kazi umekuwa ni mgumu na ambayo kwa kweli siyo usimamiaji unaotakiwa.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutengeneza mfumo wa kulipa OC za uendeshaji wa Vikao vya Madiwani katika kila Halmashauri kwa wakati angalau hilo liweze kufanyika na usimamiaji wa shughuli za Halmashauri uende kama ilivyopangwa kwa kupitia Vikao vya Madiwani? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEM): Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo tunalipata mwaka huu ni kama vile ambavyo Naibu Waziri amesema kwamba kuna vyanzo ambavyo vilifutwa katika Bajeti ambayo tumemaliza. Lakini katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda nao vyanzo vile vimerejeshwa na fedha imeongezeka kutoka bilioni 50 ile ambayo tulistahili kupata ikafutwa hadi shilingi bilioni 63.5 ambazo zenyewe sehemu nyingine inayobaki ni kwa ajili ya vikao.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na uhakika kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha Vikao vya Madiwani vitaenda kama kawaida. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Luhaga Mpina, atauliza swali hilo.

Na. 208

Mradi wa Maji - Kisesa

MHE. LUHAGA J. MPINA aliuliza:-

Je, Serikali iko tayari kuanza upembuzi yakinifu na ujenzi wa Mradi wa Maji toka Maswa hadi Mwandoya katika Jimbo la Kisesa ambapo kuna umbali mfupi sana?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kisesa lenye Makao Makuu yake katika Kijiji cha Mwandoya, linakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 192,917 ambapo kati yao ni asilimia 44.5 wanapata maji toka kwenye mradi wa maji wa bomba Igobe/Mwandoya (1), visima vifupi (253) na matanki ya kuvuna maji ya mvua 48. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Meatu inakadiriwa kufikia asilimia 54.6.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali iliidhinisha jumla ya shilingi milioni 440.3 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwa vijiji vya Sakasaka na Mwang'humbi vyenye wakazi wapatao 11,085.

Katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, zimetengwa jumla ya shilingi milioni 144.3 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji vya Mwamalole na Bukundi. Kati ya hizo fedha shilingi milioni 48.2 zitatumika kufanya upembuzi yakinifu kwa vijiji vya Mwanjoro, Nkoma, Mwambiti, Mwamishali, Ng'hoboko, Lubiga na Itinje.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, kwa waka 2012/2013 imetenga shilingi milioni 1.04 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa umeme kwenye mtambo wa maji wa kijiji cha Mwandoya.

Aidha, kijiji hiki kitaendelea kupewa kipaumbele cha kufanyiwa upembuzi yakinifu kadri rasilimali fedha zinavyopatikana.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa wakati nauliza swali langu hili la msingi nilikuwa na ufahamu wa kutosha kuwa mradi wa maji wa bomba la Ziwa Victoria ambao sasa hivi utajengwa mpaka pale Wilayani Maswa ukitokea Kishapu; na kwa kuwa ukiwa pale Maswa kwenda Makao Makuu ya Jimbo la Kisesa ni kilomita 40 tu, ndiyo nikataka Serikali sasa kwa sababu wananchi wa Maswa maji hayo yatakuwa yamefika Maswa; na kwa kuwa yatakuwa yamekaribia sana kufika Jimbo la Kisesa pale Makao Makuu ambapo ni Mwandoya kwa kupitia katika vijiji vya Mwabayanda, Guguli, Senani, Mwabusalu na kisha Makao Makuu ya Jimbo la Kisesa.

Kutoka Mwandoya halafu yanaenda safari kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu ndiyo nikataka Serikali sasa ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba upembuzi yakinifu unafanyika haraka na ujenzi unafanyika haraka

kufikisha maji katika Makao ya Makuu ya Jimbo la Kisesa na Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu?

Lakini swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza hapa kwamba wanaendelea kufanya upembuzi yakinifu katika vijiji alivyovitaja vikiwemo Itinje pamoja na Lubiga, lakini leo ni karibu miaka mitatu toka visima hivyo vitobolewe katika vijiji hivyo na hakuna hatua yoyote ambayo imefanyika. Sasa ni lini hizi danadana zitakwisha na maji yatapatikana kwa wananchi katika vijiji hivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, umenitaka nieleze kwa kifupi na ninaheshimu maelekezo yako. Mimi nataka niseme kitu kimoja hapa, hii Halmashauri ya Meatu inayozungumzwa hapa inao mradi mkubwa pale. Yapo Majimbo mawili ya uchaguzi pale Kisesa pamoja na Meatu yenyewe. Wizara ya Maji imeweka pale bilioni 150 mimi nataka tupate hiyo picha kwanza.

Naiielewa *concern* ya Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Mpina mimi nimekwenda mpaka katika Halmashauri yake nimekwenda mpaka katika lile Jimbo lake la Uchaguzi ni kweli anachosema kuna tatizo pale. Maji yanayotumika pale yanatoka katika Mto mmoja unaitwa Igobe.

Kwa hiyo, hii milioni 1.04 tulitenga hapa kwa ajili ya nguzo za umeme tu pale ili kuweka mfumo wa umeme ili kusukuma maji. Nikawaita watu wangu nimezungumza mimi na engineer wa maji, nimewaita watu wote wa Mkoa nikawaambia niambieni Mheshimiwa Mpina anataka maji

yanayozungumzwa hapa maji yanatoka Kishapu yanakwenda Maswa yakitoka hapo yanakwenda kule Meatu.

Tukifanya hesabu za haraka haraka hapa *engineer* wa kule akaniambia kama tukiwa na bilioni 8 au 9 hivi yanaweza yakafika. Wale watu wa kwangu wakaniambia hazitoshi lazima hapa uwe na *access road* za kwenda kwenye barabara na nyumba za watumishi na kadhalika ikaonekana ni shilingi bilioni 30, tuiweke vizuri hapa ili tuweze kuelewana, mimi siwezi kupinga jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tutakachofanya hapa kwa sababu hiyo bilioni 30 itakuwa ni *issue* ya Bajeti ambayo itakuwa ni kitu kigumu. Bajeti ni mfumo wa Serikali unavyoonyesha hela zitakavyopatikana na jinsi zitakavyotumika *which is almost impossible*.

Lakini tutakachomsaidia sisi ili aondokane na tatizo hili pale Mwandoya anapozungumzia tutasaidia kuimarisha kile chanzo cha maji pale. Lakini wakati huo huo tutaweka matanki mengine makubwa kule na hii itaingizwa kwenye B+ajeti inayokuja sasa ili kusaidia kusukuma maji pale yapelekwe kwanza mlimani halafu yashuke kwa *gravity* ndiyo yaweze kwenda kule Meatu kunakozungumzwa.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, swali la msingi la Mheshimiwa Mpina halitofautiani na watu wa Jimbo la Nkenge ambao wanakaa kando kando ya Mto Kagera, lakini huwezi kuamini hatuna maji safi na salama.

Je, ni lini Serikali itafanya utaratibu wa kufanya watu wa Misenyi wapate maji safi na salama, kwa kuwa kuna mto ambao hauna hata kilomita moja waweze kupata maji ya kunywa? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naye pia Mheshimiwa Assumpter Mshama anafahamu kwamba nimekwenda Misenyi na kule nimefika nimeiona hii *problem* tunayozungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa sisi wote tulimsikia Waziri wa Maji aliposimama hapa Profesa Maghembe akizungumzia nini ambacho wanakusudia kufanya hapa. Ni kweli kwamba ukichukua maji haya kutoka mtoni kuyapandisha kule na ukiyapeleka kule anakotaka Mheshimiwa Assumpter Mshama na ninafahamu huko anakozungumzia. Maana yake ni kwamba gharama za kuchukua hayo maji zitakuwa ni kubwa sana.

Kwa hiyo, yule mtumiaji wa mwisho pale ujue pia yale maji yatakuwa na kelele, hivi hapa ninatokea Mpanda na Sumbawanga kule, tumekwenda tumeshusha maji pale kule kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoka ndoo moja sh. 150 tumeirudisha sh.30 na tumetoa maelekezo tukasema kwamba hakuna mtu atakayetoza zaidi ya hizo hela tulizosema hapo na kama watu wanataka kujaribisha wajaribishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini turudi Misenyi kinachozungumza hapa tumeambiwa kwamba kila watu wachague vijiji vyao vitano, nafikiri Mheshimiwa Mshama atakwenda kufanya hivyo. Vijiji vitano mwaka huu na vijiji

vitano mwaka mwingine unaokuja ili tuweze kuondoa tatizo lililopo hapo la maji.

Lakini hili la mto analisema tutakwenda kukutana na watu wetu tuchunguze vizuri kwamba ni kiasi gani kinachohitajika katika hili eneo ili tuweze kumpa *position* na *status* ya hilo tatizo. (*Makofi*).

Na. 209

Kuutangaza Mlima Kilimanjaro

MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO aliuliza:-

Wakenya wanautangaza Mlima Kilimanjaro kuwa uko Kenya, Serikali yetu nayo inatangaza kuwa ukitaka kupanda Mlima Kilimanjaro njoo Arusha wakati wananchi wa Moshi wanasema mlima huo uko Moshi:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya mkanganyiko huu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umaarufu wa Mlima Kilimanjaro katika Soko la utalii Duniani ni mkubwa na wenye kuvuta hisia za wadau wa utalii, wapenzi na wapanda milima kote ulimwenguni; na hivyo imepelekea kuwepo mvutano wa wapi hasa Mlima huu upo na wageni wapitie Mji gani

katika safari yao ya kwenda kutimiza ndoto yao ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Mlima Kilimanjaro uko Tanzania, katika Mkoa wa Kilimanjaro; na nakubaliana na Mheshimiwa Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kuwa ili mtu yeyote aweze kupanda Mlima Kilimanjaro ni sharti afike Mkoa wa Kilimanjaro, na kupanda mlima kupitia njia zake rasmi za Marangu, Machame, Londorosi, Umbwe na Rongai, ambazo husimamiwa na Hifadhi za Taifa (TANAPA).

MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ningepomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Mlima wa Kilimanjaro ndio unauingizia nchi fedha nyingi za utalii kuliko sehemu nyingine yoyote. Na kwa kuwa wageni huwa wanatumia ndege ili waweze kuja kupanda Mlima wa Kilimanjaro. Ningemwomba Waziri hata kutumia fedha zake za ujirani mwema tukarabati Uwanja wa Ndege wa Moshi Mjini ili uweze kutumiwa na wageni?

Pili, kwa kuwa nchi jirani ya Kenya inajenga Kiwanja cha Kimataifa pale Taveta kilomita 5 tu kutoka mpakani, Kiwanja hiki kitatupokonya mapato yote ya Mlima Kilimanjaro. Kwa nini Serikali isiwe na mkakati maalum wa kuweka miundombinu ambayo inafaa pamoja na Uwanja wa Ndege, Reli na Barabara katika mji wa Moshi na kuutangaza ndio mji wa utalii wa Kilimanjaro ili tusije tukakosa mapato ya Mlima huu kwa sababu Kenya itatumia Taveta kama ndio mji wa Mlima wa Kilimanjaro. Naomba majibu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inafahamu mipango ya wenzetu wa Kenya ya kujenga uwanja Taveta. Jitihada ambazo Serikali tayari imefanya moja tunahakikisha kwamba tunaongeza matumizi ya Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Muda wowote kuanzia sasa hivi Shirika la Ndege la *Qatar* litafanya safari za moja kwa moja kutoka *Qatar* mpaka Uwanja wetu wa Kilimanjaro kuungana na *KLM* ambao tayari wanafanya kila siku, *Ethiopia Airways* na *Precision Air* ambao wanaunganisha watalii wanaopitia Nairobi na *KQ*, *South African Airways* na ndege zingine ambazo tunaendelea kuzungumza nao waweze kuja Kilimanjaro. Kwa maana ya wageni wanaotoka nje ya nchi uwanja wa Ndege wa Kimataifa bado utaendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, la pili ninakubaliana naye kwamba itakuwa ni muhimu kwa Mamlaka zinazofuata kuboresha zaidi Uwanja wa Ndege wa Moshi kama ambavyo tumeendelea kufanya katika Uwanja wa Ndege wa Arusha. Na ni matumaini ya Serikali kwamba Uwanja wa Ndege wa Arusha na Uwanja wa Ndege wa Moshi peke yake pia unaweza ukawa kivutio kikubwa kwa watalii ambao wasingeweza kuwa barabarani kwa muda mrefu kutokana na sababu za kiafya au sababu za muda.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimhakikishie tu Mheshimiwa Ndesamburo kuwa Halmashauri yake ya pale Moshi kwa kushirikiana na Wizara yangu tunaweza tukaendelea kukaa na kuangalia ni jinsi gani tushirikiane kwa pamoja kwanza kuendelea kuutetea Kilimanjaro, lakini pia kuhakikisha kwamba miundombinu ya Mji wa Moshi inaboreka ili watalii wanaochagua kukaa Arusha ili wapande Kilimanjaro wawe na kitu tunachoita katika utalii

options, mtu aamue atakaa, atalala Marangu, atalala mji wa Arusha au atalala Moshi au atalala eneo gani kabla hajapanda Mlima wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uchumi wa dunia sasa hivi umedorora kila mahali na kwa kuwa kila nchi inakumbatia vivutio vyake kwa ajili ya kuboresha uchumi wa Taifa lake.

Je, Serikali haioni kwamba huu uongo unaorudiwa kila mara kwamba Mlima wa Kilimanjaro uko Kenya, ni vyema sasa Serikali ikatoa tamko rasmi hapa ili ieleweke kwamba Mlima huu uko Tanzania na sio mahali pengine popote?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Mlima wa Kilimanjaro ni maarufu sana. Kila upande ikiwa ni pamoja na upande wa Kenya wanajaribu kusema kwamba Mlima huu uko kwetu, Tanzania. Huko nyuma Kenya walikuwa wanasema kabisa kwamba Mlima wa Kilimanjaro uko Kenya na Serikali ilipowabana katika dira za Kimataifa wakaacha kutumia huo usemi. Wanachokisema sasa hivi wanasema "Njoo Kenya utapanda Mlima wa Kilimanjaro". Na ni kweli mtu atakapofika Nairobi anaweza akaingia kwenye magari akaja Kilimanjaro akapanda mlima atakuwa hajasema uongo wa aina yoyote.

Serikali inachosisitiza kwanza kuanzia taasisi zake zote zilizo chini ya Wizara na chini ya Serikali tuhakikishe tunainuka kuutangaza Mlima wa Kilimanjaro. Kwa sababu kama anavyosema Mzee Ndesamburo ndio wa kwanza unaotuletea kipato, lakini ndio wa kwanza unaoamsha hisia za watu duniani, watu wakisikia Kilimanjaro kuna hisia

zinawakuta. Korea Kusini nilienda wana wimbo maalum uliotungwa na mtunzi baada ya kupanda Mlima Kilimanjaro na ni moja wa wimbo ambao kwa kweli ukiimbwa watu wote wanaanza kusakata rumba.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba wadau wa utalii ikiwa ni pamoja na wamiliki wa mahoteli ya kitalii nchini ikiwa ni pamoja na wamiliki wa Makampuni ya Kitalii tunawaomba na tunawasihi.

Saa imefika kwa Watanzania kuwa *dynamic*, Watanzania kuwa *aggressive* na kwa Watanzania kutokuogopa kwamba mtu atasema mlima uko kwake kwa sababu dunia nzima inajua mlima Kilimanjaro uko Tanzania. Tufanye kazi ya kuvutia wageni wapitie katika Mlima wetu wa Kilimanjaro wakijua uko Tanzania.

SPIKA:Mheshimiwa Waziri jengeni na hoteli pale *Airport* kwa sababu watu wanatembea usiku. Hilo tunaongea kwa sababu hata kiwanja tuliwahi kuwapeni cha kujenga hoteli kubwa pale.

Na. 210

Barabara ya Nyololo – Igowole- Mtwango - Mgololo

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Nyololo – Igowole – Mtwango – Mgololo kama ilivyokwisha kubaliwa katika mwaka 201'2/2013?

(b) Je, kwa nini ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami usianze mara moja ili kurahisisha usafiri wa bidhaa bila matatizo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyololo – Igowole – Mtwango – Mgololo yenye urefu wa kilomita 80.4 ni barabara inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuifanyia Upembuzi yakinifu na Usanifu barabara ya Nyololo – Igowole – Mtwango – Mgololo katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 ikiwa ni maandalizi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Spika, taratibu za kuanza ujenzi wa barabara hiyo zitaanza baada ya kazi ya usanifu kukamilika na pia itategemea upatikanaji wa fedha. Aidha, kipaumbele kwa sasa ni kumaliza kwanza kujenga kwa lami barabara kuu katika maeneo mbalimbali ya nchi.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa jibu zuri la Naibu Waziri, napenda niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri atakuwa tayari kufika katika vijiji husika ili kutoa elimu ya kutolipwa au kulipwa kwa wale waliojenga nyumba jirani na barabara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakubali kwamba nitafika kuwaelimisha wananchi kwamba ni wapi nyumba zao kama wako ndani ya hifadhi ya barabara hawatalipwa. Lakini kama barabara imewafuata watalipwa na tunaweka alama za aina mbili. Kwanza kuna alama "X" nyekundu hii inaonyesha kwamba wewe uko ndani ya barabara kwa hiyo hutalipwa, inabidi upishe hii barabara ya lami ambayo Mheshimiwa ameifuatilia kwa bidii sana tuweze kujenga. Lakini kama umewekewa alama ya "X" ya kijani Serikali itakulipa kabla ya kazi ya ujenzi haijaanza.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa vile barabara ya Lujewa – Madibira - Mufindi imekuwa ikipangiwa Bajeti kila mwaka, lakini ujenzi wake unaahidiwa hauanzi, nataka kujua je mwaka huu katika fedha ambazo zimetengwa ni shughuli zipi zitaanza ili wananchi wa Mbarali waweze kujua?

SPIKA:Hilo swali ni jipya sana lakini ebu jaribu kujibu, labda kwa sababu ya ukaribu. Ukiuliza swali ambalo ni jingine utegemee jibu sio sawasawa sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara ya Lujewa Mafinga tumeielezea kwenye mpango wa Bajeti ambayo sasa siwezi kukumbuka ni fedha ngapi zimewekwa, lakini tutaongea nje nitamwelewesha vizuri fedha zile ni kazi gani itafanyika. *(Makofi)*

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba kwa wananchi ambao walifuatwa na barabara watalipwa fidia.

Sasa mimi nina kesi kule Mwanza hii barabara ya Musoma maeneo ya Igoma kuna wananchi barabara iliwafuata miaka nenda rudi na mpaka leo bado wanadai fidia mpaka sasa hawajapewa. Sijui kauli ya Wizara inasemaje watakuja kulipwa lini na wameshafuatilia sana?

SPIKA: Wewe uliza swali la sera tu la kutengeneza barabara ndio atakujibu. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali hiyo sera ya alama zenu za barabarani.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama kuna kesi ambayo kuna watu wanastahili kulipwa na hawajalipwa basi naomba tuwasiliane tuweze kushughulikia suala hilo kulingana na taratibu zilizopo.

Na. 211

Ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Chunya - Makongolosi

MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA) aliuliza:-

Mwaka 2008 Serikali ilianza ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi kwa kiwango cha lami lakini mpaka hivi sasa hakuna hata mita moja ya lami:-

Je, Serikali inawambia nini wananchi wa Mbeya na Chunya kuhusu ujenzi wa barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina wa barabara ya Mbeya – Makongorosi yenye urefu wa kilomita 115 ulikamilika mwaka 2006, kwa kutumia fedha za ndani.

Utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii uligawanywa katika sehemu tatu ambazo ni sehemu ya kwanza toka Mbeya hadi kijiji cha Lwanjilo yenye urefu wa kilomita 36; sehemu ya pili toka Kijiji cha Lwanjilo hadi Mjini Chunya yenye urefu wa kilomita 36 na sehemu ya tatu toka Chunya hadi Makongorosi yenye urefu wa kilomita 43.

Mheshimiwa Spika, awali ujenzi wa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo kilomita 36 ulianza mwezi Septemba 2007 na ulitegemewa kukamilika mwezi Machi 2010. Kwa bahati mbaya mnamo tarehe 29 Aprili, 2009, wakati utekelezaji wa mradi ukiwa umefikia 27% tu, Mkandarasi aliyekuwa akifanya kazi ya ujenzi huo, Kundan Singh *Construction Ltd.* toka nchini Kenya alisitisha mkataba na kutelekeza mradi kinyume na taratibu za mkataba.

Baada ya mkataba wa Mkandarasi wa awali kuvunjika, mnamo tarehe 17 Desemba 2010, TANROADS ilisaini Mkataba mpya na Mkandarasi aitwaye China *Communications Construction Co. Limited* toka nchini China.

Mkandarasi alikabidhiwa eneo la mradi tarehe 26 Januari, 2010 na muda wa mkataba ni miezi 24.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi kwa ujumla umekuwa wa kusuasua kutokana na matatizo mbalimbali yakiwemo ya upatikanaji wa fedha na uzembe wa Mkandarasi, kwa sasa tatizo hili limekwisha kwani Serikali mwishoni mwa mwezi Juni 2012, imemlipa Mkandarasi kiasi cha shilingi 5,287,245,181.00 alichokuwa anadai. Baada ya malipo haya Mkandarasi anapaswa kuendelea na kazi kulingana na Mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya pili toka Lwanjilo hadi Chunya (*km. 36*), mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2009 kati ya Wakala wa Barabara na Mkandarasi *China Communications Constructions Co. Ltd.* toka nchini China, ambapo Mkandarasi alianza kazi rasmi tarehe 5 Agosti, 2009 na muda wa utekelezaji ni miezi 27. Mkandarasi wa barabara hii pia amelipwa kiasi cha shilingi 2,760,284,287.00 alizokuwa anadai. Hivyo anapaswa kuendelea na kazi kulingana na Mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu iliyobaki ya Chunya – Makongorosi yenye urefu wa kilomita 43, kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kimetengwa katika Bajeti ya 2012/2013 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, jumla ya shilingi bilioni 8.145 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mbeya hadi Chunya (*km. 72*). Serikali inawaahidi wananchi wa Mbeya kuwa barabara hii sasa inaendelea kujengwa kama tulivyoahidi kwenye Bajeti

ya mwaka 2012/2013 na itakamilika katika mwaka wa fedha 2013/2014.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu yake mazuri ninaomba kumwuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Waziri amekiri kwamba utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukiendelea kwa kusuasua kutokana na uzembe wa Makandarasi.....

SPIKA: Mbunge kijana Mheshimiwa Salim rudi ulikotoka, naomba urudi ulikotoka. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Hilda Ngoye endelea.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuanza tena.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mradi huu umekuwa ukitekelezwa kwa kusuasua kutokana na uzembe wa Makandarasi lakini vilevile kwa Serikali kutotoa fedha kwa wakati zilipohitajika.

Je, Serikali sasa iko tayari kuhakikisha kwamba inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu katika kipindi hiki ili mradi huu ukamilike katika muda uliopangwa na kujenga imani ya wananchi wa Mbeya kwa Serikali yao?

Kwa kuwa eneo la Chunya Makongorosi limepewa fedha katika kipindi hiki. Je, ni lini Mkandarasi atatangazwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane naye kwamba tutajipanga kuweza kufuatilia kwa ukaribu sana Makandarasi hawa ili yasijitokeze haya yaliyotokea nyuma na Serikali inajipanga kwamba fedha ambazo Makandarasi wanahitaji ziweze kupatikana kwa wakati ili wasisimamishe kazi.

Swali la pili, ni lini Mkandarasi ataanza. Kama nilivyosema kwamba tumeshatenga fedha tayari kwa ajili ya maandalizi. Kwa hiyo kitu cha kwanza ni kutangaza tenda na tukishatangaza tenda tutafanya uchambuzi wa tenda zile na Mkandarasi kwa hiyo muda ukifika tutawatangazia wananchi kwamba lini Mkandarasi ataanza kazi hiyo.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa kuna msemo wa Kiswahili unaosema "Unapomwona Jumbe ni hapo hapo unapotoa salamu". Naomba niulize swali moja.

Je ni lini Serikali itakuja kutengeneza barabara ya Kisarawe inayoanzia Mpuyani mpaka Msanga? Kwa sababu hili ni agizo lililotolewa na ahadi ya Mheshimiwa Rais mwaka 2005. Baada ya misimu ya mvua Serikali inaingia hasara ya kuchonga barabara kwa nini wasitumie fedha hizo wanazochonga barabara kila baada msimu wa mvua kuongeza japo kilomita moja barabara ya Kisarawe?

SPIKA: Barabara ya Kisarawe hajui, isipokuwa barabara kuwekewa lami ndiyo jibu. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi ni kutoka Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo kuna kazi mbalimbali ambazo tumeainisha. Kwa hiyo, kuna matengenezo ya kawaida, kuna matengenezo maalum kwa hiyo siwezi kupata *details* kujua katika barabara ile ni kitu gani kinafanyika na wapi. Lakini matengenezo yatafanyika ili barabara hii iweze kupitika wakati wote wa mwaka. (*Makofi*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea uzembe wa makandarasi na kwa kuwa makandarasi wanaposaini mikataba hii na Serikali ni suala la kisheria na lina hatua kuu tano za kuzingatiwa.

Je, uzembe huu walioufanya upande wa pili ambao ni wa makandarasi Serikali iliweza kwa mujibu wa Sheria ilipoteza kiasi gani au tulipata fidia kiasi gani kutoka kwa makandarasi hawa walioufanya kazi ya uzembe kule Mbeya?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba katika kuchelewesha kazi huwa inatokea mkandarasi hatekelezi kulingana na mkataba ambao amepewa. Mara nyingine unamwambia aanze labda tarehe kumi anachelewa kuanza. Sasa ukichelewa katika Mkataba ziko penalti anakatwa kulingana na kiasi cha fedha kulingana na kosa analokuwa amelifanya.

Lakini kwa huyu mkandarasi wa Mbeya Lwanjilo ilibidi twende kwa *arbitration* kwa sababu yeye aliamua kuacha *site* kwenye mataa na akaamua kuondoa kwa sababu zake mwenyewe. Sasa hiyo nayo ni issue ambayo ilibidi lazima twende kwa *arbitrator* ili tuweze kuona ni adhabu ipi kupewa huyu mkandarasi.

Na. 212

Ukosefu wa Majisafi na Salama - Kibaha

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Mji wa Kibaha ni mojawapo ya Miji midogo inayokua kwa kasi ambapo bomba kuu la maji linalosimamiwa na DAWASCO linapita, lakini zaidi ya 70% ya wakazi wake hawana maji safi na salama ya kunywa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hao maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mji wa Kibaha unapata huduma ya maji kutoka mtambo wa maji wa Ruvu Juu ulioko eneo la Mlandizi mkoani Pwani. Huduma ya maji hupatikana kwa siku mbili kwa wiki, isipokuwe eneo la Mkoani ambalo hupata maji kwa siku tano za wiki kwa wastani wa saa 12 kwa siku. Mtandao wa mabomba ya usambazaji, katika mji wa Kibaha, unakadiriwa kufikia asilimia 80 baada ya mradi

wa kupanua mfumo wa mabomba ya usambazaji uliokamilika mwaka 2010 kwa kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 300 na kuwaunganisha wateja wapatao 8,000.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma ya maji katika mji wa Kibaha na maeneo yote yanayopata maji kutoka mtambo wa Ruvu Juu, Serikali kupitia ufadhili wa Serikali ya India, iko katika hatua za mwisho kukamilisha usanifu kwa ajili ya upanuzi wa mtambo huo na baadaye ujenzi utaanza na kukamilika mwezi Desemba 2014. Ujenzi huo utakapokamilika uwezo wa uzalishaji wa maji katika mtambo utaongezeka kutoka lita milioni 82 za sasa kwa siku hadi lita milioni 196 kwa siku na huduma ya maji itaongezeka kutoka saa 12 za sasa kwa siku hadi saa 24 kwa siku.

Aidha, mtandao wa mabomba ya usambazaji maji utapanuliwa hadi kwenye maeneo yasiyo na huduma.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mji huu wa Kibaha maeneo ya Vikawe Bondeni, Vikawe Shuleni maeneo ya viziwaziwa, maeneo ya Sovu na hata Kidenge hayana maji kabisa na wananchi hawa wanatumia maji machafu na sio salama kwa kuchimba visima vidogovidogo kwa kutumia mkono; na kwa kuwa sasa mradi huu unaelekea kwenda kukamilika mwaka 2014 na kwa kuwa Mji wa Kibaha na wakazi wake hawana uwakilishi wa DAWASCO na DAWASA, swali la kwanza

Jje, kuna hatua gani sasa Serikali inazichukua za dharura kuwasaidia wananchi hawa waweze kupata maji safi wakisubiri mradi huu kukamilika?

Swali la pili, Serikali ina mpango gani kwa muji huu unaokuwa kwa kasi kwa kupitia Mto Ruvu kuhakikisha kwamba sasa na wenyewe unapata mamlaka yake ili kuweza kuhudumia wananchi ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana kwa namna ya pekee anavyofuatilia miradi ya maji katika Jimbo lake la Kibaha Mjini. Kuhusu hali ya maji katika vijiji alivyovitaja kwamba wakati huu wanaposubiri mpango huu wa kutoa maji Ruvu Juu kwenda mjini ambao utakamilika mwaka 2014 Desemba nashauri mambo yafuatayo.

Kwanza tumesambaza kwenye pegion hole kile kiwango cha fedha ambacho kimeongezeka ambayo Mheshimiwa Waziri aliisema wakati wa hotuba hapa kwamba kuna vijiji viwili vitakavyoongeza katika kila Halmashauri. Kwa Kibaha mjini *ceiling* ya kwanza ilikuwa ni milioni 506.7/- na *ceiling* mpya sasa hivi ni milioni 890.8.

Kwa hiyo tunashauri hilo ongezeko hilo la milioni 300/- walitumie kwa ajili ya uchimbaji visima ikiwa ni hatua ya dharura ya kuwasaidia hawa wananchi. Lakini hatua ya pili, DAWASCO wanafanya kazi ya kupunguza upotevu wa maji. Kwa hiyo, hatua hii itakapokuwa imekamilika itasaidia upatikanaji maji kwa wingi zaidi na hivyo itapunguza mgao ambo sasa hivi ni siku mbili na penyewe inawezekana siku za upatikanaji maji ukaongeza.

Kuhusu swali la pili ni kwamba ili mji uweze kuwa mamlaka kigezo kimojawapo cha kwanza ambacho ni muhimu ni pale wanapokuwa na vyanzo vyao vya maji. Kama unavyoona kibaha hawana vyanzo vyao vya maji. Wanatumia vyanzo vya maji ambavyo vimetengenezwa na DAWASA na vinaendeshwa na DAWASCO. Kwa maana hii huwezi kuruhusu mamlaka ikaweza ikaendesha ndani ya mamlaka nyingine. Tunachoweza kukifanya hapa ni kwamba ni lazima tuone uwezekano wa wananchi wa Kibaha Mjini wawe na uwakilishi kwenye Bodi ya DAWASCO ili waweze kuwasemea wananchi wao kuhusu suala zima la maji kama ilivyo kwenye Bodi ya DAWASA ambako tuna mwakilishi Mheshimiwa Makilagi ndiyo mwakilishi wa Bodi ya DAWASA. Kwa hiyo hata kwenye Bodi ya *DAWASCO* itabidi tuangalie uwezekano wa kuwa na mwakilishi ambaye ataseme Kibaha ambao ni watumiaji wakubwa wa maji.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. kwa kuwa Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maji kwa kutegemea wafadhili na kwa kuwa hakuna mtu yoyote anayeweza akakupa kitu chake bure bila kutegemea faidi kubwa zaidi. Sasa ni lini Serikali itazingatia hili na ianze kutekeleza miradi ya maji kwa kutegemea fedha za ndani?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali imeshachukua hatua tulisema kwenye Bajeti yetu kwamba katika mwaka 2011/2012 Serikali ilitenga fedha za ndani bilioni 41/- lakini katika Bajeti hii Serikali imetenga bilioni 140/- inaonyesha wazi kwamba dhamira ya Serikali ni kuongeza fedha za ndani ili kuweza kutekeleza miradi ya maji kwa fedha zetu sisi wenyewe.

Upelekaji wa Umeme Vijijini vya Jimbo la Karagwe

MHE. GOSBERT B. BLANDES aliuliza:-

Serikali imeanza kupokea umeme kwenye vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi, Rugu, Bujala na Ihembe II na kuviacha vijiji vya Rukale, Rubake, Misha, Ruhita, Kibogoizi na vitongoji vya kashamba na Rwanda kiji cha Ihembe II; na kwa sababu Mheshimiwa Rais mwaka 2010 aliahidi umeme Tarafa yote ya Nyabionza kupitia vijiji vya Rukole na vijiji vya Nyakaiga, Chamuchuzi, Kandegeho, Kanywamagana na Bukangara.

Lakini hakuna kilichofanyika licha ya nguzo za umeme zilizowekwa maeneo ya Kituntu na Rwambaizi takribani miaka mitano sasa:-

(a) Je, ni lini umeme utapelekwa vijiji vya Rukale, Kibogoizi, Rubale, Misha, Ruhita, Vitongoji vya Kashambi, Rwanda katika kijiji cha Ihembe II?

(b) Je, ni lini umeme utapelekwa kwenye vijiji vyote vya Taarifa Nyabiyonza kupiyia vijiji vya Rukole, Rularo na Kiruruma?

(c) Je, ni lini umeme utapelekwa Kata za Kituntu, Chanika, Kanoni na Igurwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vijiji vya Rukale, Kibogoizi, Rubale, Misha na Ruhita vipo katika orodha ya miradi ya Umeme (*REA*), miradi ambayo itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka huduma ya umeme Taarifa ya Nyabionza Chamuchuzi, Kandegesho, Kanywamagana na Bukangara kupitia vijiji vya Rukole, Rularo na Kiruruma utekelezaji awamu ya kwanza unaendelea na unatarajia kukamilika mwezi Agosti 2012. Aidha awamu ya pili itaanza mwaka wa fedha 2012/2013 itahusisha kupeleka umeme kwenye vijiji vya Kata ya Nyabionza Nyaishozi vikiwemo vijiji vya Nyakaiga, Ahakaishaka Nyakagoyegoye Chabalisa, Kamagambwa A, B na C, Nyakisa Karongo pia Umurusimbi Nyakatundu, Nyakaiga, Lukole na Nyakahanga kwa upande wa Bugene. Makadirio ya gharama za utekelezaji wa mradi huu ni jumla ya shilingi bilioni 1.5.

(c) Mheshimiwa Spika, Kata za Katuntu, Chanika, Kanoni, Igurwa pamoja na Vijiji vyake vitapata umeme kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na utekelezaji wa miradi hiyo utaanza mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha kazi zitakazofanyika katika miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa umeme wa njia kubwa ya msongo wa KV 33 yenye urefu wa kilometa 25.8, ujenzi wa umeme wa njia ndogo wa KV 0.4 yenye urefu wa kilometa 18, ufungaji wa *transfoma saba (7)* zenye uwezo wa *KVA 50 transfoma moja* yenye ukubwa wa *KVA 100* na *transfoma moja* ya ukubwa *KVA 200*.

Makadirio ya gharama za utekelezaji wa mradi huu ni jumla ya shilingi bilioni. 1.9.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Lakini kabla sijauliza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na kwa jinsi anavyojitahidi sana kujibu vizuri hapa Bungeni kama vile ana miaka zaidi ya kumi kazini.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna mradi unaoendelea katika Tarafa wa Nyaishozi kwa vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi pamoja na Ihembe lakini mradi huu pamoja na kupokelewa vizuri lakini una tizo moja kwamba umeme haujaenda ndani kwa wananchi waliko. Mradi huu umepita barabani na wananchi wengi wanalalamika.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unasemaje kuhusiana na hilo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa kunipongeza asante sana ni watu wachache wanaoweza kumpongeza mtu lakini nakushukuru sana.

Mradi ulioutaja wa umeme kwenda tarafa ya Nyaishozi katika vijiji ulivyovitaja ambao unaendelea na kwamba bado unaacha pembeni baadhi ya maeneo au vijiji unavyodhani ni muhimu kwa kweli vingeweza kupatiwa umeme katika awamu hiyo.

Ninachoomba tu ni kwamba pengine ni vizuri tukaonana, uje ofisini tujaribu kuangalia upya kwa ile miradi inayokuja kutekelezwa 2012/2013 itakayoanza tuone tunaweza tukafanya marekebisho gani pengine inaweza ikatusaidia kuliko nikitaka kukujibu moja kwa moja.

Na. 214

Msimu wa Kilimo Cha Vuli – Bonde la Kiru

MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Msimu wa Kilimo cha Vuli unaanza kwenye maeneo ya Bonde la Kiru ambapo wananchi wa maeneo hayo walikumbwa na mgogoro baina yao na wawekezaji ambao umesababisha hasara na njaa kutokana na wananchi kushindwa kulima katika msimu uliopita:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mgogoro huo na maandalizi ya kilimo kwa msimu huu kwa wananchi wa Bonde la Kiru?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa mgogoro baina ya wakulima na wawekezaji katika Bonde la Kiru. Katika kushughulikia mgogoro huo mwezi Februari, 2011 Waziri Mkuu aliagiza Mawaziri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI na Uwekezaji na Uwezeshaji, Wizara ya

Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi watembelee Mkoa wa Manyara hususan Bonde la Kiru ambalo limekuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya wakulima wakubwa (wawekezaji) na wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, timu hiyo ilibaini kuwa mgogoro uliopo unahusu kugombea ardhi kati ya wakulima wakubwa na wakulima wadogo. Chimbuko la mgogoro huo ni umilikiswaji wa ardhi kwa wadau hao uliofanywa na watendaji bila kuzingatia umilikishwaji uliokuwepo awali.

Aidha vijiji vilianzishwa katika maeneo ya mashamba bila kufuta hati za mashamba husika zilizokuwepo na baadhi ya wakulima wakubwa pia walimilikishwa mashamba bila kutambua kuwepo kwa Hati za Vijiji vilivyoanzishwa katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatambua kwamba mgogoro huo hauleti tija kwa upande zote mbili. Aidha taarifa niliyonayo ni kwamba tayari yamefikiwa makubaliano baina ya wakulima na mwekezaji wa *Kiru Valley Estate*, hali ambayo itawezesha suala hili kushughulikiwa nje ya Mahakama kwa haraka na hivyo kuepusha mgogoro.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kwa kuwa huu mgogoro unachukua sasa takribani miaka 25 mpaka leo haupatiwi uvumbuzi . Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Naibu Waziri ameeleza kwamba huu mgogoro chanzo kikubwa ni watendaji wa Serikali kutokuwa

waaminifu kufanya *double allocation*. Kwamba vijiji vilikuwepo lakini kuna baadhi ya wakulima wakaja wakapewa tena mashamba lakini vijiji viliwekwa juu ya mashamba pia. Yaani hizo GN zinatolewa kwa watu wanaomiliki hayo mashamba.

Naomba nifahamu, hao watendaji wamechukuliwa hatua gani mpaka sasa?

Swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Babati ina mashamba takribani 11 ambayo hadi sasa umiliki wake haueleweki. Mfano shamba la *Rivaku*, shamba la *Breweries* ambalo linapakana na vijiji vya Sigino Endasago na maeneo ya Kiru na kwa kuwa mwekezaji huyu yupo tayari na wakulima wote kwamba mwekezaji aachie miongoni mwaka hekali 3,003 aachie takribani heka 2300 awaachie wale wakulima lakini wakulima wale wako tayari kuhama kwenye mashamba haya ambayo mpaka sasa yanakodishwa tu. Kwa nini Serikali haitaki kumaliza mgogoro huu na kuufanya *re-allocation* wa wakulima hao ili huu mgogoro usiendelee?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:
Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nisahihishe tu kwamba tatizo sio la miaka 25. Haya mashamba wagiriki wapo pale tangu mwaka 1920, miaka 1950 ndiyo zikaja Hati za mara ya kwanza, mwaka 1968 waka *abandon* yakaenda *NAFCO*, *NAFCO* mwaka 1980 ikafilisika ikashindwa kuyaendesha watu wakavamia pale.

Kwa hiyo kuna songombingo. *LART* ikaja pale ikagawa yale mashamba vijiji vikaingia wakati wa *operation* vijiji, vijiji vikapenya humo humo. Kwa hiyo ninachosema ukiaanza

kutafuta watendaji ambao walishughulika na hili jambo kuna wengine tutaenda kuwatafuta tangu miaka 1950 hawatapatikana.

Maana yangu ni kwamba hili tatizo sasa hivi lina ugumu kwa sababu viongozi wa kisiasa nao tunahusika katika kuchochea jambo hili. Hiyo ndiyo tatizo kubwa na lazima tuambizane ukweli. Mathalani mwaka jana kuna mashamba yamechomwa pale. Kuna watu wameuawa, mahindi yamekuwa *destroyed* kwa maslahi ya nani?

Mheshimiwa Waziri ametoa Mawaziri wanne wametoka hapa na wengine ni wenyeji wa Mkoa wa Manyara na Mkuu wa Mkoa Parseko Kone akaambiwa shughulikia suala hilo wakati huo anakaimu na Mheshimiwa Jitu Soni naye alikuwepo katika sehemu ya *delegation* hiyo. Wamekwenda pale wameondoka wamerudi nyuma mtu kauawa.

Kwa hiyo, hili linakuwa gumu mimi ninasema kwa kuwa Serikali tumeonyesha dhahiri kushughulikia tatizo hili mimi ninakuhakikishia Mheshimiwa kwamba tutarudi tena. Kunaonekana kwamba kuna uelewa fulani ambao unataka kukubaliwa baina ya wawekezaji alivyosema Mheshimiwa Paulina ni kweli nina barua ya Mheshimiwa Diwani hapa anakiri kwamba kuna maelewano yanataka kupatikana sisi tutakwenda kusimamia pamoja na uongozi wa Mkoa lakini Mheshimiwa Mbunge Jitu Soni na nyinyi wadau wa Mkoa wa Manyara mhusuke katika kupata ufumbuzi ambao utakuwa *lasting solution*.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba katika hilo pia nimejibu na hili suala la pili ambalo ni kweli analosema Mheshimiwa anataka kuachia ekari huku lakini na sisi wenyewe viongozi tuwasimamie wananchi ili tupate ufumbuzi wa kudumu na sisi tutakwenda kusimamia tatizo hili.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa jitihada ambazo inafanya lakini sisi kama wadau ambao tunahusika huko Babati tunaona bado ule mwendo wa kufanya kazi bado ni mdogo na inawanyima fursa wananchi wa Kirudiki ambao hata hati miliki za kimila wameshindwa kupata kwa sababu ya kuwepo kwa Hati ya Kimila. Wananchi wamewekwa pale na *operation* kijiji na *right of occupancy* iko pale lakini mapendekezo tunayoendelea kutoa kila mwaka bado hayafanyiwi kazi, tunaomba safari hii usuluhisho wa kudumu upatikane na yale mapendekezo ambayo tumependekeza yafanyiwe kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa pale ni suala la wale ambao wanatakiwa kuja kusaidia kutatua mgogoro wanageuka na kung'ag'ania maeneo kwa maslahi yao. Je, Serikali ngazi ya Taifa iko tayari kuingilie kati na ihakikishe kwamba tunapata ufumbuzi ili wananchi wapate haki yao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwanza ninaomba nitambue kazi anayofanya Mheshimiwa Jitu Soni katika kupata ufumbuzi lakini pia naomba niseme kuna Kamati ya Kitaifa chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina taasisi mbalimbali inafanyia kazi taarifa za wawekezaji na

matatizo ya wadau kwa maana ya wakulima yaani wananchi walioko pale.

Ni lazima tukubali kuwa na hawa wawekezaji nao siyo wote ni wakweli kuna wengine ndivyo sivyo kwa hiyo, naomba niseme kwamba kupitia hii Kamati ya Kitaifa sisi kwa upande wetu wa sekta ya kilimo tutachukua taarifa hizi na wawekezaji waliopitia kwetu na wakaenda ndivyo sivyo tutavunja mikataba hii maana haina maslahi kwa Taifa letu wala kwa wananchi. *(Makofi)*

Na 215

Uwekezaji Katika Sekta ya Viwanda vya Sukari

MHE. JUMA S. JUMA (K.n.y. SAID M. ZUBEIR) aliuliza:-

Uwekezaji katika sekta ya viwanda vya sukari bado haujaleta tija kwa kiasi kikubwa:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka wa kuanzisha viwanda vidogovidogo vya sukari ili kutengeneza ajira nyingi kwa vijana na kupunguza uhaba wa sukari pamoja na upandaji holela wa bei ya sukari?

WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Zuber, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sekta ya viwanda vya sukari bado

haijakidhi mahitaji hapa nchini. Hata hivyo, serikali kupitia Bodi ya sukari Tanzania inatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano (2011/2012-2015/2016) wa maendeleo ya sekta ya sukari unaohusisha pia wadau katika sekta hiyo. Lengo la mkakati huo ni kuliwezesha Taifa kujitosheleza kwa mahitaji ya sukari, kuongeza ajira na kuondoa umasikini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha maeneo ya ziada yanayofaa kwa kilimo cha miwa na uanzishwaji wa viwanda vidogo (*small scale sugar plants*) na vya uwezo wa kati (*mini sugar factories*) vya usindikaji wa miwa na kuzalisha sukari. Maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya viwanda vidogo vya sukari ni pamoja na Kilosa na Mwaya (Morogoro), Kiru (Manyara), Lumuma (Dodoma), Peramiho (Songea), Liuli (Mbinga), Amani (Tanga) na Kintinku (Singida). Maeneo mengine yaliyoainishwa kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya uwezo wa kati wa kuzalisha sukari ni Mahurunga (Mtwara), Pangani (Tanga) na Babati (Manyara).

Mheshimiwa Spika, chuo cha sukari cha Taifa (*National Sugar Institute (NSI)*) Morogoro kimeweza kutengeneza mashine ndogo ndogo zaidi ya mashine 5 zilishatengenezwa na kusambazwa Jimbo la Peramiho, Lumuma- Mpwapa, Same, Pemba, Jimbo la Bumbuli na kikundi cha akina mama wajane wa Ruaha (*Mshikamano Group*) ambao wanatumia mashine za chuo kuzalisha sukari. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya usindikaji wa sukari na kilimo bora cha miwa ambapo wanavikundi toka Kilosa, Kisanga, Kibondo, Kasulu, Kigoma Vijijini wameweza kupata mafunzo hayo mwaka huu, 2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya utafiti wa kina katika maeneo hayo pamoja na maeneo mengine nchini yanayoweza kufaa kwa uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati vya kuzalisha sukari.

Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wasaidie katika kuhamasisha wananchi katika viwanda vidogo vidogo vya sukari katika maeneo yatakayoibuliwa na ambayo yanafaa kwa kilimo cha miwa. Hatua hii, itasaidia kutengeneza ajira nyingi kwa vijana na kupunguza uhaba wa sukari na kudhibiti upandaji holela wa bei ya sukari nchini. *(Makofi)*

MHE. JUMA S. JUMA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali pamoja na mipango mkakati naweza kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na mipango hiyo je Watanzania wategemee lini utoshelezaji wa Sukari katika nchi yao?

WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa ina mikakati ya karibu aina tatu ya kuhakikisha kwamba tunajitosheleza katika uzalishaji wa sukari.

Kwanza, ni uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo ambao unafanywa na Chuo cha Taifa cha Sukari kikisaidiana na baadhi ya Halimshauri ya Wilaya na kituo chetu cha Nyumbu. Mantiki yake ni kuhakikisha kuwa vile viwanda vidogo vidogo vinawakuta wazalishaji wadogo ili wasindike miwa yao na kuzalisha sukari.

Pili Serikali inaingia kwenye mpango wa *SAGOT* ambao ni eneo ambalo litaendeleza mazao ya kilimo na mabonde kadhaa yameshateuliwa kwa ajili ya uzalishaji wa miwa.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kwamba tunajaribu kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha viwanda vilivyopo vinaongeza uwezo wa uzalishaji kwa maana ya *capacity* yao karibu ya 50% ya wanavyozalisha sasa ili kuhakikisha kuwa sukari inazalishwa kwa wingi.

Nne Serikali itajitahidi kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hasa utaratibu wa kupeleka umeme vijijini kuhakikisha umeme unapelekwa vijijini kuhakikisha viwanda vidogovidogo vinaanzishwa katika mkakati huu tunategemea kwamba katika miaka miwili au mitatu tuwe tunajitosheleza kwa sukari hasa kwa matumizi ya nyumbani.

Na. 216

Askari Polisi Kusumbuliwa Wakati wa Kufuatilia Mafao

MHE. HAMAD A.HAMAD aliuliza:-

Baadhi ya wastaafu wa Jeshi la Polisi husumbuliwa wakati wa kufuatilia mafao yao kwa kupewa visingizio vingi kama vile kupotea kwa mafaili na kadhalika.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwaondolea usumbufu wastaafu hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa muda mrefu kumekuwepo na ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu wa Jeshi la Polisi. Ucheleweshaji huo ulikuwa ukisababishwa na pamoja na mambo mengine, kutokupatikana kwa wakati kwa baadhi ya Nyaraka.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo hilo kwa hivi sasa Serikali imeboresha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za watumishi wa Jeshi la Polisi. Taarifa mbalimbali za watumishi wa Jeshi hilo zitatunzwa kwa njia ya mtandao (*TEHAMA*).

Program ya maboresho ya Jeshi la Polisi itarahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za mtumishi kama vile tarehe ya kuajiriwa, kuthibitishwa kazini, kibali cha kustaafu na tarehe ya kuingizwa kwenye malipo ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, sambamba na matumizi ya *TEHAMA* Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu wa kutoa nyaraka muhimu zinazohusiana na madai ya mafao ya wastaafu kwa watumishi wake lengo ni kuwasaidia wao na familia zao kufuatilia mafao yao kwa haraka. Ni imani ya Serikali kuwa na njia hizi zote zitasaidia kuondoa kabisa tatizo la ucheleweshaji wa mafao kwa wastaafu wa Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

MHE. HAMAD A. HAMAD: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, matumizi haya ya teknolojia hii ya *TEHAMA* yatasaidia kutunza kumbukumbu kwa wale ambao watataka kustaafu sasa na kwa sababu madai haya na malalamiko yako kwa wale ambao wameshastaafu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unawaambia nini wale ambao wana madai walishastaafu siku zilizopita juu ya kupata mafao yao?

(b) Kwa kuwa, mstaafu ni Mtanzania ambaye amewekeza muda wake na nguvu zake katika kulitumikia Taifa lake. Je, Serikali kwa kisingizio chochote cha kumcheleweshea mafao yake mstaafu huyu haioni kwamba inamdhalilisha yeye na familia yake?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Nomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kabisa kuwa *TEHAMA* itawasaidia wale ambao bado hawajapata kadhia hii lakini taratibu za kawaida bado zinaendelea kuzitafuta nyaraka ambazo zimekosekana kutoka kwenye taasisi moja hadi nyingine kwa sababu nyaraka mara nyingi zinakuwa katika maeneo tofauti. Kwa hiyo, ninawahakikishia wale ambao bado wanadai mafao yao kuwa jitihada zitaendelea kuhakikisha kwamba mafao yao yanapatikana haraka iwezekavyo.

(b) Swali la pili ni kuhusu kukosa mafao kuwa ni udhalilishaji ninaomba nitofautiane kidogo na Mheshimiwa

Mbunge kwamba kwa mtazamo wangu ni kwamba huu siyo uzalilishaji isipokuwa ni kasoro ambayo inaleta usumbufu na tunahitaji kuishughulikia. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tatizo hili hivi sasa linapungua na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba matatizo haya yataisha hivi karibuni.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumechukua dakika ambazo siyo za kipindi hiki lakini maswali yamekwisha. Ningependa tutambue wageni tulio nao ndani ya Bunge na katika ukumbi huu, tunao wageni kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bwana Mbarack Abdulwakil naomba alipo asimame yupo na Bibi Mwamini Malema yeye ni Naibu Katibu Mkuu mbona hampigi makofi na jana mlisema kuwa wako wanaume tupu leo yupo mwanamke. (Makofi).

Waliopo ni pamoja na *Inspector wa General* wa polisi Bwana Said Mwema, Bwana Magnus Ulungi Kamishna wa Mkuu wa Uhamiaji, Bwana Fidelis Mboya Kaimu Kamishna na Jenerali wa Magereza, Bwana Pius Nyambacha Kaimu Kamisha jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Bwana Dickson Maimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Bwana Clodivick Mtweve, Kamishna wa Polisi Utawala na Rasilimali, Bwana Musa Ali Musa Kamishana wa Polisi Zanzibar, nitaomba wafuatao wasimame kwa pamoja.

Wapo Wakurugenzi Wakuu wa Vitengo na Maafisa kutoka Makao Makuu ya Wizara wasimame pale walipo kwa pamoja. Wengine pia wasimame kwa pamoja Maafisa Watendaji wa Idara ya Polisi na wapo pia Maafisa Watendaji, wasimame kwa pamoja Idara ya Magereza,

Maafisa Watendaji wote Idara ya Uhamiaji, Maafisa Watendaji Idara ya Zimamoto na Uokoaji waliko wasimame. Ninawashukuruni sana na karibuni leo ni siku yenu na tutakwenda kwa muda wa siku moja na nusu.

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Vicent Nyerere, ambao ni familia yake ikiongozwa na Mke wake mpendwa Bi. Helen Nyerere, huyo mke mpendwa yuko wapi ahsante sana. Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Philipa Mturano, ambao ni wafanya biashara kutoka *China National Heavy machinery Corporation*. Hawa sijui jinsi ya kutamka majina kama ni Bwana au bibi, yuko Bwana Fang Yong, Helen Hei, Thiobert Maima huyo siyo Mchina huyu au na wewe Mchina.

Pia, kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu ambao wanaongozwa na Ndugu Barnabas Luis Siame wako wapi hawa wageni watatu. Halafu kuna Dkt. Zaveli Rweitama ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi Mstaafu na pia Mwanafalsafa mahiri hapa nchini asimame huyo ahsante sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira ambao ni Ndugu Amina Malumbo, Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT). Pia yupo Ndugu Shamimu Mgayu Binti wa Amina Mambo, huyu ni Mjumbe na Binti yake ahsanteni. Halafu wageni walioko hapa Bungeni kwa ajili ya mafunzo hawa ni wageni 17 sasa sijui wanatoka wapi hawa wanaongozwa na Peter Chacha wako 17. Sijui wanatokea wapi sasa naomba wasimame hao watu 17 na huyo Bwana Peter Chacha. Tuna wageni watatu (3) sijui wanatoka wapi wakiongozwa na Mrs. Hawa

Lembeli sasa hawa watatu wasimame sijui ni akina nani wanaoongozwa na Bibi Hawa Lembeli.

Kuna wageni 25 ambao ni wana kwaya wa Kigarama Kanyigo Wilaya ya Misenyi na Wenyeji wao kutoka upendo kwaya ya hapa Dodoma. Naomba wale wa Misenyi wasimame kwanza na wenyeji wenu kwaya ya upendo wasimame okay. Kumbe ni group moja karibuni sana na poleni na safari. Tuna wanafunzi 50 kutoka shule ya sekondari ya *City*, Dodoma wasimame walipo. Msome kwa bidii, tuna wanafunzi 30 kutoka shule ya sekondari Magoza ya Ilala Dar es salaam na hawa wasimame. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wanafunzi 100 kutoka chuo cha Elimu cha *Capital* kutoka Dodoma hawa wako wapi okay! Kumbe ni nyie karibuni sana. Tuna wanafunzi 50 kutoka shule ya sekondari ya Itungwa *Adventist* ya Morogoro karibuni sana, kuna wana madrasa 30 kutoka Itishamu Majengo Dodoma Mjini karibuni sana, nadhani wamekosa nafasi kwa sasa hivi.

Waheshimiwa Wabunge wakati huohuo tuna Sheikh kutoka Jimbo la Siha Mlewa Shaaban karibu sana. Nadhani amekosa nafasi. Kuna Mkurugenzi mkuu wa *Image for you* Ndugu Omar Ige. Wageni mlioko kwenye ukumbi wetu tunawakaribisha, kama mmekosa nafasi ni bahati mbaya lakini Bunge ni kwa ajili ya watu wote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tuna matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa

saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Suleiman J. Zedi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa tano asubuhi hii, watakuwa na Kamati katika Ukumbi Na. 231, mtu ninayemtangaza kufanya kikao saa tano asubuhi maana yake nimempa ruhusa. Kwa hiyo huyu amepewa ruhusa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ambacho kitafanyika katika Ukumbi Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Kaimu Katibu wa Wabunge wa CHADEMA Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao chao kwenye ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, Wabunge wa CHADEMA mnatakiwa muwepo huko.

Waheshimiwa Wabunge mwisho wa matangazo, tunaendelea. Katibu tuendeleee na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunateua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Kumteua Mheshimiwa Pereira Ame Silima Mbunge kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Namshukuru kwa imani aliyoionesha kwetu na tunamhakikishia kwamba tutafanyakazi usiku na mchana kwa kushirikiana na Wataalam, Maafisa na Askari katika kutekeleza majukumu ya Wizara na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2010 ili kukidhi matarajio ya Rais na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi wa Jiji la Dar es Salaam kutokana na mvua kubwa iliyonyesha mwishoni mwa mwezi Desemba, 2011 ambayo ilisababisha mafuriko na hivyo

kuleta adha kubwa kwa wananchi vikiwemo vifo na uharibifu wa mali na miundombinu. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao kutokana na tukio hilo. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa ushauri wao na maelekezo yenye tija katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao walizozitoa mapema katika mkutano huu wa Bunge ambazo zimetoa mwelekeo wa bajeti ya Serikali na hali ya uchumi kwa jumla kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini, na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Usalama Nchini. Amani, utulivu na usalama wa wananchi ni mihimili mikuu ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kuongezeka kwa matishio ya uhalifu na kupungua kwa hali ya usalama wa raia husababisha kuathirika kwa mfumo mzima wa ustawi wa nchi katika nyanja mbalimbali na kwa ujumla hudhoofisha nguvu na jitihada za wananchi katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2011 makosa ya jinai makubwa na madogo 564,716 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi ikilinganishwa na makosa 543,358 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2010. Idadi ya makosa imeongezeka kwa asilimia 3.9. Kutendeka kwa makosa haya kwa kiwango kikubwa kunachangiwa na mmomonyoko wa maadili, tamaa ya utajiri wa haraka haraka, imani za kishirikina, tamaa ya maisha na umaskini. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau limeendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya aina mbalimbali ya kukabiliana na uhalifu nchini ukiwemo mkakati wa Ulinzi Shirikishi.

Mheshimiwa Spika, yapo baadhi ya maeneo hapa nchini ambayo kutokana na sababu zikiwemo za kijamii, kiuchumi na kisiasa yalikithiri kwa vitendo vya uhalifu vilivyosababisha uvunjifu wa amani na kuleta hofu miongoni mwa wananchi. Hali ya aina hii ilipojitokeza, Jeshi la Polisi lililazimika kuongeza nguvu na kuendesha operesheni kwenye maeneo husika. Katika mwaka 2011/2012, operesheni maalum ziliendeshwa katika Bahari ya Hindi kutokana na tishio la uharamia, kwenye majimbo ya Arumeru Mashariki na Igunga yaliyokuwa na uchaguzi mdogo wa nafasi ya ubunge, Mbeya kutokana na vurugu

za wafanyabiashara wadogo wadogo, Rufiji kutokana na vurugu za wakulima na wafugaji, Tandahimba kufuatia vurugu za wananchi kudai malipo ya korosho awamu ya pili, Zanzibar kufuatia vurugu za wafuasi wa kundi la UAMSHO, Songea kutokana na vurugu zilizosababishwa na uvumi wa kuuawa kwa waendesha pikipiki kwa imani za kishirikina na katika maeneo mengine. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi litaendelea kujiimarisha katika kufanya kazi za operesheni kwa mtindo wa Vikosi Shirikishi ili kukabiliana na matishio ya uhalifu yanayoikabili nchi yetu hususan ugaidi, uharamia, uhalifu unaovuka mipaka kama vile biashara ya dawa za kulevya, biashara haramu ya kusafirisha binadamu, uhamiaji haramu, wizi kwa kutumia mitandao ya TEHAMA, bidhaa bandia, biashara haramu ya silaha, uchafuzi wa mazingira na ongezeko la vifo na majeruhi kutokana na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma ya usalama wa raia na mali zao katika maeneo ya uwekezaji, mwezi Mei, 2012 Jeshi la Polisi ngazi ya Makao Makuu limeanzisha vitengo maalum vya kuratibu usalama katika migodi, ulinzi wa mazingira na usalama wa watalii. Kabla ya kuanzishwa kwa vitengo hivi huduma ya usalama katika migodi, maeneo ya utalii na ulinzi wa mazingira ilikuwa ikitolewa kwa kutumia vikosi vya Jeshi la Polisi vilivyopo katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Kazi ya awali iliyofanywa na vitengo hivi ni kuandaa muundo wa vikosi vitakavyoanzishwa na mikakati ya kuimarisha usalama wa maeneo hayo kwa kushirikiana na wadau wa sekta husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, makubaliano maalum ya kutoa huduma ya ulinzi katika benki za biashara na katika migodi ikiwemo inayomilikiwa na Kampuni ya Barrick Gold na Williamson Diamond yaliendelea kutekelezwa. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha uwezo wake wa utendaji kwa kuongeza weledi wa watendaji na vitendea kazi hususan pikipiki kwa ajili ya kuongeza wigo wa doria za Jeshi la Polisi hadi ngazi ya Kata/Shehia.

Mheshimiwa Spika, Vyanzo vikubwa vya ajali za barabarani hapa nchini ni pamoja na:-

- (i) Uzembe wa madereva, ukiwemo uendeshaji wa kasi usiozingatia sheria na alama za barabarani;
- (ii) Ubovu wa magari;
- (iii) Ubovu na ufinyu wa barabara zilizopo;
- (iv) Usimamizi usioridhisha wa usalama barabarani;
- (v) Ukosefu wa alama za barabarani; na
- (vi) Ongezeko la vyombo vya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani bado zinaendelea kuwaangamiza wananchi. Ajali hizi zimeendelea kupoteza maisha na kusababisha ulemavu wa kudumu na upotevu wa mali za wananchi. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2011 ajali za barabarani 24,078 ziliripotiwa katika vituo vya Polisi ambapo watu 4,013 walipoteza maisha na wengine 20,917 kujeruhiwa ikilinganishwa na ajali 24,926 zilizoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2010 ambapo watu 3,687 walifariki na wengine 22,064 kujeruhiwa. Idadi ya ajali ilipungua kwa asilimia 3.4.

Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine kama *SUMATRA*, *TBS*, *TANROADS* na Shule za Udereva limeendelea kuchukua hatua zifuatazo ili kudhibiti ajali za barabarani:-

(i) Kutoa elimu ya kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa watumiaji wa barabara;

(ii) Kuhuisha viwango vya adhabu kwa makosa ya usalama barabarani;

(iii) Kushirikisha wadau wa usalama barabarani katika kuhuisha mikakati ya kupunguza ajali za barabarani;

(iv) Kuendeleza doria za masafa mafupi na marefu katika kusimamia sheria za usalama barabarani;

(v) Kufanya ukaguzi wa magari;

(vi) Kutumia kamera za kutambua madereva wanaotumia mwendo kasi bila kuzingatia alama za usalama barabarani;

(vii) Kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya(viii) Kushirikisha jamii ili kupata taarifa za madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani; na

(ix) Wamiliki wa Mabasi kutakiwa kubandika kwenye Mabasi yao namba za simu za viongozi wa Polisi Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 Katika Kipindi cha 2011/2012. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina

malengo 10 ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kwanza ni kuendeleza mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Aprili, 2012 Jeshi la Polisi liliwahamasisha na kushirikiana na wananchi katika Ulinzi Shirikishi ili kudhibiti uhalifu ukiwemo uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo yao. Ushirikiano wa wananchi na vyombo vingine vya dola uliliwezesha Jeshi la Polisi kukamata watuhumiwa 10,384 wakiwa na jumla ya kilo 397.984 za dawa za kulevya za viwandani aina ya *Cocaine* kilo 140.547, *Heroine* kilo 257.437, *Mandrax* gramu 5 na kilo 63,480.738 za dawa za kulevya za mashambani. Dawa za kulevya za mashambani zilizokamatwa ni bhangi kilo 50,548.41 na mirungi kilo 12,932.328. Aidha, ekari 235 za mashamba ya bhangi ziliteketezwa katika Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotambuliwa kuingiza nchini dawa za kulevya ni vituo vya mipakani na nchi jirani, Viwanja vya Ndege, bandarini na vituo vya Mabasi yaingiayo na kutoka nchini. Maeneo ya usambazaji na utumiaji ni yale ambayo yana mkusanyiko wa watu wasiokuwa na ajira maalum maarufu kama "Vijiwe". Jeshi la Polisi litaendelea kubaini mtandao wa wahalifu wa ndani na nje ya nchi unaojikusisha na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini, kushirikiana na Shirika la Polisi la Kimataifa (*INTERPOL*) kupata taarifa za kiintelijensia kuhusu wasafirishaji wa dawa za kulevya na kukiimarisha Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Vyombo vya Ulinzi na Usalama cha kupambana na biashara ya dawa za kulevya kwa

kukiongezea rasilimali watu pamoja na vitendea kazi. Lengo la pili ni kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza. Tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu bado ni kubwa licha ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kukabiliana nalo. Tarehe 1 Aprili, 2012 idadi ya wafungwa na mahabusu waliokuwepo Magerezani ilifikia 37,676. Wafungwa walikuwa 18,068 na mahabusu 19,608 kama ilivyofafanuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 wafungwa 142 waliachiliwa huru kwa utaratibu wa *Parole*. Jumla ya wafungwa 693 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje kwa kutumia kanuni za kifungo cha nje za mwaka 1968. Vile vile wafungwa 1,080 waliachiliwa na Mahakama ili kutumikia kifungo cha nje chini ya Sheria ya Huduma kwa Jamii na wafungwa 3,803 walifaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2011 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru na wafungwa 2,973 waliachiliwa tarehe 26 Aprili, 2012 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 48 ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, hatua zingine zinazochukuliwa ili kupunguza msongamano ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu haki ya dhamana kwa watuhumiwa, Wakuu wa Magereza wa Mikoa kuwasilisha kwenye Kamati za Kusukuma Mashauri orodha ya mahabusu ambao kesi zao zimechukua muda mrefu kabla ya kukamilika, Jeshi la Magereza kuifahamisha Mahakama Kuu kila mwezi idadi ya mahabusu waliokaa gereza zaidi ya siku 60, upanuzi, ukarabati na ujenzi wa mabweni ya wafungwa na kuundwa kwa Kikosi Kazi chini ya uenyekiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo wajumbe wengine ni Jeshi la Polisi,

Jeshi la Magereza na Mahakama ili kushughulikia tatizo la msongamano Magerezani na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa. Lengo la tatu ni kuimarisha na kuboresha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinai ili kurahisisha uendelezaji wa kesi mahakamani. Kati ya Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 Jeshi la Polisi limetoa mafunzo ya Intelijensia na mbinu za kisasa za upelelezi kwa wapelelezi 511 na limepata vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kisayansi (*forensic*) katika Maabara iliyopo Makao Makuu ya Polisi.

Aidha, mchakato wa kuikabidhi Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kazi za kuendesha mashtaka Mahakamani umekamilika katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya katika Mikoa 22 ya Tanzania Bara na Mikoa mitano ya Zanzibar. Waendesha Mashtaka wa Polisi 120 waliokuwa wanafanya kazi za kuendesha mashtaka Mahakamani wamehamishwa na wamepangiwa kufanya kazi za upelelezi katika Mikoa mbalimbali nchini. Lengo la nne ni kuanzisha mpango wa kuwapatia askari nyumba bora za kuishi. Tathmini iliyofanywa na Jeshi la Polisi inaonyesha kwamba ili askari wote waweze kuishi kambini, zinahitajika kujengwa nyumba mpya zipatazo 32,114 katika Mikoa ya Kipolisi 33 ikiwemo Mikoa mipya ya Katavi, Njombe, Geita na Simiyu. Katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Polisi lilikamilisha ujenzi wa nyumba 30 za ghorofa katika Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa na kukamilisha ujenzi wa nyumba nane eneo la Uwanja wa Ndege Mkoani Arusha ambapo jumla ya askari 128 pamoja na familia zao walipata makazi katika nyumba hizo. Aidha, ujenzi uliendelea wa nyumba sita za ghorofa Mkoani Mwanza, nyumba sita za ghorofa Mkoani Mara, nyumba tatu za ghorofa Mkoani Kagera na nyumba nane Wilaya ya

Ludewa uliendelea. Ujenzi wa nyumba hizi utakapokamilika jumla ya askari 74 na familia zao watapatiwa makazi. Kwa upande wa Jeshi la Magereza ujenzi wa nyumba tatu umekamilika Gereza Singida na ujenzi wa nyumba mbili uliendelea Gereza Chato, nyumba moja Gereza Ngara na nyumba moja Gereza Magu.

Aidha, Idara ya Uhamiaji ilikamilisha ujenzi wa nyumba moja katika Kituo cha Rusumo na kukamilisha ukarabati wa nyumba nne Kibaha na nyumba nne Sirari. Ujenzi na ukarabati wa nyumba unafanyika kwa kadri uwezo wa fedha unavyoruhusu. Mheshimiwa Spika, lengo la tano ni kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa nchini. Hivi sasa Jeshi la Polisi lina jumla ya vituo 417 vya daraja A, B na C nchi nzima. Kwa kutumia vigezo vya Amri za Kudumu za Jeshi la Polisi, vituo vya Wilaya ambavyo ni daraja "A" vilivyopo ni 162, vituo vya Tarafa ambavyo ni daraja "B" vipo 91 na vituo vya Kata daraja "C" vipo 164. Ni azma ya Serikali kujenga vituo katika Tarafa 526 za Tanzania Bara na Majimbo 50 ya Zanzibar na hatimaye kufikisha vituo katika Kata 3,876 zilizopo nchini hatua kwa hatua kadri bajeti itakavyoruhusu. Kutokana na ufinyu wa bajeti, badala ya kujenga vituo vipya katika Tarafa Jeshi la Polisi limewapanga Wakaguzi 526 kuwa Wasaidizi wa Wakuu wa Polisi wa Wilaya wanaoshirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuzuia uhalifu katika Tarafa hizo.

Mheshimiwa Spika, lengo la sita ni kuwapatia wananchi mafunzo ya Ulinzi Shirikishi ili wawe tayari kujilinda katika maeneo yao. Lengo la Ulinzi Shirikishi ni kuiwezesha jamii kuishi maisha ya amani na utulivu katika maeneo yake. Serikali inazingatia ukweli kwamba kila raia anawajibika kwa ulinzi wake binafsi, familia yake, jirani yake na jamii kwa

ujumla tofauti na fikra potofu za baadhi ya watu kwamba usalama wa raia na mali zao ni jukumu la Jeshi la Polisi na viongozi wa Serikali pekee.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Polisi liliendelea kutoa mafunzo ya Ulinzi Shirikishi na kuanzisha mradi mpya wa Utii wa Sheria Bila Shuruti. Aidha, kupitia mikutano ya hadhara na vyombo vya habari, Jeshi la Polisi liliendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha utekelezaji wa miradi ya Ulinzi Jirani, Usalama Wetu Kwanza, Ukamataji Salama, Michezo na Vijana na Miji Salama. Wizara inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuanza kufundisha somo la Usalama Wetu Kwanza kwa kuanzia katika shule 10 za msingi za majaribio. Uamuzi huu ni wa kizalendo na utawawezesha watoto kujenga uzalendo wa kuilinda nchi yao dhidi ya maadui na hata kuzuia uhalifu kutendeka kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu katika vituo vya Polisi. Hadi sasa jumla ya vikundi 3,876 vya Ulinzi Shirikishi vimeanzishwa na Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya wanaendelea kuwapanga askari katika Kata na Shehia kwa lengo la kushirikiana kwa karibu zaidi na wananchi katika kutatua kero za uhalifu na wahalifu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na wananchi kuhamasika na Ulinzi Shirikishi, Jeshi la Polisi litaendelea kujenga uelewa wa wananchi kuhusu ushiriki wao katika kutekeleza kwa vitendo falsafa ya Polisi Jamii, kuimarisha uwezo wa wananchi katika kuzuia na kutanzua uhalifu, kujenga uwezo wa askari Polisi kushirikiana na jamii katika kazi ya kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu pamoja na kuongeza hatua za kukamilisha

Sera ya Usalama wa Raia itakayorasimisha Polisi Jamii kuwa mkakati wa kitaifa wa kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, lengo la saba ni kuimarisha mafunzo ya askari wa vyombo vya ulinzi na usalama. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Aprili 2012 askari 15,728 kutoka Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji wamepatiwa mafunzo katika fani mbalimbali ambapo Polisi ni 13,389, Magereza 1,764, Zimamoto na Uokoaji 60 na Uhamiaji 515. Mwaka 2012/2013, mafunzo yatatolewa kwa jumla ya askari 23,713 ambapo Polisi ni 20,000, Magereza 500, Uhamiaji 600 na Zimamoto na Uokoaji 2,613.

Mheshimiwa Spika, lengo la nane ni kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za kilimo katika maeneo ya Magereza. Katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Magereza limelima hekta 1,047.20 za mashamba ya mbegu bora za kilimo kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Lindi, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Morogoro kwa matarajio ya kuvuna tani 1,500 za mbegu bora.

Aidha, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Kampuni ya *Highland Seed Growers Ltd* na *TANSEED* limelima hekta 990.2 za mashamba ya mbegu bora za kilimo katika Mikoa ya Rukwa, Ruvuma na Kigoma na matarajio ni kuvuna tani 1,500 za mbegu bora. Lengo la mwaka wa fedha 2012/2013 ni kulima hekta 1,094 za mazao mbalimbali kwa matarajio ya kuvuna tani 4,923.

Mheshimiwa Spika, lengo la tisa ni kutoa vitambulisho vya Taifa. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imekamilisha utengenezaji wa kituo cha muda cha kuingizia

kumbukumbu na kituo cha muda cha utunzaji na utengenezaji wa mfumo wa utambuzi na usajili wa watu na hatimaye kutoa vitambulisho. Aidha, michoro kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za utambuzi na usajili wa watu za Wilaya Tanzania Bara na Zanzibar imekamilika ikiwa ni pamoja na michoro ya kituo kikuu cha kudumu cha utunzaji wa taarifa na uchapishaji. Hatua inayofuata ni ujenzi wa ofisi katika Wilaya 40 katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, zoezi la majaribio hatua ya kwanza ambalo limehusisha watumishi wa Serikali Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar wapatao 290,000 na wananchi wa Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro wapatao 220,000 limekamilika. Zoezi hili limehusisha ujazaji wa fomu, uhakiki wa taarifa na uingizaji wa taarifa katika mfumo wa kompyuta. Hatua itakayofuata ni uchukuaji wa alama za vidole, picha na saini kwa lengo la kuingiza katika mfumo na hatimaye kutoa vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyo mbele yetu ni upatikanaji wa rasilimali fedha, vifaa na watu ili zoezi hili likamilike katika kipindi cha miaka miwili kwa lengo la kusaidia vitambulisho kutumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Mfumo wa utambuzi na usajili wa watu utakapokamilika utasaidia katika kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato, kupunguza gharama za uendeshaji wa mfumo mingine mikubwa ya Serikali na hivyo kuipunguzia mzigo Serikali. Aidha, wananchi watapata fursa ya kutambulika na kufaidika na fursa mbalimbali za kijamii mathalani mikopo na huduma nyinginezo. Mfumo huu vile vile utasaidia kudhibiti uhalifu na hivyo kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hasa baada ya kuridhia makubaliano ya

kuondoa vizuizi vya mipaka katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lengo la kumi ni kuimarisha vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vyenye wataalam na zana za kisasa ili kukabiliana na majanga ya moto. Hatua mahsusi zimechukuliwa za kuwaunganisha askari wa Zimamoto na Uokoaji kutoka katika Halmashauri na Viwanja vya Ndege kwa upande wa Tanzania Bara kuwajibika chini ya komandi moja kuanzia mwezi Julai 2012. Askari 60 wamepatiwa mafunzo ya uongozi katika Chuo cha Magereza Ukonga Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, jumla ya magari makubwa manne ya kuzimia moto yamepatikana kwa ajili ya Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Viwanja vya Ndege. Magari hayo yatatumika katika Viwanja vya Ndege vya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Ili kusogeza huduma ya zimamoto na uokoaji karibu zaidi na wananchi, katika mwaka 2012/2013 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kufungua vituo vipya vya Zimamoto na Uokoaji katika Jiji la Dar es Salaam katika maeneo ya Tegeta, Mwenge, Kigamboni, Mbagala, Tabata, Mbezi Luisi na Gongo la Mboto.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2011/2012 na Malengo ya Mwaka 2012/2013. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 72,751,137,075. Hadi tarehe 30 Aprili, 2012 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 70,775,666,564 sawa na asilimia 97.3 ya lengo la mwaka.

Katika mwaka 2012/2013 Wizara ina lengo la kukusanya mapato ya shilingi 96,652,212,000. Nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zitolewazo na taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliidhinishiwa kutumia shilingi 482,394,883,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2012, jumla ya shilingi 382,944,359,941 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 79.4 ya bajeti. Jumla ya shilingi 211,906,987,554 zimetumika kulipia mishahara, Matumizi Mengineyo shilingi 159,577,911,122 na fedha za maendeleo ni shilingi 11,459,461,265. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imetengewa shilingi 555,540,268,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi, katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Polisi liliendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha nchi inakuwa na usalama, amani na utulivu. Jeshi la Polisi limefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuwalinda wananchi na mali zao, kusimamia utii wa sheria za nchi, kuzuia makosa, kupeleleza makosa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa wa makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia rasilimali watu, fedha na vitendea kazi vilivyopo, Jeshi la Polisi limeendelea kuhuisha mifumo ya kuzuia uhalifu na kupeleleza makosa ya jinai, kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kazi za Polisi, kuimarisha mifumo ya menejimenti na maslahi ya askari,

kupunguza tatizo la uhaba na uchakavu wa kambi na vituo vya Polisi, kupunguza tatizo la uhaba na uchakavu wa vitendea kazi hususan magari na pikipiki, kuhamasisha wananchi na wadau mbalimbali kuhusu Ulinzi Shirikishi na kuimarisha ukaguzi, usimamizi na tathmini ya malengo, shahaba na kazi zinazotakiwa kufanywa na Jeshi la Polisi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Udhhibiti wa Silaha za Kiraia, Jeshi la Polisi liliendelea kuweka alama maalum katika silaha zinazomilikiwa na taasisi za Serikali, makampuni na raia ambapo katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012, jumla ya silaha 15,883 zimewekewa alama hiyo. Hivyo kufanya jumla ya silaha 37,604 zilizowekewa alama hiyo tangu zoezi hili lilipoanza mwaka 2009. Zoezi hili limefanyika katika Mikoa ya Dodoma, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Tabora, Manyara, Singida, Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara. Zoezi la kuweka silaha alama maalum litaendelea katika mwaka 2012/2013 na kuanza mchakato wa kutunga sheria mpya ya kusimamia umiliki wa silaha.

Mheshimiwa Spika, kuzagaa kwa silaha ndogondogo ni tishio kwa usalama wa raia na mali zao. Jeshi la Polisi limeendelea kukabiliana na tatizo la kuzagaa kwa silaha hizo ambapo katika misako na operesheni maalum zilizofanyika katika mwaka 2011/2012, jumla ya silaha ndogondogo 503 zilikamatwa zikiwa zinamilikiwa kinyume cha sheria. Aidha, katika kutekeleza agizo lililotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi mwezi Agosti, 2011 la kusalimisha silaha kwa hiari, jumla ya silaha 59 zilisalimishwa.

Mheshimiwa Spika, Jukwaa la Haki Jinai, ushirikiano wa kiutendaji kati ya Jeshi la Polisi na taasisi nyingine kuu zinazounda Jukwaa la Haki Jinai ambazo ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Magereza na Mahakama umeendelea kuimarika ambapo Jeshi la Polisi limejikita katika eneo la kuongeza ufanisi katika upelelezi wa makosa ya jinai. Ili kuendeleza azma hiyo, katika mwaka 2012/2013 Jeshi la Polisi litatumia vyo vyake vya Dar es Salaam na Kidatu kutoa mafunzo ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za kiintelijensia na mbinu za kisasa za upelelezi kwa Maafisa, Wakaguzi na askari wapatao 1,000.

Mheshimiwa Spika, Ushughulikiaji wa Malalamiko, Jeshi la Polisi limeendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya watendaji wake wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya malalamiko 625 ya wananchi dhidi ya kero ya rushwa yalishughulikiwa. Askari 68 walifukuzwa kazi, 9 kesi zao zinaendelea katika Mahakama za jinai na wengine 15 uchunguzi unaendelea. Aidha, Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu wa kuwazawadia askari wanaokataa kupokea rushwa katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Polisi Kikanda na Kimataifa, Jeshi la Polisi liliendelea kushirikiana na Mashirika ya Polisi ya kikanda na kimataifa katika kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu hapa nchini, ukanda wa Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika, Barani Afrika na dunia kwa ujumla. Mashirika hayo ni pamoja na Shirikisho la Polisi la Kimataifa – *Interpol*, Shirikisho la Polisi la nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika – EAPCCO na Shirikisho la Polisi la nchi za Kusini mwa Afrika – SARPCCO. Ushirikiano uliopo umejielekeza katika ubadilishanaji wa taarifa za uhalifu na

wahalifu, mafunzo, operesheni za pamoja na mikutano ya pamoja ya Wakuu wa Majeshi ya Polisi na Wakuu wa Upelelezi wa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2011 ilifanyika operesheni maalum iliyojulikana kama Operesheni Kwacha. Operesheni hii ililenga katika kuwasaka na kuwakamata wahalifu wa baadhi ya makosa yanayopewa kipaumbele katika kudhibitiwa na Shirikisho la Majeshi ya Polisi Kimataifa na Kikanda ambayo ni wizi wa magari, usafirishaji wa dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa silaha, usafirishaji haramu wa binadamu na wahamiaji haramu. Katika operesheni hiyo jumla ya kilo 9,789 za dawa za kulevya za mashambani na viwandani na magari 19 yaliyoibwa kutoka Japan, Uingereza, Malaysia na Afrika Kusini yalikamatwa. Katika kuendeleza ushirikiano huu mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi litashiriki katika mafunzo, ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia, operesheni za kikanda na litakuwa mwenyeji wa mkutano Mkuu wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi wa nchi za Kusini mwa Afrika kwa kuwa hivi sasa Inspekta Jenerali wa Polisi Tanzania ndiye Mwenyekiti mteule wa Shirikisho hilo.

Mheshimiwa Spika, Maslahi ya Askari hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuboresha maslahi ya askari. Hatua hizo ni pamoja na kuanza kutumika kwa kanuni za fidia kwa askari wanaoumia au kuuawa wakiwa kazini. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya askari 62 waliumia na 16 waliuawa wakiwa kazini. Askari hao au wategemezi wao wanastahili kulipwa fidia kati ya shilingi milioni moja na shilingi milioni 15 kwa walioumia na wategemezi wao kulipwa shilingi milioni 15 kwa askari aliyeuawa wakati akiwa kazini. Pia katika kuongeza morali wa askari na kumpunguzia askari ukali wa

maisha, Serikali imeongeza posho ya chakula ya askari kutoka shilingi 100,000 kwa mwezi hadi shilingi 150,000. Kiwango hiki kitatumika pia kwa Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Ajira, katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Polisi limeajiri askari wapya 3,264. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi linatarajia kuajiri askari wapya 3,000. Idadi kubwa ya waajiriwa itapatikana kutoka katika mashule na vyo vya elimu ya juu. Utaratibu huu unalenga kuwa na askari wenye sifa stahiki na waaminifu kwa kazi ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi na Vituo vya Polisi, katika mwaka 2011/2012, hatua mbalimbali za ujenzi zimefikwa katika ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa kama ifuatavyo:- Kusini Pemba (asilimia 100), Mara na Manyara ujenzi upo hatua ya msingi na vituo vya Polisi vya daraja "B" vya Ludewa (asilimia 60), na Kwimba (asilimia 98) na vituo vya daraja "C" vya Horohoro (asilimia 100) na Mtambaswala (asilimia 85).

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya UKIMWI, katika mwaka 2011/2012, uhamasishaji wa askari Polisi wote kutekeleza Sera ya Ukimwi mahali pa kazi ulifanyika nchi nzima kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya ya VVU na ukimwi. Matokeo yake ni kwamba maambukizi ndani ya Jeshi la Polisi yamepungua kutoka asilimia 5 mwaka 2010/2011 hadi asilimia 4.8 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Jeshi La Magereza, Usafirishaji wa Mahabusu Kwenda Mahakamani na Kurudi Magerezani Jeshi la Magereza linatekeleza jukumu la kuwasindikiza

mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi Gerezani katika Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya mbili za Mkoa wa Pwani za Kisarawe na Mkuranga. Jukumu hili kwa kiasi kikubwa lilikuwa linapata fedha kutoka Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ambapo vitendea kazi kama vile magari ya kubebea mahabusu yalinunuliwa kupitia fedha za kapu la programu hiyo. Hivi sasa, ufadhili wa programu hii umeshuka kwa kiwango kikubwa na kubaki na eneo lenye fedha kidogo la mafunzo.

Kutokana na hali hiyo, jukumu hili imeshindikana kutekelezwa katika Wilaya zilizobakia za Mkoa wa Pwani na kuanza katika Mkoa wa Arusha kama ilivyokuwa imetarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Programu za Urekebishaji wa Wafungwa, hivi sasa mradi wa uendeshaji wa shughuli za wafungwa kwa kutumia mtandao wa kompyuta unafanya kazi katika Magereza ya Mkoa wa Dar es Salaam. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Magereza linatarajia kuanza awamu ya pili ya utekelezaji katika Magereza ya Mkoa wa Dodoma, Mwanza na Tabora kwa kusimika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, Ajira, katika mwaka 2011/2012, jumla ya askari 684 walijajiriwa na katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri askari 1,800.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Magereza Yenye Ulinzi Mkali, ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza umefanyika na unaendelea katika Magereza ya Maweni – Tanga, Karanga – Moshi na Isanga – Dodoma. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, ukarabati wa

majengo na miundombinu utaendelea katika Gereza la Butimba – Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Upanuzi, Ukamilishaji, Ukarabati na Ujenzi wa Mabweni ya Wafungwa, kazi ya upanuzi na ukarabati wa mabweni ya wafungwa iliendelea katika Gereza la Masasi. Aidha, kazi ya ujenzi iliendelea katika Magereza ya Chato, Utete na Masasi. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, lengo ni kuendelea kukamilisha ukarabati wa kuta katika Gereza la Kilwa na Ilagala-Kigoma. Pia ukarabati wa mabweni ya wafungwa katika Magereza ya Korogwe na Bukoba utaanza.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa, ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Magereza katika Mikoa ya Dar es Salaam na Singida umeendelea. Ujenzi wa Ofisi ya Magereza Singida upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Jeshi la Magereza litakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Singida na kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Nishati Mbadala Magerezani, katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni Magerezani na hivyo kuweko na tishio la uharibifu wa mazingira na kuongeza athari za tabianchi, Jeshi la Magereza limeendelea kuchukua hatua za kuanza kutumia gesi asilia, nishati itokanayo na tungamotaka na makaa ya mawe kama nishati mbadala ya kupikia chakula cha wafungwa Magerezani. Mfumo wa usambazaji wa gesi asilia na ufungaji wa vyungu husika umekamilika katika Gereza la Keko na matumizi yameshaanza. Matumizi ya nishati

itokanayo na tungamotaka katika Gereza la Ukonga, ujenzi wa mfumo umekamilika na kuanza kutumika. Hivi sasa mtambo wake unazalisha asilimia 77 ya mahitaji yote ya nishati inayohitajika katika Gereza hilo. Upo uwezekano wa kuboresha mtambo huu ili uweze kuzalisha gesi zaidi kwa kuongeza malighafi ya kuzalishia gesi hiyo. Makaa ya mawe yanaendelea kutumika katika Magereza ya Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Askari, ujenzi wa nyumba tatu za makazi ya askari umekamilika Gereza la Singida na ujenzi wa jengo la ghorofa uliendelea Mkoani Iringa na pia ujenzi wa nyumba moja Chato, moja Ngara na moja Magu uliendelea. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa la kuishi askari Mkoani Iringa.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Mifumo ya Majisafi na Majitaka, ukarabati wa miundombinu ya majitaka ulifanyika katika Magereza ya Kasungamile, Ngudu, Isanga na Chuo cha Ukonga. Vile vile mfumo wa majisafi umeboreshwa katika Magereza ya Keko, Ukonga, Maweni, Mbigiri, Handeni na Shinyanga. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, ukarabati wa mfumo wa majisafi utafanyika Gereza Isupilo- Iringa pamoja na ukarabati wa mfumo wa majitaka katika Gereza Mkwaya – Mbinga.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magereza, Shirika la Magereza limeongeza eneo lililolimwa mazao mbalimbali ya chakula kutoka ekari 5,435.5 msimu wa 2010/2011 hadi ekari 6,343 msimu wa 2011/2012 kwa matarajio ya kuvuna tani 8,563 za mazao mbalimbali. Ongezeko hili la eneo

lililolimwa linatarajiwa kutoa ziada ya tani 1,224 ya mazao mbalimbali ikilinganishwa na msimu uliopita wa 2010/2011. Aidha, Shirika limeongeza ubora wa mifugo kwa kutumia uzalishaji wa ndama kwa njia ya uhamilishaji (AI) na pia limeweza kutengeneza samani bora zikiwemo za watu binafsi, mashirika, idara na taasisi za Serikali. Matarajio ya Shirika ni kutumia ipasavyo soko la ndani la samani za ofisi, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi ambalo linaendelea kupanuka.

Mheshimiwa Spika, Kilimo cha Umwagiliaji, ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Magereza ya Idete – Morogoro na Kitengule – Kagera upo katika hatua mbalimbali za kufanya tathmini ya mazingira na usanifu wa michoro. Jeshi la Magereza litaendelea na miradi hiyo katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Jamii, Programu ya Huduma kwa Jamii ilianza rasmi mwaka 2005 kama njia mojawapo ya adhabu mbadala ya kifungo gerezani. Programu hii inatekelezwa katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Kagera, Mara na Shinyanga. Katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 jumla ya wafungwa 1,080 wamefaidika na programu hii ambapo wanaume ni 908 na wanawake 172. Wafungwa hao hutumikia vifungo vyao nje ya magereza kwa kufanya kazi bila ya malipo katika taasisi za umma. Changamoto kubwa ya programu hii ni ufinyu wa bajeti unaokwamisha Mikoa mingine kushindwa kunufaika na programu hii.

Mheshimiwa Spika, Idara Ya Uhamiaji, katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 jumla ya wageni 794,934

waliingia nchini, ikilinganishwa na wageni 625,308 walioingia nchini katika kipindi kama hiki mwaka jana. Wageni 779,174 walitoka nje ya nchi ikilinganishwa na wageni 664,037 waliotoka nchini katika kipindi kama hiki mwaka jana. Idadi ya wageni walioingia imeongezeka kwa watu 169,086 sawa na asilimia 27. Kuongezeka kwa idadi hii kunaweza kuelezwa pamoja na mambo mengine ni kutokana na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na hali ya usalama nchini.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waliopatiwa Hati za Ukaazi katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 wageni 14,781 walipewa hati za ukaazi nchini ikilinganishwa na wageni 12,563 waliopewa hati hizo katika kipindi kama hiki mwaka jana. Idadi ya hati zilizotolewa imeongezeka kwa hati 2,218 sawa na asilimia 17.7. Hali hii ni matokeo ya kuanza kuimarika kwa uchumi duniani na hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waliopatiwa Uraia wa Tanzania, wageni 18 walipatiwa uraia. Wageni waliopata uraia ni wa kutoka India (7), Kenya (2), Pakistani (2) na Somalia (7). Wageni wawili kutoka Pakistani ni wanawake ambao wameolewa na Watanzania na kutoka Somalia ni watoto saba wa Kisomali ambao wazazi wao tayari ni raia wa Tanzania.

Aidha, maombi ya wageni 43 kutoka India (20), Kenya (6), Rwanda (3), Uingereza (5), Pakistani (2) na Somalia (7) yalikataliwa kwa kushindwa kutimiza masharti. Hivi sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kuandaa

Sera ya Uhamiaji na Uraia ili kuweza kudhibiti kiwango cha wageni wanaopewa uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Watanzania 34 walipata uraia wa mataifa mengine ya Namibia (3), Uingereza (4), Ujerumani (6), Norway (3), Kenya (5), Botswana (4), Denmark (4), Korea ya Kusini (1), Marekani (1), Afrika Kusini (2) na Cuba (1) hivyo kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, Hati za Kusafiria Zilizotolewa. Jumla ya hati za kusafiria 39,586 zimetolewa katika kipindi cha 2011/2012. Kati ya hizo 38,422 ni za kawaida, 895 za Afrika Mashariki, 209 za kibalazi na 60 za kiutumishi, ikilinganishwa na hati za kusafiria 36,818, ambapo 35,546 za kawaida, 813 za Afrika Mashariki, 360 za kibalazi na 99 za kiutumishi zilizotolewa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Misako na Doria, katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 misako na doria iliwezesha kukamatwa kwa wageni haramu 5,603 ambao walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikilinganishwa na wageni haramu 3,339 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka 2010/2011. Miongoni mwa idadi hiyo wageni haramu 1,376 ni wa kutoka nchi za Somalia na Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Nyumba. Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga upo katika hatua za mwisho na ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Ruvuma, Morogoro na Manyara

unaendelea. Aidha, upanuzi wa Afisi Kuu ya Uhamiaji Zanzibar na ujenzi wa nyumba moja katika Kituo cha Rusumo na ukarabati wa nyumba 4 katika Kituo cha Sirari na 4 Kibaha umekamilika. Wakandarasi wa kukarabati nyumba za watumishi katika Vituo vya Horohoro – Tanga, Igoma – Mwanza na Chuo cha Uhamiaji Kikanda, Moshi wamepatikana na taratibu za mikataba zinakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la mwaka 2012/2013, ni kuendeleza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Morogoro, Manyara na Ruvuma, kuanza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Pwani na Singida na kufanya ukarabati wa nyumba za watumishi Mkoani Dodoma na katika Vituo vya Uhamiaji vya Borogonja na Tunduma. Ajira na Mafunzo, katika mwaka 2011/2012, askari 52 wameajiriwa ambao watapatiwa mafunzo katika mwaka wa fedha 2012/2013 na watumishi 515 wamepatiwa mafunzo katika fani mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, mafunzo yatatolewa pia kwa watumishi 600.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Vyombo vya Usafiri. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya magari tisa na pikipiki tano zimenunuliwa ili kuimarisha misako na doria. Katika mwaka 2012/2013 Idara itanunua magari 34, pikipiki 100 na boti tatu.

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya UKIMWI. Katika suala la kupambana na maambukizi mapya ya UKIMWI mahali pa kazi Idara imeendelea kuwahudumia waathirika na kutoa elimu kwa askari na familia zao katika Mikoa ya Kagera, Mwanza na Mtwara sambamba na zoezi la kupima afya ambapo watumishi 450 pamoja na familia zao walijitokeza kupima virusi vya ukimwi kwa hiari. Aidha,

vipeperushi vimesambazwa katika vituo vya kuingilia nchini kwa lengo la kutoa elimu juu ya janga la ukimwi kwa wasafiri wanaoingia na kutoka nchini.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, katika mwaka 2011/2012 Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vimeendelea kutoa huduma za kuzima moto na uokoaji katika sehemu mbalimbali. Huduma hii inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya mwaka 2007. Aidha, katika kuboresha utoaji wa huduma hii, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limezingatia utoaji wa elimu juu ya kinga na tahadhari ya moto. Jumla ya maeneo 41,774 yamefanyiwa ukaguzi ikiwa ni majengo 23,570 na vyombo vya usafiri na usafirishaji 18,204 kama ilivyofafanuliwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, limeajiri askari wapya 124 na kutoa mafunzo maalum ya uongozi na ukaguzi wa majengo pamoja na vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa askari 60 ili kuboresha uendeshaji wa zoezi zima la ukaguzi. Mafunzo hayo yalitolewa katika Chuo cha Magereza Ukonga - Dar es Salaam. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea na zoezi la ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto, kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kununua magari matano na kuajiri askari wapya 2,613 na kuwapatia mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Idara Ya Wakimbizi. Tarehe 30 Aprili, 2012 Tanzania ilikuwa na jumla ya wakimbizi 112,645 wakiwemo Warundi 48,195, Wakongo 62,632, Wasomali 1,548 na 270 wakimbizi wa mataifa mbalimbali kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali Na. 6. Katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Aprili, 2012 jumla ya wakimbizi 189 walirejea kwao ambapo Warundi ni 155 na Wakongo 34.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2011/2012 nilieleza kwamba wakimbizi 38,800 walioko katika kambi ya Mtabila, wangerejeshwa kwao na kambi hiyo kufungwa. Hata hivyo, katika mwaka 2011/2012, idadi ya wakimbizi wa Burundi kutoka kambi hiyo waliorejea kwao ni 155 tu, hali iliyosababisha kambi hiyo kutofungwa. Mkakati mpya wa kufunga kambi hiyo ni kwamba limefanyika zoezi la mahojiano ya kina na wakimbizi hao kwa lengo la kubaini kama wapo wakimbizi wenye sababu za msingi za kuendelea kuwepo nchini kama wakimbizi. Zoezi hilo lilifanyika mwezi Septemba hadi Desemba, 2011. Matokeo ya zoezi hilo yanaonyesha kuwa wapo wakimbizi 33,705 ambao hawana sababu za msingi za kuendelea kuwa wakimbizi na wengine 2,045 walionekana kuwa na sababu za msingi za kuwa wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matokeo ya zoezi hilo, kikao cha Pande Tatu (Tanzania, Burundi na UNHCR) kilifanyika Bujumbura - Burundi tarehe 22 Februari, 2012 na kukubaliana kwa pamoja kuifunga kambi ya Mtabila ifikapo tarehe 31 Desemba, 2012. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekwishawasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili iandaliwe Hati ya Ukomo wa Ukimbizi (*Cessation clause*), kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa. Mara hati hiyo itakapokuwa tayari litatolewa tamko la ukomo wa ukimbizi

kwa wakimbizi hao walioko katika Kambi ya Mtabila. Baada ya tamko hilo, wakimbizi hao wataendelea kusaidiwa kurejea Burundi mpaka kambi itakapofungwa hapo tarehe 31 Desemba, 2012. Watakaokuwa wamegoma kurejea mpaka kufikia wakati kambi inafungwa, watachukuliwa kuwa ni wahamiaji haramu na hivyo kushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria za Uhamiaji. Kwa upande wa wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usalama nchini humo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Katika mwaka 2011/2012 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeajiri watumishi 105 na imenunua magari 12. Katika mwaka 2012/2013 Mamlaka itaajiri watumishi 110, itanunua magari 15 kwa ajili ya zoezi la utambuzi na usajili wa watu, kuanza ujenzi wa ofisi za utambuzi wa watu na usajili katika Wilaya 40, kupanua jengo la Makao Makuu Dar es Salaam na kuendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa watu katika Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni 2011/2012, utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali Bungeni katika mwaka 2011/2012, umezingatiwa katika eneo la III na la IV katika hotuba hii katika maeneo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi pamoja na mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2011/2012. Kwa ujumla wake, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni katika mwaka 2011/2012 ni kama inavyoonyesha katika Kiambatisho Na. 1 cha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Sensa ya Watu na Makazi. Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka 2012/2013 unafanyika miezi michache kabla ya kufanyika kwa zoezi muhimu la sensa ya watu na makazi. Kabla ya kuwasilisha maombi ya fedha, naomba nieleze machache kuhusiana na umuhimu wa wananchi kushiriki kwenye sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika tarehe 26 Agosti, 2012 yenye kauli mbiu ya "Sensa kwa Maendeleo Jiandae Kuhesabiwa".

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yanawezeshwa na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu. Hali ya amani na utulivu ni kipimo kinachoashiria kuwepo kwa usalama wa raia na mali zao. Zoezi la sensa ya watu na makazi ni muhimu katika suala zima la usalama wa raia na mali zao.

Kwa kuzingatia umuhimu wa zoezi lenyewe, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaweza kupata takwimu ya idadi kamili ya watu na makazi na hivyo kuiwezesha Wizara kupanga mipango na mikakati sahihi na endelevu ya kukabiliana na changamoto katika kulinda usalama wa raia na mali zao. Hivyo, ninawaomba kila mmoja wetu ashiriki katika sensa hii na awe ni balozi wa kuhamasisha umma kujitokeza na kushiriki kikamilifu katika zoezi zima la sensa ya watu na makazi kwa maendeleo na ustawi wa Taifa letu.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dharti kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa

mwaka 2012/2013. Ushauri wa Kamati hiyo utaisaidia Wizara yangu kuimarisha utendaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee nazitoa kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mbunge wa Chumbuni, Katibu Mkuu Ndugu Mbarak Abdulwakil, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwamini Malemi, Inspekta Jenerali wa Polisi Ndugu Saidi Mwema, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Ndugu Magnus Ulungi, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Ndugu Dickson Maimu, Kaimu Kamishna Jenerali wa Magereza Ndugu Fidelis Mboya, Kaimu Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Ndugu Pius Nyambacha na Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda, askari pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao wamefanikisha maandalizi ya hotuba hii. Nachukua pia fursa hii kuwashukuru nchi wahisani ikiwemo Japan, China, Marekani, Misri na Saudi Arabia, taasisi za INTERPOL, IOM, EU, UNHCR, Dfid, UNICEF, WFP, Pharm Access na Marie Stopes pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kibali chako ninawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Kiserikali na ya Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimikwa Spika, Mwisho ingawa sio mwisho kwa umuhimu ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa maelekezo yake mbalimbali na Mheshimiwa Mizengo Peter

Pinda (Mb), Waziri Mkuu kwa kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2012/2013 ya shilingi 555,540,268,000 kwa ajili ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida na miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya maombi hayo shilingi 540,002,518,000 ni za Matumizi ya Kawaida ambapo shilingi 242,894,300,000 ni Matumizi Mengineyo na Mishahara shilingi 297,108,218,000. Maombi ya shilingi 15,537,750,000 ni kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

Fungu 14: Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Matumizi Mengineyo shilingi	8,306,262,000
Mishahara shilingi	8,661,572,000
Maendeleo shilingi	0.00
Jumla Shilingi	16,967,834,000

Fungu 28: Jeshi la Polisi

Matumizi Mengineyo shilingi	133,329,019,000
Mishahara shilingi	198,944,297,000
Maendeleo shilingi	3,332,250,000
Jumla Shilingi	335,605,566,000

Fungu 29: Jeshi la Magereza

Matumizi Mengineyo shilingi	51,449,403,000
Mishahara shilingi	62,908,822,000
Maendeleo shilingi	1,555,500,000

Jumla Shilingi 115,913,725,000

Fungu 51: Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Matumizi Mengineyo shilingi 2,107,467,000

Mishahara shilingi 2,902,343,000

Maendeleo shilingi

650,000,000

Jumla Shilingi 5,659,810,000

Fungu 93: Idara ya Uhamiaji

Matumizi Mengineyo shilingi 47,702,149,000

Mishahara shilingi 23,691,184,000

Maendeleo shilingi 10,000,000,000

Jumla Shilingi 81,393,333,000

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA - K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:
Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha taarifa, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika suala zima la kuleta maendeleo na kutatua kwa pamoja changamoto zinazotukabili katika Jimbo letu la Ukonga. Lakini pia nawapongeza sana wanachama wa Chama

cha Mapinduzi katika Kata zote kwa kumaliza uchaguzi wa Chama kuanzia ngazi za Mashina, Matawi, Kata kwa amani na utulivu mkubwa. Naishukuru sana familia yangu, Mr. Ali Mwaiposa na watoto wangu Meketilide na Salmira kwa ushirikiano na uvumilivu wao mkubwa hasa pale wanapokosa ushirikiano wangu kwa sababu ya majukumu niliyonayo. Mwisho, namshukuru pia Mchungaji Ibrahim Kigole wa KKT Kitunda relini kwa jinsi anavyonitia moyo kuniombea, kunisaidia kiroho hasa pale mambo yanapokuwa magumu. Mungu akubariki sana Mtumishi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwasilishe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2012/2013, na kuliomba Bunge lako lipokee na kujadili na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama katika kutekeleza majukumu yake,

imekuwa ikifuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

Njia iliyotumika kutekeleza jukumu hilo ni pamoja na ziara, kutembelea baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hii pamoja na kuagiza maandalizi ya Taarifa mbalimbali zilizoletwa na kujadiliwa kwa undani kwenye Vikao vya Kamati. Mfano wa Taasisi za Wizara hii zilizotembelewa katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu na malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ni Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2012, tarehe 30 Mei, 2012 Kamati ilitembelea Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili kujiridhisha kuhusu namna Mamlaka hiyo ilivyotekeleza lengo lake la bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Pia, tarehe 31 Mei, 2012 Kamati ilitembelea Mradi wa nyumba za Jeshi la Polisi katika eneo la *Kilwa Road Dar es Salaam* pamoja na Makao Makuu ya Uhamiaji kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo pamoja na mazingira yake.

Mheshimiwa Spika, mbali na ziara hizo, Kamati pia iliweka utaratibu wa kufuatilia hali ya usalama wa raia na mali zao sambamba na kuoanisha matumizi na utekelezaji wa malengo ya Bajeti kwa mafungu yote matano ya Wizara hii. Mafungu hayo ni:-

- (i) Fungu 14 - Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji;
- (ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;

- (iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;
- (iv) Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na
- (v) Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Katika kikao cha Kamati cha tarehe 05 Juni, 2012, Kamati ilielezwa kuhusu malengo ya Wizara hii yaliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Utekelezaji huo ni kwa mafungu yote matano chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pamoja na maelezo hayo, pia taarifa ilibainisha changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji. Wajumbe walihoji mambo mbalimbali na kupatiwa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo hayo uliambatana na matumizi ya fedha kama zilivyopokelewa kutoka Hazina. Kamati ilipenda kujua mwenendo wa matumizi ili kulinganisha na makusudio ya Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa Wizara hii. Katika uchambuzi wake, Kamati ilipitia kifungu kwa kifungu ili kubaini utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilionyesha miongoni mwa malengo yaliyofanikiwa kutekelezwa ni lengo la Wizara katika eneo la mafunzo. Hadi kufikia Aprili, 2012 watumishi 15,760 walipatiwa mafunzo katika fani mbalimbali. Watumishi hao ni wale wa Jeshi la Polisi, Watumishi 13,389; Jeshi la Magereza, Watumishi 1,764; Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, Watumishi 60; Uhamiaji, Watumishi 515; na Makao Makuu ya Wizara, Watumishi 32.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako Tukufu lilipokuwa likipitia na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, tarehe 28 Julai, 2011, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alilieleza Bunge kuwa, Wizara yake imejiwekea lengo la kukusanya Shilingi bilioni 79 na kutaja mikakati miwili iliyowezesha ufikiaji wa lengo hilo kama ifuatavyo:-

- (i) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato katika Taasisi zake; na
- (ii) Kusisitiza malipo ya huduma yafanywe kwa kutumia Mabenki ili kudhibiti upotevu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionyesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2012 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa imekusanya jumla ya Sh. 70,765,054,768/= ambayo ni sawa na asilimia 97.3 ya lengo. Mwenendo huo kwa ujumla ni mzuri katika kufikia lengo la makusanyo lililowekwa.

Kwa upande wa Uhamiaji, makusanyo hadi kufikia mwezi Aprili, 2012 yalikuwa yamevuka lengo kwa kukusanya jumla ya Sh. 58,168,185,106/= katika lengo la Sh. 57,351,304,995/=. Ni maoni ya Kamati kuwa bado kuna uwezekano mkubwa wa makusanyo iwapo juhudi na usimamizi vitaimarishwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Kamati kutathimini ipasavyo, taarifa iliyowasilishwa ilionyesha mwenendo wa matumizi ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bunge liliidhinisha matumizi ya jumla ya Sh.

482,394,883,000/= na fedha zilizotoka Hazina hadi kufikia mwezi Aprili ni Sh. 210,843,865,000/= sawa na asilimia 88.4 ya bajeti ya mwaka mzima. Uchambuzi uliofanywa na Kamati, unaonyesha kuwa wakati fedha iliyopatikana kutoka Hazina ilikuwa ni asilimia 89.8 ya makadirio, kwa upande wa makusanyo fedha iliyokusanywa ilikuwa ni asilimia 97.3 ya lengo. Ongezeko hilo la asilimia linadhihirisha umuhimu wa kufanyia kazi zaidi vigezo vya makadirio ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, nidhamu ya matumizi na utaratibu mzima wa bajeti unaweza kuathiriwa na mwenendo wa madeni. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilitaka kujua hali ya madeni kwa mafungu ya Wizara hii. Maelezo yaliyotolewa kwenye Kamati, yalionyesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2012 Wizara ilikuwa na madeni yanayofikia Sh. 70,697,009,866/= ambapo madeni ya Wazabuni ni Sh. 47,240,626,771/= na madeni ya watumishi ni Sh. 23,456,383,095/=.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ilisababisha Kamati itake maelezo kuhusu mkakati uliowekwa kulipa madeni hayo. Maelezo ya Waziri yalionyesha kuwa, hatua mojawapo iliyochukuliwa ni kuwasilisha baadhi ya madeni hayo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili yahakikiwe. Aidha, Hazina imeombwa kuharakisha uhakiki wa madeni kwenye Fungu 29 - Jeshi la Magereza ili mchakato wa kuyalipa ukamilike.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Ushauri huo ulihusu mambo 13

ambayo yalikuwa katika majukumu ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uhamiaji, na Makao Makuu ya Wizara yenyewe. Taarifa iliyowasilishwa kwenye kikao cha Kamati inaonyesha kuwa sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati inaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa, kasi ya upelelezi katika kesi mbalimbali iongezwe bila ya kuathiri matakwa ya Sheria husika. Maelezo ya Waziri yalionyesha kuwa, mojawapo ya hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza ushauri huo, ni kutoa mafunzo ya intelijensia na upelelezi kwa askari 511 pamoja na kuikabidhi Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka kazi ya kuendesha mashitaka Mahakamani. Waliokuwa Waendesha Mashitaka wa Polisi, wamepangiwa kazi ya upelelezi wa kesi ili kuongeza kasi kama ilivyoshauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa uzingatiaji wa ushauri, ni ule uliohusu hatua za kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani. Taarifa imeonesha kuwa zipo hatua zilizochukuliwa kukabiliana na msongamano huo. Mojawapo ya hatua zilizoelezwa kwenye Kamati ni kuundwa kwa kikosi kazi chini ya Uenyekiti wa Mkurugenzi wa Mashitaka ili kushughulikia tatizo la msongamano Magerezani na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua. Aidha, kuna utaratibu wa Jeshi la Magereza kuifahamisha Mahakama Kuu kila mwezi idadi ya mahabusu waliokaa Gereza zaidi ya siku 60 kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzingatia sehemu ya ushauri, bado kuna mambo muhimu yanayohitaji kufanyiwa kazi ingawa kwa taarifa iliyowasilishwa, Serikali haikuyazingatia. Mfano mojawapo ni ushauri kuwa ili Zimamoto na Uokoaji iweze kutekeleza sheria ya

kuanzishwa kwake ipasavyo, inahitaji kutengewa fedha kwa ajili ya maendeleo kwenye Fungu 14.

Taarifa ilionyesha kuwa Serikali haikuzingatia ushauri huu kwa vile katika mwaka wa fedha 2012/2013, hakuna fedha ya maendeleo iliyotengwa kwenye Fungu 14 - Zimamoto na Uokoaji. Hii siyo ishara njema ya kujipanga kukabiliana na matukio ya moto nchini. Kamati haikuridhishwa na jambo hili na inasisitiza kuwa Serikali izingatie ushauri wake unaohusu kuimarisha hali ya usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilielezwa majukumu 59 yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 kwa mafungu yote matano, ili kulinganisha malengo yaliyowekwa na fedha zilizotengwa. Mtoa hoja alifafanua mantiki ya maombi ya fedha kwa kila kifungu (*Subvote*) na Kasma (*Item*) katika kila Fungu.

Mheshimiwa Spika, jambo moja lililojitokeza wakati wa uchambuzi huo, ni kuongezeka kwa makadirio ya kiasi cha jumla ya fedha inayoombwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ikilinganishwa na fedha iliyoombwa na kuidhinishwa na Bunge mwaka jana 2011/2012. Pamoja na ongezeko hilo Jeshi la Magereza ambalo limepewa jukumu maalumu la utekelezaji wa dhana ya Kilimo kwanza nchini, linaombewa fedha kidogo ikilinganishwa na fedha iliyombwa mwaka wa fedha 2011/2012. Eneo hasa la bajeti yake linaloathirika ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati mwaka jana Jeshi hili lilitengewa jumla ya Sh. 4,563,212,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo, mwaka huu linaombewa Sh. 1,555,500,000/=. Tofauti hii ni kiasi cha Sh. 3,007,712, 000/= ambacho ni sawa na asilimia 66 pungufu ya fedha iliyotengwa mwaka 2011/2012. Inawezekana hali hii ikawa na tafsiri kuwa Jeshi la Magereza kwa mwaka wa fedha 2012/2013 litapunguza utekelezaji wa malengo ya bajeti ya maendeleo kwa asilimia 66 jambo ambalo halipendezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kupitia kifungu kwa kifungu kwa mafungu yote matano. Katika majadiliano hayo, Kamati ilizingatia majukumu ya Wizara hii kama yalivyoainishwa katika Hati ya Serikali kuhusu mgawanyo wa majukumu ya Wizara (*Government Instrument*). Vilevile, Kamati ilizingatia ahadi za Serikali, hali ya usalama wa raia na mali zao, hali ya uingiaji wa wageni nchini, mambo yanayojadiliwa na wananchi nchini na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010, kisha kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Jeshi la Polisi.

(i) Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali bado kuna umuhimu mkubwa wa kuandaa mkakati mahususi wa kuendelea kujenga nyumba za kuishi Askari hao;

(ii) Suala la kuzagaa kwa silaha linapaswa kuendelea kudhibitiwa ili kuimarisha zaidi usalama wa raia na mali zao. Aidha, Jeshi la Polisi liongeze juhudi za kudhibiti uhalifu unaofanywa kwa kutumia silaha;

(iii) Jeshi la Polisi liongeze kasi ya kudhibiti na kuzuia matukio yote yanayohatarisha usalama wa raia na mali zao ili kuendeleza utulivu na amani nchini;

(iv) Ili kutekeleza azma ya Taifa kudumisha umoja, amani na usalama, Serikali ifanye juhudi za kutosha kuimarisha Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji pamoja na Uhamiaji, kwa kuviwezesha vyombo hivyo kuwa na zana na vifaa bora zaidi, sambamba na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; na

(v) Ili kukabiliana na tatizo la baadhi ya raia kujichukulia sheria mikononi na kuvamia vituo vya Polisi, ni vyema kuchunguza kwa kina sababu za matukio hayo na kurekebisha dosari na kasoro zilizosababisha hali hiyo.

(b) Jeshi la Magereza.

(i) Suala la msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani limekuwa tatizo kubwa kwa muda mrefu. Wakati umefika kwa Serikali kuandaa mpango na mkakati utakaosaidia kutatua tatizo hilo. Sambamba na hilo, muundo na utendaji wa Kamati za kusukuma kesi unapaswa kuangaliwa upya na kuboreshwa zaidi. Aidha, kuna umuhimu mkubwa wa kuwaweka wafungwa ambao ni watoto katika Magereza tofauti na yale ya watu wazima.

(ii) Kwa kuwa Jeshi la Magereza likiwezesha kwa vifaa na bajeti litaweza kuzalisha mazao ya kutosha kwa chakula na kwa ajili ya soko, Serikali iliwezeshe Jeshi hilo kutumia uwezo wake kuongeza uzalishaji. Kwa mfano, wakati wa majadiliano kwenye kikao cha Kamati,

Magereza walisema kuwa wanahitaji jumla ya matrekta 70 na zana zake zenye thamani ya Sh. 3,772,800,869/= na zana nyingine zenye thamani ya Sh. 1,614,700,000/= mahitaji ambayo hayakuzingatiwa katika makadirio haya. Kamati inasisitiza kuwa mahitaji hayo yazingatiwe kwa lengo la kuiwezesha dhana ya Kilimo Kwanza kuwa na maana katika Jeshi la Magereza.

(iii) Jeshi la Magereza liwezeshwe kuwa na idadi ya watendaji wa kutosha kutekeleza majukumu yake. Aidha, ili kumudu kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, Jeshi hili liongezewe bajeti na kupatiwa fedha kwa wakati.

(iv) Kwa kuwa Magereza ni vituo muhimu vya taarifa za msingi katika udhibiti wa hali ya amani, usalama na utulivu nchini, Serikali iongeze kasi ya kuliwezesha Jeshi hili kuwa na mawasiliano ya simu na *TEKNOHAMA* kwa ujumla.

(c) Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji.

(i) Serikali iongeze kasi ya kuboresha mazingira na uwezo wa kikosi cha Zimamoto na Uokoaji ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(ii) Pamoja na Serikali kutozingatia ushauri wa Kamati wa kutenga fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa Zimamoto na Uokoaji, Kamati inasisitiza kuwa ili Jeshi hili liweze kukabiliana na matukio ya moto na uokoaji kwa mujibu wa Sheria, ni muhimu kukiwezesha kikosi hiki kuwa na bajeti ya kutosha ya maendeleo.

(iii) Kamati inaendelea kushauri kuwa, uandaliwe utaratibu maalumu wa kuzitaka Taasisi zote zenye mkusanyiko mkubwa wa watu kuhakikisha kuwa watumishi wake wanapata mafunzo ya Zimamoto na Uokoaji. Maelezo ya kuwa kikosi cha Zimamoto na uokoaji kinaendelea kutoa elimu kwa Taasisi mbalimbali, hayaoneshi mpango wa kuzitaka Taasisi zenye mkusanyiko wa watu kupata mafunzo ya kujihami dhidi ya moto.

(d) Idara ya Uhamiaji.

(i) Wakati umefika kwa Serikali kukamilisha Sera ya Taifa ya Uhamiaji nchini ili kuwa na dira ya Taifa katika masuala ya msingi kuhusu uhamiaji.

(ii) Ili kuepuka tatizo la ulimbikizaji wa madeni kwa Idara ya Uhamiaji, uandaliwe utaratibu mzuri wa kumaliza madeni yaliyopo.

(iii) Vituo vya Uhamiaji vilivyopo mipakani viongeze umakini katika udhibiti wa wahamiaji haramu pamoja na kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama kudhibiti tatizo la biashara haramu ya usafirishaji wa watu (*human trafficking and smuggling*). Aidha, Uhamiaji wawezeshwe kwa kupewa vyombo vya usafiri kama vile magari, pikipiki pamoja na boti za doria ili kuimarisha misako na doria.

(iv) Elimu kuhusu madhara ya kuwahifadhi wahamiaji haramu itolewe kwa wananchi ili kukabiliana na ongezeko la vitendo vya uhalifu nchini vinavyosababishwa na wahamiaji hao.

(v) Kwa kuwa Idara ya Uhamiaji imepanga kuanza mchakato wa kutoa huduma za uhamiaji kupitia mfumo wa kielektroniki, kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha mtandao wa mawasiliano na zana muhimu kwa jukumu hilo.

(e) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

(i) Zoezi la utoaji wa vitambulisho nchini linahitaji umakini mkubwa na tahadhari ya mambo mengi. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ijizatiti kutekeleza zoezi hilo kwa namna itakayokuwa na tija iliyokusudiwa.

(ii) Kwa kuwa kuna uelewa mdogo wa wananchi kuhusu dhana nzima ya mfumo wa utambuzi na usajili wa watu, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iandae utaratibu thabiti wa kuwaelimisha wananchi kuhusu mfumo huo.

(iii) Kwa kuzingatia umuhimu wa Sheria Na. 11 ya Usajili na Utambuzi wa Watu ya Mwaka 1986 (*The Registration and Identification of Persons, Act, 1986*) Serikali iongeze kasi ya kuipitia Sheria hiyo ili ifanyiwe marekebisho haraka na kuwezesha usajili, utambuzi na utoaji wa vitambulisho ufanyike kwa ufanisi mkubwa.

(iv) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iwezeshe kujenga Ofisi za Utambuzi na Usajili katika kila Mkoa na Wilaya badala ya Wilaya 40 zilizopangwa katika Fungu 93 la Wizara hii.

(f) Ushauri wa Jumla.

(i) Kwa kuzingatia umuhimu wa watumishi wa kutosha wenye ujuzi na stadi za msingi katika suala la kuimarisha usalama wa raia na mali zao, Serikali iongeze juhudi za kuajiri watu wenye sifa katika vyombo vyote vya ulinzi na usalama chini ya Wizara hii.

(ii) Bunge linapopitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa kadiri inavyowezekana Serikali ijitahidi kuhakikisha kuwa utoaji wa pesa kwa mafungu husika unazingatia bajeti iliyoidhinishwa. Kufanya hivyo kutawezesha utekelezaji wa malengo yanayowekwa na kuepusha kukua kwa gharama za utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

(iii) Ili kudhibiti uhamiaji haramu, ulinzi na usalama katika mipaka yetu, Serikali iboreshe barabara za ulinzi sehemu za mipakani.

(iv) Pamoja na jitihada za Serikali kuboresha vyombo vya Ulinzi na usalama nchini, bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinaepukana na madeni kwa kulipa madeni yaliyokuwepo na kufanya malipo mapya kwa wakati.

(v) Utaratibu wa doria na misako ya pamoja itumike kudhibiti tatizo la wahamiaji haramu na biashara haramu ya Binadamu nchini.

(vi) Pamoja na ufinyu wa Bajeti, Wizara ya Mambo ya Ndani ifanyie kazi kasoro zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

(vii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iongeze umakini na usimamizi wa taratibu na nidhamu za matumizi ya fedha zinazoidhinishwa ili kupunguza hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Umakini huo utajenga imani na kuondoa mashaka katika utekelezaji wa malengo ya bajeti inayoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha taarifa hii na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2012/2013. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Pereira Ame Silima - Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano mzuri waliutoa kwenye Kikao cha Kamati. Nawashukuru pia Watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi chini ya uongozi wa Ndugu Mbarak M. Abdulwakil - Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa ushirikiano wao uliofanikisha uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Musa A. Zungu, kwa kunisaidia kuongoza vyema Kamati. Nawashukuru pia Wajumbe wengine kwa kazi nzuri, ushirikiano mkubwa na umakini wao wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Edward N. Lowassa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa *Capt.* Mst. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Vita R.

Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura. *(Makofi)*

Mwisho, lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Ndugu Athumani Hussein na Ramadhani Issa, Makatibu wa Kamati hii na Watumishi wengine wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah - Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili lipokee taarifa na maoni haya ya Kamati na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama alivyowasilisha mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MHE. VINCENT J. NYERERE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, napenda kuchukua fursa hii kuwasilisha maoni yake kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha

2012/2013. Aidha, napenda kuwashukuru Askari wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza wanaoishi Kambi iliyoko katika Kata ya Mkendo kwa kunichagua kuwa Diwani wao. Vile vile, nawashukuru wananchi wote wa vyama vyote na dini zote wa Jimbo la Musoma Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge na mtetezi wao. Pia napenda kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa imani yake kubwa kwangu kwa kunitewa kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upekee kabisa, kwa wanaoeneza propaganda kwamba, *CHADEMA* inachukia au kudharau Askari Polisi wetu, naomba nitoe shukrani zangu kwa mke wangu V. Nyerere, ambaye pia ni Askari wa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

SPIKA: Kwamba, na yeye humchukii. Ahsante. *(Kicheko)*

MHE. VINCENT J. NYERERE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, Polisi wote ni shemeji zangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha uliopita, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilihoji matukio mbalimbali ya mauaji ya raia yaliyowahusisha Askari wa Jeshi la Polisi pamoja na wa vyombo vingine vya dola. Aidha, tulihoji matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za binadamu na wananchi wetu hasa katika maeneo yenye migodi mikubwa ya dhahabu kama vile Nyamongo, Arusha na kwingineko katika nchi yetu. Vile vile, tulihoji sababu za Serikali kushindwa kuwachukulia hatua za kisheria na za kiutendaji watuhumiwa wa makosa haya makubwa.

Mheshimiwa Spika, wakati anatoa hoja yake ya kuahirisha Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka jana 2011/2012, Waziri Mkuu aliahidi kwamba, Serikali, ingefanya uchunguzi wa matukio yote ya mauaji kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo (*The Inquests Act*), Sura ya 24 ya Sheria za Tanzania. Kwa maneno yake mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema: "vifo ambavyo vimetokea katika mazingira ya kutatanisha chini ya mikono ya Vyombo vya Dola, ni lazima vichunguzwe."

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi wakati tunaandika maoni haya, hakuna Mahakama ya Korona hata moja ambayo imeitishwa kwa lengo la kuchunguza vifo vilivyotokana na matumizi ya nguvu ya vyombo vya dola. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama kauli ya Waziri Mkuu ilitolewa kwa lengo la kuwahadaa Watanzania. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itamke ni lini Serikali itaunda Mahakama za Korona ili kuchunguza matukio yote ya mauaji ya wananchi katika maeneo yote tuliyoyataja mwaka 2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya Serikali kutotimiza ahadi yake ya kuchunguza matukio ya mauaji kwa mujibu wa Sheria tajwa, vitendo vya mauaji na ukiukwaji wa haki za binadamu vimeendelea kutokea katika nchi yetu. Kwa mfano, katika taarifa yake ya Haki za Binadamu kwa Mwaka 2011, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*) kinaripoti kwamba, "mwenendo wa matukio ya ukatili wa Polisi na mauaji yanayofanywa kinyume cha Sheria na vyombo vya dola umeendelea kuongezeka katika nchi yetu. Kati ya Januari na Desemba, 2011 tayari watu 25

wamekwisharipotiwa kuuawa wakiwa mikononi mwa Polisi na Maafisa wengine wa usalama, wakati ambapo watu wengine 50 walijeruhiwa." Taarifa hii inaungwa mkono na taarifa ya *Hali ya Haki za Binadamu* kuhusu Tanzania iliyotolewa mwaka huu na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani (*State Department*) inayoonyesha kuwa bado yapo mauaji yanayotokea mikononi mwa vyombo vya dola ikiwemo Jeshi la Polisi, utesaji na wananchi wanaotuhumiwa kujikuta wakipata vipigo kinyume na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeiridhia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Serikali kutochukua hatua kukabiliana na matukio ya mauaji yanayohusishwa na vyombo vya dola...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 64 (1) (a) na (b). Hotuba ya Mheshimiwa Nyerere, anayokusudia kuisoma, ukurasa wa tatu mpaka ukurasa wa tano ina mkanganyiko wa maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hotuba yote hii katika vifungu vinne vya maelezo yake, kesi zake ziko Mahakamani, ikiwepo ya ndugu yangu Msigwa; kesi zake vifungu vinne katika hii ziko Mahakamani. Lakini mengine yote yako kwenye uchunguzi mkali sana wa Jeshi la Polisi, yanafanyiwa uchunguzi.

WABUNGE FULANI: Aaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, nami kwa ushauri wangu kwa ndugu yangu Vincent, maelezo haya ni mazuri sana kama yangeweza kuisaidia Polisi kuliko kuyasema hapa ndani. Kwa sababu, nikitoa ufafanuzi, kwa mfano, *paragraphs* zile za mwanzo zote, wote tunajua kwamba Polisi, wameshawafikisha baadhi ya watuhumiwa Mahakamani. Hata tukio la jana la Singida, liko kwenye upelelezi, lakini baadhi wameshapelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, jana ulilifafanua vizuri kwa kutumia Kanuni ya 48. Ukienda ukurasa wa nne, inazungumzia. Kwa hiyo,...

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Mwache amalize kusema, ndio utaratibu wetu. Muache amalize kusema.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Kiti chako kitumie busara, maelezo yaliyopo hapa yanaweza yakavuruga mwenendo wa kesi zilizopo Mahakamani. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Hoja zinazoendelea hivi zitavuruga uchunguzi. Kwa maana hiyo, kwa kuwa maeneo haya yanaonyesha nia njema ya kuisaidia nchi hii ili iwe na amani, basi nilikuwa napendekeza maelezo haya yapelekwe Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, naomba kiti chako kitutendee haki sisi ambao tuko wachache kwenye Bunge hili. Hiki anachokisema Mheshimiwa Mnadhimu Mkuu wa Upande wa Serikali, wamekizungumzia jana siku nzima, wametoa na wameshatoa hukumu, wametoa hukumu kwamba CHADEMA inahusika, na nilimsikiliza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akitoa maelekezo kwamba kuna watu wataitwa, wanatutisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni suala la kanuni, mimi sijawahi kuona tangu nimekuja kwenye Bunge lako Tukufu mtu anayesoma hotuba ya Kambi anakatishwa katikati, sijaona kwa upande wa Serikali, sijaona kwa upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani anayesoma maoni ya Serikali au maombi ya Kambi anazuiliwa kusema kile ambacho upande wake umemtuma kwa sababu ambazo zimetolewa kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Msemaji Rasmi wa Kambi Rasmi ya Upinzani alikuwa ndiyo kwanza anaanza...

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Tundu Lissu hoja yako inakuwaje?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Hoja yangu inasema kwamba, Msemaji wa Kambi Rasmi Bunge, aachiwe apate fursa yake sawa na upande wa Serikali ambao umetoa maoni yao, aeleeze msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani, azungumze anachotaka kuzungumza kama ambavyo upande wa Chama chenye Wabunge wengi humu Bungeni kimezungumza masuala haya tangu juzi. Vinginevyo, Bunge hili litakuwa halitendi haki kwa wale ambao ni wachache.

Mheshimiwa Spika, kanuni ya tano ya kanuni zetu inakutaka utende haki kwa pande zote, ututendee haki sisi ambao tuko wachache humu ndani. Nashukuru. *(Makofi)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kanuni ya tano inahitaji utende haki, lakini kutenda haki ni pamoja na kufuata kanuni zinazoendesha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, siyo kweli kwamba jana watu waliongelea mambo na kutoa hukumu, na kusema kwamba CHADEMA inahusika na mauaji. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Naomba tumsikilize ndiyo utaratibu wetu. Msikilize kama tunavyopenda kusikiliza kila mtu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nilisema zamani kwamba nidhamu inatupwa mkono na Mnadhimu Mkuu anayesimamia Kambi ya Upinzani. Nafikiri nidhamu inakuwa tatizo. Nakuhakikisha kwamba nidhamu ni tatizo ukienda hapo alipokaa, hiyo meza aliyokaa hiyo amevunja! *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Eeh! Waheshimiwa Wabunge, tungesikiliza hoja, naomba msikilize!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, jana jioni ...

SPIKA: Naomba msikilize kwa sababu sauti zenu zote zinasikika.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Waheshimiwa Wabunge ambao wataombwa kwenda kutoa maelezo watoe ushirikiano, na nilisema hivyo, maelezo haya ambayo yako ukurasa wa nne, hayo ndiyo yanatakiwa yasemwe huko. Narudia tena kwamba humu ndani ukurasa huo huo wa tatu na jambo hili wewe jana ulitoa uamuzi kwa kutumia kanuni ya 48 na nina imani kwamba Waheshimiwa Wabunge ambao wanajua hizi kanuni, na wenye nidhamu watakubali kwamba hili siyo jambo la kuingia kwenye hotuba hii.

Jambo lingine ni lile ambalo linazungumziwa kwenye ukurasa wa tatu *paragraph* ya mwisho, ile ambayo kila mtu anafahamu kwamba suala hilo liko kwenye upelelezi na mtu tayari ameshakwenda Mahakamani. Suala la Mheshimiwa Peter Msigwa na lenyewe liko Mahakamani, suala la Marehemu Msafiri Mbwambo mnaafahamu kwamba liko Mahakamani. Kwa hiyo, nilikuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwamba maneno haya yawe kwake, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Hamwezi kuwa wote mnatoa hoja zinazofanana halafu tukaendelea. Kwanza, kusema kwamba wanapozungumza Kambi ya Upinzani wanakuwa *interrupted* hiyo siyo utaratibu. Lakini yeyote atakayekwenda kinyume cha matakwa yetu ya kanuni atakuwa *interrupted* awe upande huu au upande huu.

Hiyo naomba iwe *very clear* na kwamba haijawahi kutokea asome *Hansard*, inatokea. *Provided* yule anayesema kitu kinakuwa kinyume na kanuni zetu atakuwa *interrupted* awe mtu mmoja, awe Kambi, awe mtu yeyote, hiyo mfahamu kabisa. Yeyote atakayekwenda kusema kitu

ambacho ni kinyume na kanuni zetu atakuwa *interrupted*, awe Waziri, awe Mbunge wa Chama chochote. Huo ndiyo utaratibu wetu. Ni kwa mujibu wa kanuni. Lakini kwa mujibu wa kanuni vilevile, mnaopenda kusema siyo tatizo, lakini yale yote yaliyoko Mahakamani kweli hapa yaliyoko mahakamani, hapana. Yaliyoko kwenye upelelezi mnaweza kusema, maana mtakuwa mnamsaidia Polisi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tuwe na heshima kwa Kiti, mimi sizungumzi ya kwangu, yaliyopo Mahakamani naomba mniambie ni yapi hayatapita hapa? Yaliyopo upelelezi, maneno yale yatakuwa ni sehemu ya upelelezi ukiitwa kusaidia itakuwa vizuri tu.

MBUNGE FULANI: Sawa!

SPIKA: Lakini yaliyoko Mahakamani, namwomba Mheshimiwa Vincent, tafadhali ipo kwenye kanuni yetu, ipo kabisa kanuni yetu ya 64 kwamba yaliyoko Mahakamani yasijadiliwe. Sasa mimi bahati yangu mbaya, sijui yapi yapo Mahakamani katika haya yaliyotajwa, lakini yaliyopo Mahakamani ni marufuku kuyasoma hapa.

Halafu kwa mujibu wa kanuni, mkitaka nitumie kanuni ya nane ndiyo inasema *impartiality of the seat*. Kwa hiyo, mimi mni-*clarification*, yapi yapo kwenye Mahakama. Yaliyoko kwenye Mahakama naomba mniambie na naomba wayaondoe yaliyoko Mahakamani.

MBUNGE FULANI: Wataje na kesi.

SPIKA: Yaliyoko Mahakamani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, nadhani wote tunazungumza kwa kujenga, hakuna mtu mwenye nia mbaya na mwingine. Mimi sina nia mbaya na rafiki yangu Mheshimiwa Tundu, wala Mhesgunuwa Vincent. *(Kicheko)*

SPIKA: Hapana, kwa hiyo, sisi tunaomba mambo yaliyoko Mahakamani...

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Naomba niseme mambo yaliyoko Mahakamani ambayo hata vyombo vya habari vyote, hata kama hatuko Mahakamani, vyombo vya habari vimeshaeleza.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe na nidhamu. Mimi nafikiri ya Mahakamani tumeyasikia jana jioni, ndiyo maana nikasema, wakati ule ilipotolewa pale nikawaambia vitu vilivyoko kwenye upelelezi viendeleo, ilikuwa asubuhi, nimesema mimi mwenyewe. Kwanini hampendi hata kusikiliza ukweli? *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): *Paragraph* ya kwanza, sisi wote tunafahamu Polisi...

SPIKA: *Paragraph* ya kwanza upande gani?

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Polisi waliwakamata watuhumiwa, wako Mahakamani. Kesi inaendeleaje, mimi sijui. Ukurasa wa tatu...

WAHESHIMIWA WABUNGE FULANI: Aaaaah!

SPIKA: Ipi hiyo? Jamani, mkitulia mimi nitaelewa. Haya, ipi? Anza upya, ukurasa gani? Anza!

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Ya pili, kesi ya Mheshimiwa Msigwa hata picha ya gazeti ninalo wakiwa mahakamani na Diwani Chonanga, na mimi yalipompata Msigwa nilikuwa Iringa kwa bahati njema nafahamu sana.

MBUNGE FULANI: Yaani unazungumzia jambo ambalo liko Mahakamani!

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Ndiyo nasema hili jambo liko Mahakamani.

SPIKA: Endelea usiwasikilize hao. Naomba nisikilize.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): La tatu, la Dkt. Ulimboka wote tumeshuhudia kukamatwa kwa mtuhumiwa..

WABUNGE FULANI: Ni kichaa!

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Kama ni kichaa Mahakama hawajasema ni kichaa, lakini mahakama imeshapokea kesi hii. Jimbo la

Irama Magharibi, mauaji yaliyotokea wiki hii, wameshakamatwa, wameshafikishwa Mahakamani. Halafu nyingine ambayo mimi najua ile ya Mwanza, waliotuhumiwa kuwaumiza Waheshimiwa Wabunge wawili walipelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, na mmojawapo alimtaja na Mbunge mwingine humu ndani na yule Mbunge akataja uthibitisho, kesi iko Mezani kwako. Kwa hiyo, yote mawili hayawezekani kwa sababu kesi moja iko kwako, inataka uthibitisho; na nyingine iko Mahakamani na Mheshimiwa Mbunge yumo humu ndani, anaendelea vizuri. Kwa hiyo, hayo ndiyo nilikuwa naomba kwa kweli kwa sababu yameshafikishwa mbele ya vyombo vya sheria, yasizungumzwe hapa.

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Naomba mkae, taarifa ipi? Kwamba kesi hizi haziko Mahakamani.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, naomba unisikilize, nina taarifa!

SPIKA: Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, mimi sio Mwanasheria, lakini ninachoelewa ni kwamba, kikanuni, hatutakiwi kuzungumzia mienendo ya kesi zilizopo Mahakamani, lakini hapa hotuba yetu inatoa maelezo ya awali ya kesi zilizo Mahakamani. Hakuna mtu anayejadili

mienendo ya kesi zilizopo Mahakamani, ndivyo ilivyo kwenye kwenye kanuni na *besides*, jana haya mnayosema ndiyo haya alikuwa anasema Mheshimiwa Tundu Lissu. Jana Mheshimiwa Kebwe pale amesema *live* kwamba CHADEMA mnahusika na ametoa hukumu kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu, na ndiyo maana hii ni *biasness* na hatukubali kama Bunge linaendeshwa hivi. (Makofi)

SPIKA: Kwa hiyo, wewe umesemaje Mheshimiwa Wenje, hebu rudia tena, maana hujasema kitu hapo. (Kicheko)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba, naomba uelewe basi na wewe unisikilize kwa makini ili uelewe. (Kicheko)

SPIKA: Wewe mwenyewe usiongee kwa jazba. (Kicheko)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Ni hivi, kwenye hotuba yetu, haizungumzii miendeno ya kesi zilizo Mahakamani, ni hotuba ambayo imetoa tu maelezo ya jumla ya kesi ambazo zimewahi kutokea ambazo zimepelekwa Mahakamani, hatujadili mienendo ya hizo kesi, na asome vizuri kwa sababu suala la *interpretation* ambayo Mheshimiwa Lukuvi anatoa au Mheshimiwa Werema kwenye hizo *paragraphs is out of context, is person interpretation guide by narrow minded*. (Makofi)

SPIKA: Ondoa maneno yako *narrow minded!* Hebu ondoa upesi! Unapo-*argue* siyo kutukana watu!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Naomba niondoe maneno hayo, lakini niseme *guided by narrow interpretation.* (Makofi)

SPIKA: Na wewe sema!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, naomba nieleze jambo ambalo liko Mahakamani, kesi huwa ina namba, huwa inataja Mahakama, huwa inataja wahusika, Bunge lako Tukufu linapewa maneno ya juu juu yasiyokuwa na ushahidi wowote! Hatujaambiwa kesi namba ngapi? Iko Mahakama gani? Inawahusu akina nani? Inahusu nini? Tunaambiwa tu mambo yako Mahakamani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, itakuwa ni kutokututendea haki kama hotuba yetu haitasomwa. Hotuba hii tumeipitia Kambi nzima, hakuna mahali popote humu ndani tunapotaja jambo ambalo liko Mahakamani, hatujataja kesi hata moja! Tumetaja matukio ya mauaji yenye sura ya kisiasa ni kweli, lakini hatujasema kwamba Mahakama haijasikiliza hili shauri, hatujazungumza chochote ambacho kiko Mahakamani.

Upande huu unaodai kwamba haya mambo yako Mahakamani walitakiwa wakueleze ni kesi namba ngapi? Mahakamani gani? Ni akina nani wanaohusika? Imefunguliwa lini? Haya maneno ya jumla jumla hayatoshelezi kutuzuia sisi kusoma maelezo ya kambi yetu. Tunaomba tutendewe haki na naomba kurudia kwamba tutendewe haki. Wale ambao wameyazungumzia masuala haya jana nzima watusikilize na sisi wasile keki yao halafu bado wadai kwamba ipo. *You can't eat your cake and still have it!* Huwezi ukazungumza wewe, halafu wakitaka

kuzungumza wengine, unasema aaah, lipo Mahakamani. Haiwezekani! Tutendewe haki. *(Makofi)*

SPIKA: Mimi ninachotaka, kama mngekuwa na busara, mngekuwa mnatumia maneno ya kujenga hoja, siyo mara mnakula keki, mara nini, yote yanawasaidia nini?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nilikuwa naomba mwongozo wako kutokana na kanuni ya 68(7).

SPIKA: Kanuni ya 68 (7) inasema nini?

MHE. CHIKU A. ABWAO: Inasema kwamba: "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema nakuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema."

SPIKA: Mbona mlikuwa mnasimama wakati wengine wanasema?

MHE. CHIKU A. ABWAO: Nimesimama mara tatu, bahati mbaya jicho lako halikuniona mapema.

SPIKA: Kwa hiyo hukupaswa kusimama wakati wenzako wanasema. Haya endelea.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Hoja yangu ni kwamba, nilikuwa naomba Mwongozo wako

kwa sababu Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani alikuwa ameanza tu kusoma hotuba yake, lakini Mheshimiwa Lukuvi akasimama na kueleza mpaka *paragraph* za mbele ambazo Msemaji hajaweza kuzifikia. Ni utaratibu upi ambao umepitishwa katika Bunge au kanuni ipi anayoitumia Mheshimiwa Lukuvi ya kuratibu hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani na kuanza kuitolea maelezo na kuipinga kabla haijasomwa katika Bunge lako Tukufu? (*Makofi*)

SPIKA: Kwa hoja hiyo Mheshimiwa Chiku Ambwao, ngoja kwanza. Naomba tusikilizane! Tukisikilizana, taratibu tunaweza kuelewa. Hoja ya Mheshimiwa Chiku Ambwao siyo ya msingi kwa sababu tunapo-*lay on the table*, yaani tunapoweka *documents* zozote Mezani, mtu anaweza kusoma mpaka mwisho, na akasema ukurasa fulani hautakiwi. Ndiyo sababu *documents* zote tunaweka juu ya Meza, ndiyo sababu hiyo. Kwa hiyo, mtu yeyote anaweza kusoma hata kabla. Kwa hiyo hoja hiyo haina msingi. (*Makofi*)

Sasa tabu niliyonayo, naomba sasa wote tusikilizane. Mheshimiwa Tundu, tunapoongea tunapenda watu wawe wanasikilizana. Sasa tunachokisema, kama suala liko Mahakamani, hilo wala siyo la ubishani wowote ule. Kifungu cha 64(c) kinasema: "Bila kuathiri masharti ya ibara ya 100 ambayo inahusiana na uhuru wa kuzungumza, yanamlinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge." Hiyo inasema hivyo. Lakini kifungu cha 64(c): "Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo linajadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia." Sasa tunachokisema kwa usalama wetu, zipo lawama nyingi sana tunazozipata katika Bunge letu,

tunaingilia vitu vya watu wanaofanya wengine, kazi zao mara nyingi tu, tunaingilia maamuzi mengine yako nje ya uwezo wetu. Kuna wengine mpaka wanataka kuingilia kufanya kazi za mashirika mengine.

Sasa mimi nasema, hizi hotuba zetu za kisiasa na mambo yetu ya kisiasa mengine ambayo yanahatarisha uhai wa nchi yetu, ni vitu ambavyo Waheshimiwa kama kweli mnaipenda nchi yetu hii, mnatakiwa mjilinde navyo.

Kwa hiyo, hapa sina ushahidi wa kesi zilizopo Mahakamani, lakini kama kuna kesi zilizopo Mahakamani kwa mujibu wa kanuni hii, hatupaswi kusema vitu vilivyopo Mahakamani. Kwa hiyo, hiyo ndiyo inavyotakiwa kuwa. Kwa hiyo, ningependa Waheshimiwa Wabunge hata kama mnatafuta, tunatafuta mambo ya kisiasa hapa na kuunganisha mambo ya kisiasa, lakini mambo yaliyoko Mahakamani, hapana.

Kwa mfano, kesi iliyopo Singida, leo walitaka kutoa kauli hapa Bungeni lakini hawataruhusiwa kwa sababu mimi nimesikia kabisa imepelekwa Mahakamani. Siyo lazima kesi namba, lakini tunajua kabisa Askari wamewashika watu na kuwapeleka Mahakamani na mnafahamu ipo sheria mtu akichukuliwa kwa uchunguzi katika muda wa saa 48 ni lazima apelekwe Mahakamani. Ndiyo hivyo tu.

Kwa hiyo, mimi nasema hizo kesi za Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Dkt. Ulimboka, Mheshimiwa Highness S. Kiwia ni lazima zitakuwa zipo Mahakamani, hakuna namna kwamba zitakuwa bado zinaelea tu mikononi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ukurasa wa tatu na wa nne, sitapenda Wabunge watakaozungumzia kesi zozote hata baadaye. Ukurasa wa tatu na wa nne Mheshimiwa Vicent naomba usiusome, tufanye mambo ya *order*, tutafanya na mambo mengine, lakini naomba usiusome.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kanuni ya 75, nitaisoma: "Kwa madhumuni ya kudhibiti fujo, endapo itatokea ndani ya Ukumbi wa Bunge na Spika ataona kuwa kuna hoja ya kutumia nguvu, basi anaweza kuahirisha shughuli za Bunge bila ya hoja yoyote kutolewa au kusitisha kikao kwa muda atakaotaja ili fujo hiyo iweze kudhibitiwa na upande wa Bunge."

Kanuni ya 75(1) "Baada ya utulivu kurudia, Spika atapeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge suala ambalo litasababisha kutokea kwa fujo ikiwa ni pamoja na jina la Mbunge au majina ya Wabunge waliohusika na fujo hiyo ili Kamati hiyo iweze kulishauri Bunge kuhusu adhabu inayostahili kutolewa."

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba watu wengi ambao wanatuangalia wanataka haki itendeke na haki hiyo ni kwa Wabunge wote, lakini pia haki hiyo ni kwa wale wanaolisikiliza Bunge hili. Ubishi uliopo kwa sasa hivi, unaonekana ungeweza ukasitishwa kama hotuba ile ya

Kambi ya Upinzani iliyotolewa ingeangaliwa na uthibitisho ukatokea kwamba mambo ambayo wanayazungumza yapo Mahakamani na hairuhusiwi.

Kwa mantiki hiyo, labda ni vizuri au ni busara tukasitisha hoja hii ili muda utolewe kuangalia ni mambo gani yamo katika Mahakama, na baada ya hapo, tunaweza tukaendelea. Pia mimi nawaomba wenzangu wote, sisi ambao tumetoka nje na wenyewe wanajua kwamba wananchi wanategemea sana Kambi ya Upinzani iwe na utulivu ili iweze kutoa mambo ambayo wananchi wanayategemea ili watu wote wasikilize kwa utulivu bila jazba na bila kuvunja madeski na utulivu huu ndiyo utamaduni wa Watanzania. Nawaomba watupe fursa ya kuwasikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Hoja aliyoitoa Mheshimiwa Cheyo ni kweli inaweza kutumika, lakini haitumiki kwa hatua hii, kwani hatujafikia hapo. Lakini tukitakiwa kufikia hapo inakuwa hivyo na wale ambao wanahusika wanatajwa kwa majina yao na wanapelekwa kwenye Kamati, na hatua nyingine zinachukuliwa. Kwa sababu umesoma hapo kwamba unatakiwa kutumia na Mpambe wa Bunge kabisa, kwa hiyo, inakuwa ni vurugu ile vurugu kabisa.

Sasa mimi ninachokisema ni kwamba, hii *paragraph* ya kutoka ukurasa wa tatu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani asiisome ili kusudi mchana tunakaa...

WABUNGE FULANI: Aaaah!

SPIKA: Naomba mnisikilize, kwa sababu nitawataja ndiyo mtaondoka kwa mujibu wa kanuni ya kanuni 75.

Sasa ninachokisema ni kwamba mchana tutakwenda kuangalia kama katika hizi zipo Mahakamani au vipi, kama hazipo nitaruhusu Kambi ya Upinzani kuja kutoa kauli humu ndani, lakini siyo kwa sasa hivi, kwa sababu tunabishana na hakuna mwenye uhakika kwamba ipo Mahakamani ama haipo Mahakamani.

Kwa hiyo, nataka mauaji yenye sura ya kisiasa irukwe, kama itaonekana hayapo, mtakuja kupata tena nafasi ya kuisoma tena.

Kwa hiyo sasa tunaendelea, maana yake hapa ni *chapter* yote ya mauaji ya kisiasa yanaachwa, kama kutathibitika hayapo Mahakamani nitawaruhusu kuja kuyasoma tena.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

SPIKA: Kwa hiyo, tunaendelea na ninaomba uingie ukurasa wa saba. Nimesema, atakuja kusoma baadaye!

Mheshimiwa AG!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, hatuna matatizo na maslahi ya Polisi na Magereza ambayo ipo ukurasa wa tano.

SPIKA: Ndiyo maana nimesema aanze ukurasa wa saba na baada ya hapo saa saba Kamati ya Maadili

itapitia hii hotuba na kama haihusiki, nimeshaamua na ninaomba Mheshimiwa Vincent aendelee.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Polisi na Magereza. Katika maoni yake ya mwaka 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamikia utamaduni wa Serikali kupuuza maslahi ya Askari Polisi na wale wa Jeshi la Magereza. Utamaduni huu ni wa muda mrefu sana. Kwa mfano, katika hotuba ya bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2006/2007, aliyekuwa Waziri wakati huo alikiri kwamba: "Kutokana na kipato kidogo cha Askari Polisi, inawawia vigumu kukopa katika mablenki nchini kutokana na riba kuwa kubwa na kukosa dhamana za uhakika. Hivyo, Askari Polisi hawana mahali popote wanapoweza kupata fedha za kujiendeleza kiuchumi. Aidha, mishahara na posho wanayolipwa Askari bado haikidhi hali halisi ya mahitaji yao na familia zao."

Mheshimiwa Spika, toka wakati huo hadi sasa, maslahi ya Askari Polisi yamekuwa mabaya zaidi kutokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi na Mfumuko wa bei hasa za vyakula, kupanda wakati ambapo mishahara yao haijaongezeka, sambamba na ongezeko la gharama halisi za maisha. Aidha, katika hali inayoonyesha kutokujali kabisa maslahi na hali za maisha za Askari wetu, Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake iliyotolewa tarehe 17 Novemba, 2011 na aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya ndani - Mheshimiwa Khamis Sued Kagasheki, aliyeliambia Bunge hili Tukufu kwamba: "Posho ya Askari imepandishwa na kwamba inatakiwa itoke kwenye Sh.100,000/= mpaka Sh. 150,000/=. Ni jambo ambalo tunalo na tumelifanyia kazi

na tuna uhakika kwamba, litaweza kutimia." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usio na mjadala kwamba Askari Polisi na Magereza bado wanapokea posho ya kujikimu ya Sh. 100,000/= badala ya Sh. 150,000/= iliyoahidiwa na Serikali mbele ya Bunge hili Tukufu. Aidha, katika mazingira ya kushangaza kabisa, mara baada ya Serikali kutoa ahadi Bungeni juu ya posho hiyo, uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi ulituma maelekezo kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa kufanya uchunguzi ili kubaini Askari wote waliokuwa wanadai walipwe posho ya Sh. 150,000/= kama ilivyoahidiwa ili Askari hao wafukuzwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, ni lini italipa malimbikizo ya baki ya Sh. 50,000/= kwa mwezi kwa kila Askari Polisi na Magereza ambayo haijawalipa Askari hao hadi hivi sasa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ianze kuwalipa Askari Polisi na Magereza posho ya kujikimu ya Sh. 150,000/= kwa mwezi kuanzia mwaka huu wa fedha, kwa vile ahadi ya Serikali iliyotolewa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani haijawahi kukanushwa, kubatilishwa au kubadilishwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwamba Serikali haitekelezi ahadi inazotoa Bungeni juu ya malipo ya Askari Polisi na Magereza, Serikali pia imekuwa inawakopa watumishi hao bila ridhaa yao. Kwa mfano, randama ya fungu la 29 inaonyesha kuwa Jeshi la Magereza linadaiwa jumla ya Shilingi bilioni 23.65. Kati ya fedha hizo, watumishi wa Jeshi la Magereza wanadai Serikali jumla ya Shilingi bilioni 10.34

ambazo ni malipo ya stahili zao mbalimbali kama vile fedha za likizo, uhamisho, mafunzo, na kadhalika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili, ni lini italipa madeni haya ya Askari Magereza wetu wanaokeshwa Magerezani usiku na kushinda juani mchana wakiwalinda wafungwa na mahabusu waliojaa katika Magereza ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, kuna hatari kwa Askari wa Jeshi la Magereza kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo tumeyaeleza katika maoni haya, mfano ni katika Jimbo langu la Musoma Mjini.

Mbali na makazi duni ya Askari Magereza, vile vile kuna umbali mrefu kati ya Kambi ya Askari Magereza ya Nyasho na Gereza la Mkoa lililopo Kata ya Mkendo na Askari Magereza wamekuwa wakitembea kwa miguu usiku wanapokuwa zamu Gerezani. Hii inahatarisha usalama wao, kwani wanaweza kuvamiwa na kudhuriwa na wafungwa au mahabusu waliokwisha kumaliza adhabu zao lakini wakawa na visasi na Askari hao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwapatie gari Askari wa Kambi ya Nyasho na makazi mengine ya Askari Magereza yaliyoko mbali na Magereza wanakofanyia kazi ili kunusuru maisha ya Askari Magereza wetu.

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya mwaka 2011, tulipendekeza kwamba: "Utaratibu wa sasa wa Polisi wa ngazi za chini kukatwa Sh. 5,000/= kila mwezi kwenye mishahara yao kwa ajili kugharamia mazishi yao na wategemezi wao, ufutwe mara moja, kwani unawanyonya kwa sababu vipato vyao ni vidogo. Badala yake, Serikali ibebe jukumu hilo." Hata

hivyo, hadi tunaandika maoni haya, Serikali imeendelea kupuuza mapendekezo haya kwa kisingizio kwamba Mfuko wa Kufa na Kuzikana ni wa hiari, ilhali Askari Polisi wanaendelea kukatwa mishahara yao kwa lazima. Kwa mara nyingine tena, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatamka kwamba kukata mishahara wa mfanyakazi bila ridhaa yake wakati hadaiwi chochote na mwajiri wake ni kinyume cha sheria husika za nchi yetu na kitendo cha Jeshi la Polisi kuendelea kukata mishahara ya Askari Polisi kwa ajili ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana bila ridhaa ya Askari Polisi wenyewe kikome mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba Askari Polisi wanaofanya kazi za lindo katika mablenki yote ya biashara hapa nchini hulipwa posho ya Sh. 10,000/= kwa siku. Hata hivyo, Serikali haijawahi kutamka hadharani kiasi ambacho mablenki hayo hulipa Serikalini kwa ajili ya kazi hiyo ya kulinda mablenki binafsi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu kiasi ambacho mablenki ya biashara hulipa Serikalini kwa ajili ya huduma ya ulinzi inayotolewa na Askari Polisi ili Bunge lako lifahamu kama Askari Polisi wanaofanya kazi hiyo wanalipwa inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Hali ya Uchumi wa Taifa, makosa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo mbalimbali vya Polisi hapa nchini yalikuwa 62,133. Ripoti inasema kwamba kwa mwaka 2011 makosa 63,703 ya jinai yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko hili la uhalifu linasababishwa na Askari wa doria kushindwa kufika kwenye maeneo ya matukio ya uhalifu

kwa haraka pindi wapatapo taarifa kwa kisingizio cha kukosa mafuta kwa ajili ya magari ya doria.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nyaraka za Serikali zinaonyesha kwamba Bunge lako Tukufu limekuwa likiidhinisha fedha nyingi kwa ajili ya mafuta ya magari ya Jeshi la Polisi. Kwa mfano, kwa mujibu wa randama ya Fungu la 28 kwa mwaka huu wa fedha, matumizi halisi ya mafuta kwa ajili ya Jeshi la Polisi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalikuwa Shilingi bilioni 2.81. Aidha, katika mwaka wa fedha uliopita, Bunge lako Tukufu liliidhinisha Shilingi bilioni 2.61 kwa ajili ya mafuta, wakati ambapo kwa mwaka huu wa fedha Serikali inaomba Bunge liidhinisha Shilingi bilioni 2.56 kwa ajili ya mafuta ya magari ya Jeshi la Polisi.

Wakati Bunge limekuwa likiidhinisha mafungu haya makubwa ya fedha kwa ajili ya mafuta, Askari Polisi wamekuwa wakilalamika kwamba hawapewi fedha za mafuta kwa ajili ya magari ya doria, hivyo kusababisha Askari Polisi kushindwa kufanya kazi zao ipasavyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze zinakopelekwa fedha za mafuta kwa ajili ya Jeshi la Polisi kama gari moja la doria linapatiwa lita tano za mafuta kwa kutwa na/au usiku.

Mheshimiwa Spika, mipaka yetu na nchi jirani zinazotuzunguka imekuwa pakacha linalovuja. Ndiyo maana katika hotuba yetu ya mwaka 2011 tuliliambia Bunge lako Tukufu kwamba: "Kumekuwa na ongezeko la wageni wengi kutoka nchi za nje, kiasi cha kujiuliza kama nchi hii ina utaratibu wowote wa kuratibu na kudhibiti uingiaji wa wageni hapa nchini." Tulionyesha jinsi ambavyo kumekuwa na ongezeko la wageni haramu kutoka nchi za

Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi, Rwanda, Kenya, Uganda, Pakistan, Nigeria, China, India na Bangladesh “ambao wanaishi Tanzania kwa mfumo usio rasmi, bila ya kuwa na hati zinazowaruhusu kufanya hivyo.” Tulitahadharisha kwamba “utaratibu wa kuachia kila mgeni kuingia Tanzania na kuishi atakavyo bila ya vyombo husika kujua kuwepo kwake ni hatari kiusalama, hasa katika zama hizi za kusambaa kwa ugaidi na uharamia wa kimataifa katika masuala ya fedha, biashara za binadamu na kadhalika.”

Mheshimiwa Spika, maneno na tahadhari zetu ziliangukia kwenye masikio ya Serikali kiziwi. Sasa yale tuliyoyasema, yameanza kutimia. Kwani ni mwezi mmoja tu umepita tangu wahamiaji haramu zaidi ya arobaini kutoka Ethiopia kukutwa wamekufa ndani ya lori la mizigo ambalo kwa vyovyote vile lilitokea nchi jirani. Watu hawa waliingiaje nchini na kusafiri hadi katikati ya nchi yetu bila kujulikana na Maafisa wa Uhamiaji, Polisi wa Usalama Barabarani na Usalama wa Taifa kama kweli nchi yetu iko salama? Ni Afisa gani wa Idara ya Uhamiaji aliyewapitisha katika mpaka wetu wa Namanga au Horohoro au Sirari au Kogaja au Borogonja? Ni Askari Polisi gani aliyewasindikiza hadi Kongwa? Aidha, ni Afisa Mizani gani wa *TanRoads* aliyepitisha lori walimokuwa watu hao bila kulikagua na kujua kilichokuwemo?

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea, kwa kuzingatia ukubwa na uzito wa kashfa hii, viongozi waadilifu katika Wizara, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Polisi wangewajibika kutokana na uchafu huu. Hata hivyo, hakuna hata mmoja ambaye amefanya hivyo. Kwa vile uwajibikaji wa hiari unaelekea kushindikana, Kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni inamtaka Rais Kikwete kutumia mamlaka yake ya kikatiba kuwawajibisha wale wote waliohusika kuanzia viongozi wa Wizara walioko humu Bungeni na uongozi wa juu wa Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Polisi ili kuondokana na aibu hii ya nchi yetu kuwa *transit route* ya biashara ya kusafirisha binadamu katika sehemu hii ya Bara la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo ya ongezeko la wahamiaji haramu katika nchi yetu linatokana na Idara ya Uhamiaji kuendekeza vitendo vya kifisadi katika kuajiri, kupandisha madaraja au vyeo wa Maafisa wa Idara hiyo. Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo, ajira katika Idara ya Uhamiaji haizingatii tena elimu, uwezo na weledi wa Maafisa husika. Bali, kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti wa Mpango Mkakati wa Mageuzi Katika Utumishi wa Uhamiaji (*Immigration Service Reform Programme Strategic Plan Research Report*) iliyochapishwa na Wizara ya Mambo ya Ndani tarehe 27 Novemba, 2011, inasema: "Mara nyingi mgawanyo wa kazi (katika Idara) haitegemei sifa bali unategemea upendeleo, rushwa, kujuana na urafiki, vitu ambavyo viko kinyume na maana halisi ya mgawanyo wa kazi." (*Most of the time placement is not based on merits but depends on nepotism, bribery and technical know-who, friendship and favouritism that have been contrary to the whole meaning of placement*).

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa kauli hii unapatikana katika Taarifa hiyo ya Utafiti inayoonyesha kwamba maafisa wengi wa ngazi za juu katika Idara ya Uhamiaji ni watu wenye uwezo mdogo kielimu kulinganisha na maafisa wa ngazi za chini wa Idara hiyo. Kwa mfano, katika ngazi ya Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji kwenda juu hadi kwa

Kamishna Mkuu, kuna maafisa 10 wenye shahada ya uzamili (*masters degree*), wawili wenye *post-graduate diploma (PGD)*, 24 wenye shahada ya kwanza, tisa wenye stahada, saba wenye *diploma*, 11 wenye Kidato cha Sita na 248 wenye elimu ya Kidato cha Nne. Katika maafisa hawa wa ngazi za juu, kuna Kamishna mmoja mwenye elimu ya Kidato cha Nne, wakati kuna Makaimu Kamishna 216 wenye elimu hiyo ya Kidato cha Nne na Kamishna Wasaidizi Wakuu 31.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, kuanzia ngazi ya Mratibu Mwandamizi (*Senior Superintendent*) kwenda chini mpaka Koplo, kuna maafisa wenye shahada ya uzamili 36, wenye *post-graduate diploma* wako saba, wenye shahada ya kwanza wako 340, wenye stahada wako 78, *diploma* wako 10, wenye cheti (*certificate*) wako 52, waliomaliza Kidato cha Sita wako 585 wakati waliohitimu Kidato cha Nne wako 337. Katika mazingira ambayo maafisa wenye uwezo mkubwa wa elimu hawapewi nafasi za juu katika Idara, badala yake uongozi wa juu umejazwa na wenye elimu za mashaka kama inavyoonyeshwa katika Taarifa ya Utafiti ya Wizara, ni wazi kwamba matukio kama ya maafa ya wahamiaji waliokutwa wamekufa Jimboni kwa Naibu Spika wa Bunge hili Tukufu, hayawezi kuepukika.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mazingira ya upendeleo na rushwa katika ajira ya Idara ya Uhamiaji ya aina hii, Maafisa Uhamiaji hawawezi kuacha kutumiwa na wanasiasa wa Chama Tawala kuwatuhumu washindani wao kisiasa kuwa sio raia wa Tanzania ili kuwaondoa katika kinyang'anyiro cha chaguzi zetu. Hivi ndivyo ilivyotokea kwa Mheshimiwa Ali Mohamed Keissy alipotaka kugombea Ubunge kwa tiketi ya CHADEMA na kuzushiwa tuhuma

kuwa sio raia. Hata hivyo, alipojiunga na CCM bila ridhaa yake, tuhuma za kutokuwa raia ziliyeyuka na sasa ni Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini katika Mkoa anakotokea Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu juu ya mambo haya ambayo yamethibitishwa na Ripoti ya Utafiti ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Aidha, Kambi inaitaka Serikali itoe kauli kama kuna haja yoyote ya kutumia mamillioni ya fedha za wananchi kusomesha Maafisa wa Idara ya Uhamiaji ambao baada ya kufuzu hawapatiwi vyeo na majukumu yanayolingana na uwezo wao wa kielimu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, umuhimu wa Jeshi hili unaonekana pale yanapotokea majanga ya moto, mafuriko au maafa mengine kama vile tetemeko la ardhi ambapo athari za matukio haya ni makubwa sana na mara nyingi hupelekea wananchi kupoteza maisha. Malalamiko ya wananchi katika maeneo mbalimbali juu ya Jeshi la Zimamoto kuchelewa kufika katika maeneo ya tukio, yamekuwepo kwa miaka mingi na yamepigwiwa kelele sana hapa Bungeni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia ushauri wake kuwa, Serikali iboreshe mfumo mzima wa Zimamoto katika nchi yetu ili kukabiliana na majanga ya moto yanayoongezeka kutokana na kupanuka na kukua kwa Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo na kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Kama nilivyosema mchana, Kamati tutakaa, tutapitia *chapter* ile iwapo tutakuta kuna mambo yaliyoko Mahakamani hayataruhusiwa, iwapo yatakuwa hayapo Mahakamani yataruhusiwa. Kwa hiyo, sasa naomba Kamati ile ya Maadili ipitie hii *chapter*, lakini wakati huo huo naomba Wizara na wanaohusika waweze kutupa ushahidi katika maeneo hayo, ili kazi yetu ikawe rahisi zaidi.

Wakati tunaposubiri hayo, naomba niwaite wataochangia, kwa sababu tunakaribia kumaliza muda, watakuwa wachache. Nina watu ambao walipaswa kuchangia mchana, lakini kwa sababu maalum watachangia sasa hivi. Nitaanza kwanza na Mheshimiwa Juma Othman Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Filikunjombe, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Lugola. Hawa wanaweza kupata nafasi asubuhi hii. Mheshimiwa Othman.

MHE. JUMA OTHMAN ALI: Mheshimiwa Spika wa Bunge, ahsante sana.

SPIKA: Naona kama *microphone* yako haifanyi kazi vizuri.

MHE. JUMA OTHMAN ALI: Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu naomba kulishukuru Bunge lako Tukufu pamoja na wewe mwenyewe Spika, kwa kuweka hali ya utulivu katika Bunge, na vilevile kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kwanza, hapana budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa nafasi aliyopewa ambayo ni ngumu na nzito sana. Kwa hiyo, nampa hongera na

kumtaka kwanza akaze buti, asisikilize maneno ya kuambiwa, afuatilie yeye mwenyewe kwa sababu zangu maalum, kwamba mimi ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini pia nina mfanyakazi wa Jeshi la Polisi ambaye ninaona shughuli anazofanya, na hapa nimemwona rafiki yangu mpendwa sana anaitwa Mussa Ali Mussa ambaye ameshawahi kuwa katika Kituo cha Polisi Mkokotoni. Anajua Jimbo langu lina mazingira magumu sana kwa sababu lina sehemu za kisiwa na ng'ambo. Kwa hiyo, moja kwa moja anajua sana kwamba, kisiwa ni sawasawa na Kontena ambalo kila kitu kinakuwemo mle, kama huna ufuatilie. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara itoe kipaumbele katika kuviangalia sana visiwa vyetu vilivyozungukwa na Bahari ya Hindi. *(Makofi)*

Jambo lingine ninalotaka kuchangia ni kwamba, ni lazima *Police Marine* iwepo Mkokotoni ili iwasaidie askari wetu kwa huduma za kwenda na kurudi Tumbatu. Naiomba Serikali, suala hili ni moja kwa moja, naomba *Police Marine* iwepo Mkokotoni kwa sababu eneo hilo niko karibu nalo. Naishukuru Wizara kwamba kituo changu cha Polisi pale Mkokotoni kilipata ajali ya kuungua moto, hivi sasa marekebisho ya kutaka kujengwa kwa kituo hicho yameshaanza. Kwa hiyo, natoa hongera sana kwa Wizara, naomba ijitahidi hivyo hivyo kwa sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kuna kifungu kimoja mimi sitaweza kuongelea sana kwa sababu nilipofika hapa naliangalia hili Bunge letu, linawatia matatizo Askari wetu ambao wanafanya kazi usiku na mchana; jua lao, mvua yao. Kwa hiyo, naona uchungu sana kuwa kila Askari anakuwa na matatizo na masuala ya majukumu sana.

Hawalali nyumbani, sisi tunalala katika nyumba zetu na watoto wetu, tunapata raha, wao kucha hawalali kwa kutulinda sisi. Kwa hiyo, nawapa hongera sana! Hongera sana! Hongera sana! *IGP* ni mtu mzuri sana anayeweza kazi yake vizuri sana, aendeleo na msimamo huo huo, asishughulike na mawimbi ya baharini. Asishughulike kabisa, kwani mawimbi ya baharini yanaweza yakaja matatu, lakini kama nahodha ni mzuri, utakivusha chombo tu. Kwa hiyo, moja kwa moja namwombea dua kwamba, akivushe chombo mpaka mwaka 2015 wembe ni ule ule. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ushindi ni lazima. (*Makofi*)

MHE. JUMA OTHMAN ALI: Ahsante sana kwa kujazia hilo, ushindi! Kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijasahau, niseme tu kwamba, siungi mkono hoja kwa sababu hali ya Magereza kule Ludewa ni mbaya sana. Gereza letu la Ludewa limetelekezwa, limesahaulika kabisa, majengo sasa hivi yamekuwa ni makuukuu, ni machakavu na yamechoka na ukienda kwenye lile Gereza unafika mahali huwezi kutofautisha nani ni askari na nani ni mfungwa. Wafungwa wako katika hali mbaya na Askari Magereza nao wana hali mbaya. Siungi mkono hii hoja mpaka hali hii kule Ludewa itakaporekebishwa.

Haya mambo ya kwamba, Magerezani hali ni mbaya, tumekuwa tukisema kila mwaka, lakini hakuna anayesikiliza na hakuna anayejali. Tufike mahali sasa tupendekeze humu ndani, kama nyie wenzangu hamtaki kuunga mkono, mimi

nawaombea kabisa, Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu wake, hata wafungwe kwa mwaka mmoja au miezi sita, wakae Gereza na watakapotoka ndiyo watakapoweza kuja hapa na kusema yaliyopo kule ndani na ndipo watakaporekebisha hali iliyoko kule ndani. *(Makofi)*

Hali ya Magereza yetu haiwezi kuendelea kubaki katika hali ile. Gereza la Ludewa kuta zimebomoka, nyumba za wafungwa zimebomoka, gereza linavuja, halina jiko, viongozi tunao, fedha tunapitisha, lakini haziendi kurekebisha hali ya Magereza yetu. Ndiyo fedha ni kidogo, lakini tuzitumie inavyotakikana. Wale wafungwa nao ni binadamu, Askari Magereza wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, mimi siungi mkono hoja mpaka hali ya Gereza la Ludewa itakapobadilishwa, na hata pengine kama Waziri atakuja kufungwa nitaomba ufungwe Gereza la Ludewa ili aje ashuhudie na aniunge mkono humu ndani siku hiyo baada ya kutoka.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Polisi linafanya kazi katika mazingira magumu sana. Tumefika mahali sote tumeridhika tunaweka kipaumbele katika masuala mengine na tumesahau kabisa kwamba kipaumbele chetu sasa hivi hapa kinapaswa kiwe ni suala la usalama. Tunapozungumzia suala la usalama, Askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kila mwaka tunaajiri Askari, tunasahau kwamba ni afadhali tukawa na Askari wachache wakafanya kazi katika mazingira mazuri, wakalipwa mishahara mizuri na wakapata vitendea kazi bora. Tufike mahali tuzingatie ubora, tufike

mahali sasa Jeshi letu lipewe vifaa vya kufanyia kazi, vifaa vya kisasa kwa ajili ya upelelezi, vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuzuia uhalifu; Jeshi letu lipewe vifaa vya kisasa kwa ajili ya *counter surveillance* pamoja na *surveillance*. Jeshi letu halina vifaa vya kisasa kabisa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *na-declare interest* kwamba nilikuwa Askari. Afande *IGP* utaniwia radhi, ninatoa siri za Jeshi lako, lakini ni ukweli usiopingika kwamba Jeshi la Polisi halina vifaa kabisa! Zipo silaha chache, kama kuna vifaa vingi ambavyo Jeshi la Polisi linavyo leo hii, ni virungu. Virungu viko vingi sana, nadhani, sijui ni kwa ajili ya kupigia wanafunzi wa Chuo Kikuu wakigoma au vya kuwapigia CHADEMA, sijui! Lakini kwa hakika hatuwezi kuendesha Jeshi la Polisi kwa virungu peke yake. Muda umefika sasa Jeshi la Polisi liwezeshwe, liwe na vifaa vya kisasa vya uhakika kwa ajili ya kuweza kupambana na wahalifu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi liko nyuma, lakini wahalifu wako mbele kiteknolojia na sayansi. Hatuwezi kwenda! Amani tuliyonayo sasa hivi tunaichezea, *we take it for granted*. Tunadharau, lakini amani hii ni lazima ilindwe kwa gharama yoyote ile. Ni lazima tuilinde amani yetu!

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunakuomba sana utenge fedha za kutosha. Waheshimiwa Wabunge tuwaunge mkono Askari wetu. Askari tunao, wamesoma, lakini hawana vitendea kazi. Vitendea kazi ni jambo muhimu sana. Narudia tena, ni bora ukawa na jeshi dogo la kisasa kuliko kuwa na jeshi kubwa linalofanya kazi kizamani. Muda umefika sasa, ni lazima Wabunge tuunge mkono, tuisitize Serikali yetu itoe fedha kwa ajili ya Jeshi letu la Polisi ili liweze kufanya kazi ya kulinda raia pamoja na mali zake.

Mheshimiwa Spika, yasipofanyika haya mawili, naomba kusema sitaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Askari mwingine, Mheshimiwa Kangi Lugola. (*Kicheko*)

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, nianze kumkumbusha rafiki yangu Filikunjombe kwamba, amesahau kifaa kingine ambacho Jeshi la Polisi wanajivunia sana kwamba ndiyo zana ya kufanyia kazi, ni filimbi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema sikubaliani kabisa na kupitisha bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Wabunge wenzangu, wananchi mnaonisikiliza, Wizara hii ni nyeti na naomba wakati nazungumza kila mmoja awe anatafakari mambo yafuatayo: Kupanga ni kuchangua. Leo ndiyo siku ya kuchagua, Wabunge na Watanzania ama tuendelee kuwa na uhalifu hapa nchini ama tuondokane na uhalifu hapa nchini. (*Makofi*)

Mwanafalsafa mmoja *Abraham Maslow* alipofanya utafiti alisema, mwanadamu anayo mahitaji kwa vipaumbele. Akaja na *hierarchy of needs* akasema, hitaji la kwanza mwanadamu akishakula, akanywa maji na akavaa, kitu cha pili anachofikiria kifuatake ni usalama (*protection*).

Waheshimiwa Wabunge, hali ya kiusalama, ujambazi unatokea, watu wanabakwa, majini kule wavuvi wangu wanakuwa *harassed*, wananyang'anywa nyavu; leo

naomba niwaaminishe kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi, lazima tuipe kipaumbele kama tunataka kuondokana na uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, bajeti ya mwaka 2010 ilikuwa asilimia 71 waliyopata Wizara ya Mambo ya Ndani, mwaka uliofuata ilikuwa ni asilimia 79 na hivi ninavyozungumza bajeti tunayoimaliza ni asilimia 74. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nyerere anaposema Jeshi la Polisi mafuta wanapeleka wapi, mafuta yanaishia kwenye makaratasi haya mnayokubali kupitisha hapa. Kule, fedha haziendi! Hizi asilimia mtazuia uhalifu gani? *(Makofi)*

Naomba mtafakari jambo ninalotaka kuliongelea. Hivi sasa tunavyozungumza wahalifu kama sehemu ya jamii ni wadau wakubwa katika bajeti hii, na sasa wanatusikiliza, wanataka kujua Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi, wamejipanga kiasi gani? Wana bajeti kiasi gani ya kupamba nao?

Waheshimiwa Wabunge, Jeshi la Polisi walianzisha programu ya maboresho, Mheshimiwa Rais akasema sasa maboresho haya ndani ya kuwa na Jeshi la Kisasa la Weledi pamoja na Polisi Jamii ndani ya miaka mitano, wapate Shilingi bilioni 294 na kuanzia mwaka juzi wa fedha waanze na Shilingi bilioni 58. Fedha hizo za programu Mheshimiwa Waziri ziko wapi? Humu mbona sizioni? Utakuwa na Jeshi gani hili la virungu na filimbi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuwaondoe wahalifu, lazima ndani ya ukisasa tuwe na mambo yafuatayo: Vifaa au vitendea kazi vya udhibiti. Huwezi kudhibiti uhalifu kwa kupanua Magereza. Humu ndani sijui tuongeze mabweni ya

wafungwa! Kuondoa msongomano, suluhu siyo kupanua Magereza au kuanzisha Mahakama ya Jinai. Suluhu ni kudhibiti uhalifu ili wasitokee wahalifu wa kwenda Magerezani. Kudhibiti uhalifu ni vifaa vya kisasa. Lazima Miji yetu mikubwa, Mwanza, Dar es Salaam na Mbeya, tufunge Kamera ambazo Askari wachache wataalam wana uwezo wa kudhibiti wahalifu. Kwenye *crime scene* lazima waende na magari ya kisasa ambayo yana vifaa kwa ajili ya kuchukua vitu vya kwenda kutambua. Lazima *DNA* zifanye kazi.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, hakika kama hutakuwa na vifaa vya kisasa, Jeshi lako litaendelea kuwa nyuma ya wahalifu na wahalifu wataendelea kuwa mbele. Hatuwezi tukawa na bajeti ambayo ni sawa na kuota moto kwa foleni. Mtu wa mwisho atapata moto saa ngapi tunapoota bajeti ya foleni? Lazima tuwe na bajeti ya mduara, kwa maana tunaota moto kila mmoja amezunguka anapata lile joto la bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanini tunarudi kwenye makosa yale yale ya bajeti zile zile za kila mwaka? Hii inanikumbusha ninapoonna nguzo ya *TANESCO* imeandikwa maandishi ya *danger*. Utakuta mtu ndiye anakwenda kujisaidia pale haja ndogo, wala haogopi kwamba kuna *danger*. Kwanini hatuogopi bajeti ambazo haziondoi uhalifu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanini Wanajeshi wanapata Sh. 225,000/= ? Humu ndani tumeambiwa Askari Polisi mwaka uliopita 2011 wameumizwa 62, wameuawa 16, Wanajeshi mazingira yao na ya Polisi katika kuuawa na kuumizwa ni yale yale, kwanini Polisi nao wasipate Sh. 225, 000/= kama

Jeshi? Halafu Waziri unaandika humu ndani kwamba, hii ni posho ya morali. Hii siyo posho ya morali, hii ni posho ya lishe kwa ajili ya kutengeneza Askari awe na *physique*, asiwe na kitambi ambacho hakina utaratibu, Askari ambaye mhalifu akimwona ana silaha anaweza kujua kwamba hawezi kumnyang'anya. Kule Songea ilitokea walinyang'anya Askari wawili silaha. Kwa sababu gani? Kwa sababu majambazi wanamwona huyu ni legelege, hana lishe, yanakwenda tu na kumnyang'anya silaha. Kwa hiyo, maslahi haya ya posho ya chakula, siyo morali, ni kumtengeneza Askari katika lishe, na katika ukakamavu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata ukienda Dodoma hapa unakuta Askari mwenyewe ndiye amejijengea nyumba kwenye eneo la Polisi. Hii ni aibu! Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ni aibu kubwa! Askari hapa Dodoma amejijengea nyumba yeye mwenyewe kwenye eneo la Polisi. Kwa sababu gani? Kwa sababu pamoja na kutokuwa na nyumba za kutosha, wanapewa asilimia 15 ya pango la nyumba. Kule Mjini asilimia 15 kwa ajili ya pango la nyumba, utapanga nyumba ya nani Mheshimiwa Waziri, hata ukiwa ni wewe? (Makofi)

Tunasema kwamba, taarifa muhimu sasa hivi zinanunuliwa kwa fedha mbaya. Lazima tuwezeshe Jeshi la Polisi kwenye *criminal investigation fund* ili kitengo cha intelijensia wawe na uwezo wa kununua taarifa. Taarifa za kihalifu sasa hivi zinauzwa kwa bei mbaya, kwa sababu mtu anajua akimsema mhalifu, kesho yake anaweza kuuawa. Nimeona humu fedha za mafuta zimekatwa, hawana mafuta ya kutosha wakati doria ndizo zinazodhibiti uhalifu katika nchi yoyote ile. Wekeni mafuta ya kutosha, suala la

kuwa na magari siyo tija, suala ni mafuta ndani ya magari ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mtandao mkubwa ndani ya Jeshi la Polisi na ushahidi ninao, wanatoa taarifa za wananchi wanaomiliki silaha kwa wahalifu ili wahalifu wajue wananchi wana uwezo kiasi gani wa kujihami ili waende wafanye uhalifu. Naomba *IGP* unayenisikiliza anza na mtumishi wenu anaitwa Fadhiri Kweka, ana mtandao wa uhalifu ndani ya Jeshi la Polisi. Hainiingii akilini anapata wapi taarifa za wananchi wanaomiliki silaha, halafu anawapatia watu wengine ambao ni wahalifu. Anzeni na huyo na nitawapa ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nimalize na suala hilo la hivi vifaa vingine vya uhalifu vya kisasa ambavyo unaweza ukaenda kwenye eneo ukachukua hata kama ni kisu kimemchoma mtu, kimebaki, mkapeleka kwenye mtambo wa kutambua picha, baadaye wakafuatilia wakajua nani ametumia kisu hiki, halafu wakamkamata. Halafu kuna *interceptor mobile phones*, jambazi ambaye anatumia simu na Polisi wanajua simu yake, wana uwezo wa kutumia *interceptor* wakam-*trace* mahali alipo na wakamkamata. Hivi ndivyo vifaa vya kisasa. Siyo suala la kuwa na filimbi pamoja na virungu, hatutaondoa wahalifu hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumze kwamba, Askari akilewa pombe anaambiwa umekwenda kinyume na mwenendo mwema wa Jeshi la Polisi, anafukuzwa kazi. Lakini Waziri, Katibu Mkuu, *IGP* ambaye anavunja sheria ya kutompatia makazi Askari akae Kambini ambapo na penyewe ni kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, kwanini na wao wasichukuliwe hatua kwamba, wameshindwa kufanya

kazi na wao wakafukuzwa kazi kwa sababu wote wamekwenda kinyume na masuala ya sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *ni-declare interest*, mimi nimekuwa Polisi nimekuwa *on the ground*, huwezi kuondoa uhalifu nchini bila ya kuwa na vitendea kazi. Mke wangu pia na yeye ni Polisi mpaka sasa. Naomba aniwie radhi kama nimeongea jambo ambalo linaudhi Taasisi yake, nikirudi kule nyumbani asije akakataa hata kunigeukia mmh! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka kuwe na fedha za kutosha kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Kwa mara ya kwanza nimekwishajua kumbe Bunge hili limejaa wanawake na wanaume Polisi tu. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Amina Andrew Clement. Kwa muda tulionao huu nafikiri na Mheshimiwa Zaynabu Vullu atafikiwa.

MHE. AMINA A. CLEMENT: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa leo katika Bunge lako Tukufu nikaweza kuchangia nami katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza nichukue fursa hii tena kuwashukuru na kuwapongeza sana Askari wa Jeshi la Polisi kwa kazi zao nzuri wanazozifanya za kukaa na kutulinda sisi na kututetea. Sisi tumekaa hapa Bungeni tukiwa katika hali ya amani na utulivu hata kama kunatokea malumbano

humu, lakini sisi akili zetu zote tunajua kwamba wao wapo, hatutawahi kushikana mashati tukapingana kwa kuwa tunawategemea wao. Nawashukuru sana na wao ninawapongeza sana kwa utulivu wao na wanafanya kazi zao kwa uadilifu kwa kutulinda sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nachukua tena fursa hii kuwaombea sana hawa Askari wetu, jamani Askari wetu kama Askari ni waadilifu, wana heshima, hawawezi kuasi katika nchi yetu ili sisi tukae salama. Je, atawatetea nani kama hatukusimama sisi kuwatetea. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuliokuwemo humu, jamani kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini pia tuwatetee na wao katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii tena kumwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali Kuu niwatetee Askari Polisi waliomaliza kuanzia mwaka 1999 mpaka 2006. Askari wakimaliza mafunzo huwa wanapewa fedha za kuanzia maisha. Askari waliomaliza mafunzo mwaka huo 1999 mpaka 2006 baadhi yao mpaka leo hawajalipwa fedha hizo za kuanzia maisha hasa waliokuwa Kisiwani Pemba. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali Kuu iwaangalie Askari hawa ili wasivunjike moyo, waendeleo kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaunga mkono hoja iwapo haya yote nitakayoyazungumza leo yatapata majibu mazuri na kutekelezwa na ahadi zilizokuwa za kweli.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme Askari wanachangia Mfuko wa Uji. Askari wanachangia Mfuko huu wa Maafa ya Kifo, wanachanga wenyewe kila mwezi.

Nauliza, Taasisi husika inayoshughulikia fedha hizi: Je, ni kwa nini Askari anapofikwa na maafa au akipatwa na msiba fedha hizi zinachelewa wakati fedha ile imetoka kwenye mshahara wake? Naomba hili lifuatiliwe haraka maadam fedha zao zipo, wamezichangia wenyewe, wanapopatwa na misiba fedha hizi zitoke haraka. Lakini ninaiuliza Wizara kwamba kwa kuwa Askari wanaofanya kazi, shambani kwao ni kazini kwao, hawana kazi nyingine kwa sababu kutwa wapo wanalinda nchi yetu: Je, ni kwa nini Wizara nayo haiwaonei huruma ikawafikiria suala hili pindi Askari akipata maafa nayo Wizara ikamchangia? Mbona kuna sehemu nyingine wanachangiwa Wizarani hata sisi Wabunge tukipata misiba ya kufiwa na wazazi wetu na watoto wetu tunapata mchango. Kwa nini Askari nao wajichangie wenyewe? Kwa nini Wizara isiwachangie? Naomba hili liangaliwe sana na mimi nitaunga mkono pindi nikipata jibu zuri, na Askari nao wachangiwe.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Koani lililopo Unguja, nina Kambi ya Machuwi, kuna Kambi nzuri Maaskari wanafanya kazi vizuri, lakini kutokana na ukosefu wa maji katika kijiji Maaskari wamejengewa nyumba, miundombinu ya umeme ipo, lakini maji hakuna. Askari wanapoteza muda mwingi kuhangika na baiskeli na kupoteza muda mrefu wa kufanya kazi kwenda kutafuta maji ya vidimbwi. Namwomba Waziri tutakapomaliza kikao cha Bunge la Bajeti aje akatembelee katika Kambi ya Machuwi angalau awachimbie kisima ili Kambi ya Machuwi Askari waondokane na usumbufu wa kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee upande wa ajira za Polisi. Mheshimiwa Waziri zinapotokea ajira za Polisi, wote tunakuwa hatuna habari, tunashtukia tu Polisi

wanatoka kwenye mafunzo na wengine wanakuwa wanaanza mafunzo. Naiomba Wizara, pindi inapotokea ajira, zitangazwe hizi ajira za Polisi, Magereza, Zimamoto zote tunazisubiri na sisi wenye Majimbo wananchi wetu wanafikiria sisi nafasi zile tunazijua na tunaweza kuwasaidia. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, hizi ajira zikiwa tayari, mtoe matangazo kwenye magazeti, kwenye redio angalau hata kama sikusikia mimi, lakini akisikia mwenzangu, tayari nitaamini hizi nafasi zimetangazwa kweli.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hii nitakaposikia majibu mazuri juu ya haya yote niliyoyazungumza. Jamani Askari wetu wanaishi katika mazingira magumu, wanaishi kwenye nyumba za kazini, wanaridhika, hawafikirii mambo mengine; lakini pia kutokana na kipato chao kidogo, wanakuwa hawana uwezo wa kujenga nyumba. Naiomba Jeshi la Polisi lichukue hatua ya kuwakopesha angalau vifaa vya ujenzi. Wakikopeshwa mabati na saruji, watatafuta viwanja vyao wenyewe ili waweze kujenga nyumba watakapostaafu wasipate aibu zile fedha zao za kiinua mgongo wakaanza kujengea nyumba, wakashindwa kuendelea na maisha na waweze kutafuta utaratibu mwingine wa kujiendeleza na maisha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi niongelee ulinzi shirikishi. Ulinzi shirikishi jamani tumeuamua wenyewe na tumeutaka wenyewe. Kwa kweli tumewatafuta walinzi wetu shirikishi, wanatusaidia sana katika kazi zetu kuwafichua wahalifu na kazi nyingine. Nawaombea hawa wanaofanya kazi za ulinzi shirikishi wasaidiwe angalau wapatiwe semina za mara kwa mara ili kujua kazi zao na mipaka ya kazi zao. Kwa sababu walinzi shirikishi wengine wanatoka wanakwenda mpaka

ndani ya nyumba ya mtu, nyumba ya mjane kaingia mwanamume, wameingia, kwa nini umeingia ndani ya nyumba hii? Lakini wale wamekubaliana! Naomba walinzi wetu shirikishi waelimishwe ili wajue mipaka ya kazi zao. Lakini pia wapatiwe vitendea kazi kwa sababu kazi zao sana wanazifanya usiku. Naomba wapatiwe kama viatu angalau wasaidiwe. Lakini pia wasaidiwe kulipwa posho ya kununulia sabuni, kwa sababu wanaacha usingizi wao pia wakati sisi tumelala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja pindi nikipata majibu mazuri. Ahsante sana. Nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zaynabu Vullu kwa mchana huu atakuwa mchangiaji wa mwisho.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami niungane na wenzangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. La pili, kwa kuwatakia Waislam wote Ramadhani njema ambayo inakaribia hivi karibuni. Lingine ni kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Lakini kama kawaida, wanasema unaposifia ni lazima kukosoa, kuna raha zake vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni Jeshi ambalo linafanya kazi katika mazingira magumu sana pamoja na yote wanayoyafanya. Lakini mazingira wanayofanyia kazi ni magumu sana. Ni wajibu wetu kuangalia ni vipengele gani ambavyo tunaweza tukawasaidia ili waweze kufanya kazi zao kwa uadilifu. Jeshi la Polisi ndiyo mlinzi wa raia wa Tanzania hii na ndiyo mlinzi wa mipaka Tanzania hii. Lakini kama hawana vitendea kazi vya kutosha, kama hawana

fedha za kutosha kuweza kufanyia kazi, kwa kweli hilo linakuwa ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza kwenye ulinzi shirikishi, ulinzi shirikishi unaisaidia nchi hii vizuri sana. Lakini ombi langu, waongezewe mafunzo ya kutosha na ikibidi hata sisi Wabunge tupewe elimu nini wajibu wa ulinzi shirikishi ili tukitoka hapa tukaone ni vipi wanafanya kazi zao. Mlinzi shirikishi hana posho na hana mshahara. Je, tunataka mpaka apige mtu ndiyo amlipe fedha au anapokwenda kumkamata amhonge fedha? Turuhusu rushwa iingie! Naomba sana hilo suala tuwe tunaliangalia na kuliwekea mkakati ni vipi tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Mkoa wangu wa Pwani. La kwanza, namwomba Mheshimiwa Waziri mara baada ya bajeti hii, naomba afanye ziara kwenye Mkoa wa Pwani aone Askari wake walivyo katika mazingira magumu sana. Yeye mwenyewe hawezi kufika kwenye Makao ya Wizara yake kama hajapita Mkoa wa Pwani, lakini Askari wale wanafanya kazi katika mazingira magumu ajabu. Pamoja na kwamba wamepewa kamera za kutosha, sasa hivi tunashukuru kidogo ajali zimepungua, wameweza kuwazuia madereva kwenda mwendo wa kasi, vitochi vimezidi, vimeingia mpaka Mkuranga, vimeingia Rufiji, lakini haitoshi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda leo kwenye Makao Makuu ya Polisi ya Mkoa wa Pwani, ni aibu! Kwanza, jengo siyo lao; pili, choo hawana; tatu, Maaskari hata nyumba za kuishi hawana. Hivi leo itokea dharura Mkoa wa Pwani Polisi anapatikana vipi usiku akafanye kazi? Je, Mkuu wa Polisi wa Mkoa ndio atoke na silaha ile tuliyokumbushwa hapa ya

filimbi aanze kupiga, atanzia Mtaa gani ili aweze kuwatoa Askari hawa waje barabarani waende wakapambane na majambazi, waende wakapambane na uhalifu, waende wakapambane kwenye vita ya wakulima na wafugaji?

Mheshimiwa Spika, tunaomba Askari wa Pwani wapewe Ofisi. Bagamoyo wanapanga kwenye ofisi ya mtu binafsi, akikamatwa huyo! Kisarawe ukienda kuangalia ni aibu! Ofisi ya Askari haieleweki, hiyo mahabusu ndiyo hatari kabisa! Ukienda Mkuranga naona hata aibu kusema, hata kiosiki cha *ice-cream* kina nafuu. Rufiji wamehifadhiwa kwenye jengo la Halmashauri ya Wilaya ambalo lipo kwenye hifadhi ya barabara. Kesho, kesho kutwa linabomolewa! Askari wetu tumeazimwa, mawasiliano ni shida. Naomba Wizara ifanye kila inachoweza iwape angalau fedha za kununua vocha za simu ili waweze kuzitumia katika kupiga simu kupeana na taarifa. Tunaona jinsi gani magari barabarani yanavyokwenda mbio, tunajua sote Mkoa wa Pwani jinsi gani ulivyo mkubwa, sasa leo hizo *radio call* zao nyingine hazina uwezo na hazifanyi kazi, hayo magari mimi sitaki kusema mwenyewe Mheshimiwa Waziri anajua.

Mheshimiwa Spika, Waziri hayo yote anayajua. Sasa ninachotaka mimi aniambie Idara ya Polisi ya Mkoa wa Pwani inasaidiwaje? Idara ya Polisi ya Mkoa wa Pwani inapataje majengo? Inasikitisha sana, wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanasimama barabarani masaa yote wapangiwe utaratibu utakaoweza kuwasaidia. Magereza hazifai, Mkoa mzima una Magereza tatu. Hivi leo atolewe mtu kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine aende akapelekwe kwenye gereza, na hilo Gereza humo ndani likoje? Watoto, wanawake, watu wazima wote

wanalundikana humo humo ndani. Haipendezi! Kama tunathamini utu wa mtu na kama tunathamini haki za binadamu, naomba masuala haya Mheshimiwa Waziri unipatie majibu ni jinsi gani unaweza kuyatatua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, masuala ya bodaboda Mkoa wa Pwani umejitahidi, lakini naomba waongeze bidii kwenye Wilaya nyingine watoe semina, watoe elimu ya kutosha ili kuepukana na bodaboda kupakia watu mishikaki ili kuweza kupunguza ajali za barabarani. Tumeshuhudia watoto wetu, ndugu zetu, jamani zetu wengi wakikatwa sehemu ya viungo vyao kutokana na ajali za pikipiki zinazotokea huko kwenye maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kulielezea ni suala la uhalifu, umezidi! Wanawake wananyanyaswa sana. Pamoja na kwamba naipongeza Serikali kuanzisha *desk* la jinsia, lakini tujiulize: Hili *desk* la jinsia limewekwa, mbona kesi za ubakaji, unyanyasaji, udhalilishaji wa wanawake zimekuwa nyingi katika vyombo vyetu vya habari kila kunapokucha? Tatizo ni nini? Naomba hili suala liangaliwe. Tumeshuhudia kesi nyingi, watu wananyang'anywa watoto, watu wakatwa viungo, watu wanabakwa na watu wanauawa. Tatizo ni nini na Jeshi tunalo? Tuwape nyenzo, tuwape zana wafanye kazi, labda hongo zinachangia, ushawishi wa kupewa hongo nao ni mbaya. Mtu akipewa Sh. 20,000/= ataandika kweli *notification!* Wewe ukilipa atatia mfukoni ili apate hela ya kupigia simu, atatia mfukoni ili aruhusu suala la unyanyasaji liendelee. Ni vizuri Wizara ikaangalia yale maeneo ambayo wanaweza wakayadhibiti, wakayaweka sawa yakafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine naomba Jeshi la Polisi lisaidie hawa wananchi. Tunapozungumzia Watanzania kule kwenye Mkoa wangu, tuna wakulima na wafugaji. Sasa wafugaji wanakaa kila baada ya miezi miwili, mitatu wanahama, watoto wao wanasoma vipi? Askari hawa wenye *Desk* la Jinsia kama wataweza wapite kwenye maeneo ya wafugaji wachukuliwe wale watoto wasomeshwe? Badala yake watakuwa hawana elimu, hawawezi kufika popote! Naomba sana *Desk* la Jinsia, Idara ya Polisi ilianganalie suala hili na kuweza kuona wanasaidia vipi wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Lakini kuunga mkono hoja kutakuja pale nitakapojibiwa Mkoa wa Pwani unaendeshwa vipi? (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. TUNDU A.M.LISSU: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Haya Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu kanuni 68 (7) juu ya jambo ambalo limetokea kwenye Bunge hili mapema.

Mheshimiwa Spika, umetoa maelekezo kwamba hili suala la Hotuba ya Kambi ya Upinzani likazungumziwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba unisaidie kwa mwongozo wako, kama Kamati inayohusika siyo Kamati ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo ndiyo inashughulikia masuala yote yanayohusu migogoro ya *interpretation* za Kanuni zetu. Kwa sababu Kamati ya Maadili inashughulikia masuala mengine, lakini Kamati muhimu ambayo nafikiri inapaswa kulizungumzia suala hili la Kanuni na matumizi yake ingekuwa ni Kamati ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Huo mwongozo umekaa vizuri. Tumekuwa tukijadiliana hapa kwamba kwa nini tusiitumie Kamati ya Kanuni, lakini tukasema tatizo siyo kanuni, kanuni ile ya 64 (c) imekaa wazi kabisa siyo tatizo. Tatizo ni hii *chapter* ambayo tumeisema kuahirishwa kusomwa hivi vilivyotajwa humu vipo Mahakamani, ni hilo tu basi. Kama havipo Mahakamani tutakuja kuruhusu. Tumejaribu kuijadili hii tukasema tukipeleka kwenye Kamati ya Kanuni, ukweli ni kwamba tatizo siyo tafsiri ya kanuni. Kamati ya 64 (c) imekaa vizuri. Tatizo ni kwamba hiki mlichotaka kusoma kipo Mahakamani, kama kipo tutakuja kusema hapana. Kama hakiko Mahakamani, mtakuja kusoma tena ndilo hilo tu.

Kwa hiyo, natangaza kwamba Kamati ya Maadili itakutana saa 7.00 mchana. Nimekwishaagiza wanaohusika watupe ushahidi kwamba zipo Mahakamani na watakutana chumba Na. 219. Naomba mkutane ili kusudi tupate ufumbuzi, basi tutawaruhusu jioni waendeleo na shughuli yao. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wakati Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii anatoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kulitokea mjadala au ubishani kuhusu *chapter* yao ya kwanza na maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba yale yaliyotajwa yalikuweco Mahakamani au vipi.

Bahati nzuri kwa maelekezo yetu, tulielekeza kwamba tuiache ile *chapter* kwanza ili tujitosheleze ama tuthibitishe kama yale yaliyokuwa yanatajwa yako Mahakamani ama sivyo. Kwa hiyo, tuliagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge iweze kuangalia yale matamshi yaliyokuwepo kwenye *chapter* ile kama yanaruhusiwa ama hayaruhusiwi kwa mujibu wa kanuni zetu. Kwa hiyo, Kamati hiyo imekaa mchana saa 7.00 na haya ndiyo maelezo yake ambayo Kamati imeweza kupata. Siku nyingine ilitakiwa Mwenyekiti asome, siyo mimi nafikiri, maana yake nitajitaja mwenyewe.

Anyway, wamesema kwamba, kufuatia agizo langu kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kukutana leo saa 7.00 mchana ili kuweza kuchambua sehemu ya Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hususan katika ukurasa wa tatu mpaka wa sita wa hotuba hiyo kwa mujibu wa nakala ya Mezani, sehemu yenye kichwa cha habari kinachosomeka "Mauaji yenye Sura ya Kisiasa", Kamati ilikutana na kutekeleza agizo hili.

Wafuatao walialikwa kwa majadiliano ili Kamati ifikie uamuzi ambao ni wa haki ni Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Tundu Antipas Mughwai Lissu - Mnadhimu Mkuu wa Upinzani na Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere - Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hawa walialikwa na Kamati. Wajumbe wa Kamati wenyewe wapo.

Kama ilivyo kawaida ya utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilifanya kikao hiki na kurekodiwa katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kwa kumbukumbu na rejea.

Katika uchambuzi, Wajumbe wa Kamati walikubaliana kushughulikia hoja (*issue*) kuu moja kwa mujibu wa maelekezo ya Kiti, kwamba, "Iwapo maelezo yanayojitokeza katika sehemu ya taarifa inayozungumziwa yanaweza kuruhusiwa, kwa kuzingatia kuwa inasemekana taarifa hizo zinahusisha masuala yaliyoko mbele ya Mahakama." Hiyo ndiyo ilikuwa hoja.

Msingi wa hoja hii unatokana na matakwa ya Kanuni ya 64 (1) (c) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayokataza kuzungumzia jambo ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama. Kwa msingi huo, Kamati ilitaka kujiridhisha kikamilifu iwapo masuala yanayozungumzwa katika sehemu ya hotuba hiyo yako Mahakamani au kama hayako Mahakamani. Kwa kuzingatia hilo, Kamati iliwahoji watu wote walioalikwa mbele ya Kamati na kuchambua maelezo yao na Wajumbe wa Kamati wakakubaliana kimsingi kama ifuatavyo:-

- Kwanza, suala linalohusu tukio la mauaji ya Kada wa CHADEMA, Mbwana Masudi yaliyotokea wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge wa Jimbo la Igunga Haliko Mahakamani kwa sababu suala hilo bado liko chini ya upelelezi na hakuna mtuhumiwa aliyekamatwa hadi sasa;
- Pili, suala linalohusu tukio la kuuawa aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Kata ya *Usa River*, Msafiri Mbwambo liko Mahakamani ambapo washtakiwa sita wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani, *Criminal Case No. 184/2012*, Mahakama ya Hakim Mkazi, Arusha;
- Tatu, suala la tukio la kujeruhiwa Waheshimiwa Wabunge Highness Kiwia na Salvatory Machelili, liko Mahakamani ambapo washtakiwa 12 wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani, *Criminal Case No. 84/2012*;
- Nne, suala la tukio la kuvamiwa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, liko Mahakamani ambapo mshtakiwa mmoja alikamatwa na kufikishwa Mahakamani, *Criminal Case No. 100/2012*;
- Tano, suala la kutekwa na jaribio la kumuua Dkt. Stephen Ulimboka, liko Mahakamani ambapo mshtakiwa mmoja amekamatwa na kufikishwa Mahakamani, PI. No. 5/2012; na
- Sita, suala linalohusu tukio la kuuawa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Kata ya Ndago,

Singida, liko Mahakamani ambapo watuhumiwa 18 walikamatwa na kuhojiwa, kati ya hao, sita wamefikishwa Mahakamani, Pl. No. 1/2012.

Kwa madhumuni ya kuthibitisha suala hili, Wajumbe walimtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali awasilishe hati za mashtaka (*charge sheets*) alizozitaja kwa madhumuni ya kuweka kumbukumbu vizuri. Kamati imepokea hati hizo na zimeambatishwa pamoja na taarifa hii kwa rejea.

Hawa wanahitimisha kwamba, kwa wao sasa, sio mimi hapa. Kwa kuzingatia majadiliano ambayo Kamati ilifanya na waalikwa waliofika mbele ya Kamati na kwa kuzingatia ushahidi uliowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati inashauri kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 64 (1) (c) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, suala la kwanza liruhusiwe kuzungumzwa katika hotuba hiyo kwa sababu haliko Mahakamani, isipokuwa suala la pili, suala la tatu, suala la nne, suala la tano na suala la sita yasiruhusiwe kuzungumzwa katika hotuba hiyo kwa sababu ni kinyume na kanuni hiyo. Kwa hiyo, amewasilisha na kwa misingi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema asubuhi, kanuni zetu hazikuwekwa kwa sababu ya kuwekwa, ziliwekwa kwa sababu sisi ni kundi kubwa ambalo wananchi wanalisikiliza, wanalifuatilia wanaliangalia. Maneno yetu ni kama chumvi, ukiweka chumvi kidogo inakoleza tu na kuharibu amani tulizonazo. Siyo hivyo tu, sisi ni moja ya mihimili, na kuna mhimili unaofanya kazi yake. Tujenge tabia ya kuheshimu na mihimili mingine. Kwa hiyo, kwa mujibu wa kanuni ile ile *chapter* yote ambayo ilikuwa inasomwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani tunaifunga hatutaizungumza. Kwa hiyo, haya ndiyo maamuzi ya Spika na bahati nzuri yamekuwa *recorded*.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na wachangiaji wengine. Bahati mbaya asubuhi sikuwataja wanaofuatia, lakini nadhani wao wanajifahamu. Ni Mheshimiwa Ali Omar, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan halafu wengine nitawataja baadaye.

RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Watawallah* kwa kutujaalia sisi Wabunge wa Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwepo hapa katika wakati huu muhimu kabisa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili, natoa shukrani kubwa za dharti kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika bajeti iliyo katika meza yetu sasa hivi, bajeti ambayo ni ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mimi nataka niende moja kwa moja katika kuchangia bajeti hii kupitia katika Jeshi la Polisi katika sehemu ya mishahara au stahili zao. Mishahara ya Jeshi la Polisi bado ni midogo mno, kwa kweli mishahara hii haiwezi kukidhi mahitaji hasa ukilinganisha na mlipuko wa bei za bidhaa na wakati tulionao sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Jeshi la Polisi ukiangalia katika sehemu ya stahili zao posho za Jeshi la Polisi wanapata Sh. 100,000/= ingawa katika taarifa za Mheshimiwa Waziri alizowasilisha leo hii zinasema kuwa kuna ongezeko la Sh. 50,000/= na idadi yake kuwa ni Sh. 150,000/=. Lakini ukilinganisha na wakati tulionao, hii haitoshi kabisa kwa Jeshi hili la Polisi ambalo lina kazi ngumu sana,

ukilinganisha na kazi zote zinafanywa na Wizara nyingine zilizomo katika nchi yetu hii. Ulinzi ni kazi moja ambayo ni muhimu kabisa. Kazi ya ulinzi huwezi kuifananisha na shughuli yoyote katika nyanja zote za maisha na shughuli zetu tulizonazo za kila siku.

Mheshimiwa Spika, kinachonisikitisha ni kwamba posho wanayoipata Askari Polisi ukilinganisha na posho wanayoipata Askari wa Jeshi la Ulinzi wa Tanzania ambayo kiwango chake ni Sh. 225,000/= inaonesha dhahiri kwa vile shughuli zao ni moja, ni kuwanyanyasa au kuwadhalilisha kwa kiasi fulani. Kwa upande wangu kama walivyotangulia wenzangu kuzungumza, stahili za Jeshi la Polisi naomba niishauri Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, ifanye marekebisho angalau iweze kufikia kiwango kile wanachokipata Wanajeshi wetu wa Ulinzi, japo hata hicho hakikidhi, lakini ionekane usawa wa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo naelekea katika Jeshi hilo la Polisi kwa upande wa stahili nyingine zile zinazohusu safari mbalimbali katika maeneo ya kazi, zinaonyesha dhahiri kwamba Serikali haikidhi haja ya kuwapatia kwa wakati unaostahiki, inakuwa upande wao ni usumbufu ulio mkubwa, jambo ambalo linawafanya washindwe kufanya kazi zao kikamilifu na zinavyohitajika. Kwa upande wangu mimi natoa angalizo kama walivyotangulia wenzangu, tusimamie Jeshi letu kuwapatia stahili zao kwa wakati ili waweze kukidhi haja ya shughuli zao ambazo ni ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naelekea katika upande wa huduma ya makaazi ya Polisi. Jeshi la Polisi miongoni mwao wengi wanaishi katika maeneo ya raia, nyumba za

kupanga jambo ambalo hii ni sehemu moja kubwa inayowadhalilisha na kuwafanya wasiweze kumudu kazi zao kiurahisi kama inavyotakikana. Naomba kwa utaratibu huu uliopo sasa, Jeshi la Polisi liangaliwe kwa hali ya juu kabisa ili wapatiwe makazi ambayo yatawafanya yalingane na mazingira yao ya kikazi.

Mheshimiwa Spika, tukiacha hapo, twende katika Jeshi letu la Magereza. Msongamano katika jela zetu ni mkubwa mno. Hii ni hatari! Ni hatari katika nyanja mbili, sehemu ya kwanza kulundikana kwa idadi kubwa ya mahabusu na wafungwa katika jela zetu, inaweza kuleta matatizo kama yafuatayo:-

Tatizo la kwanza linaloweza kujitokeza ni hatari ya mlipuko wa maradhi. La pili, kuna taarifa zinazojitokeza ambazo ni rasmi, kutokea udhalilishaji kwa wale mahabusu ambao wamo katika mchanganyiko ule wa mahabusu na wafungwa kuwekwa pahali pamoja. Naomba nitoe ushauri kwamba Serikali kwa njia yoyote utanuzi huu wa maeneo ya wafungwa ufuatiliwe, baadaye wafungwa hawa na mahabusu wawe wanakaa katika maeneo tofauti jambo ambalo wale mahabusu ambao ni watoto wanaweza wakadhalilishwa kijinsia na mara nyingi hayo yanaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuhusu Jeshi letu la Polisi, naomba Jeshi la Polisi libadilishe kidogo mtazamo wake ule ambao ni wa kizamani wa kusimamia haki ya upande mmoja tu, na upande mwingine ukabaki vilevile.

Hii nakusudia kusema, wanapotekeleza kazi zao wafahamu kama sasa hivi tunavyokwenda wasifuate ile kusikia kama Serikali zilizopo ni Serikali za Chama cha Mapinduzi peke yake, ikawa wanaelekea upande huo tu, au kufanya matakwa ya kuelekea upande mwingine kwa mujibu wa maslahi yao. Mimi nawashauri, kazi zao ni nzuri, na ni waaminifu, lakini tu wajitahidi sana pale ambapo inawezekana au haiwezekani, hii ni haki ya kila upande. Kwa sababu huu ni Mfumo wa Vyama Vingvi vya Kisiasa wafanye kazi zao kwa mujibu wa kutoa haki, wasiegemeo upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumaliza, naomba nitoe ushauri wangu kidogo ili uweze kufuatwa na kutekelezwa. Serikali isimamie shughuli zote zinazostahiki kwa Jeshi hili la Polisi ili waweze kufanikisha kazi zao, mpango unaotakikana. Nakusudia kusema hivi wafuatiliwe mambo yao yote yanayohusu stahili zao na watekelezewe haki zao bila ya kunyimwa na wapate stahili kwa wakati unaofaa bila kucheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, lingine kabla ya kumaliza, nataka nizungumzie kuhusu wastaafu wa Jeshi hili.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. MBAROUK SALIM ALLY: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii Mambo ya Ndani. Kwanza nianze kwa kusema kwamba, siungi mkono hotuba hii kwa sababu imeshakuwa ya

kawaida. Kuna mambo mengi ambayo tuliyapigia kelele sana mwaka jana tukaahidiwa, lakini hakuna kilichofanyika na sitaunga mkono kama Waziri atakapokuja kujumuisha hatonipa maelezo ya kuridhisha ya askari ambao waliwahi kuhamishwa kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara kuanzia mwaka 2009 mpaka 2011 na mpaka hii leo hawajapa stahili zao za uhamisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sielewi kuna matatizo gani au kuna tofauti gani baina ya sekta nyingine ya ulinzi na Jeshi la Polisi kwa sababu hiki kinachofanyika kinaonekana dhahiri ni uonevu. Sehemu nyingine za ulinzi wanapopata uhamisho, wanapata stahili zao bila tatizo lolote. Lakini ukija kwenye Jeshi la Polisi kwa kweli linakuwa ni tatizo na hili limekuwa ni kero. Sasa nitamtaka Waziri atakapokuja kwa kweli, hili anipe majibu na anieleze iniridhishe ndiyo nitaweza kuunga mkono bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, sasa matatizo ya Askari Polisi yameelezwa na wenzangu wengi, lakini naomba niende moja kwa moja kwenye maeneo yangu ya Kisiwa cha Pemba. Pemba ni Kisiwa, lakini ni sehemu moja ambayo inapata ziara nyingi za viongozi wa Kitaifa na kama inavyoeleweka kwamba kila ziara basi Jeshi la Polisi ni lazima washiriki katika misafara. Tatizo ya mgao au *allocation* ya mafuta wanayopatiwa Jeshi la Polisi, Pemba kwa kweli ni kidogo mno. Mahitaji yanaweza yakafikia shilingi milioni 80 kwa mwezi, lakini pesa wanazopewa basi aidha ni shilingi milioni tano, kumi au kumi na tano na bajeti hii inaonesha kwamba watapatiwa mgao wa milioni kumi na nne wa mafuta. Ukienda katika vituo vya mafuta, hilo ni deni tu. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine, wananchi wa Pemba tunapata usumbufu sana kufuata huduma za Polisi. Hii ni kutokana na ukuaji mkubwa wa maeneo, lakini vituo vyetu vilevile vya asili ambavyo vilikuwepo na ndiyo hivyo hivyo ambavyo tunaendelea kuvitumia.

Sasa namwomba Waziri aliangalie sana ili tuweze kupatiwa *Police Post* katika maeneo mbalimbali kwenye Kisiwa cha Pemba. Kwa sasa kuna kituo kimoja tu ambacho kipo Mkanyageni. Kwa kweli kuna maeneo mengine mengi ambayo kuna kesi nyingi za uhalifu, lakini kupata huduma za Polisi kwa kweli inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, tunaomba kwa hili Waziri pia alitupie macho ili aweze kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuliongelea ni majumba mabovu. Tunashukuru kwamba, Wizara mwaka juzi na mwaka jana walikamilisha ujenzi wa nyumba moja ambayo iko Limbani kwa askari ambao wako Wete. Lakini kuna majengo ambayo yako Konde, Micheweni na kuna majengo mengine ambayo yako Kisiwa cha Pemba, ni mabovu vibaya, yanavuja na kuta zimeanza ku-*crack*. Kwa kweli huwezi kudhania kwamba wanakaa askari wetu ambao tunategemea kwamba watulinde. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu kwamba Bajeti hii pia itaangalia kukarabati baadhi ya majengo ili askari wetu waweze kupata maeneo mazuri ya kukaa.

Mheshimiwa Spika, ambalo napenda nilichangie ni Kituo cha Polisi kilichoko Matangatuani. Nafikiri sisi tuna matatizo ya ardhi kile ni kisiwa. Kile kituo kinavyoonekana Polisi wenyewe wameshakiachia, lakini hawajataka kukiachia moja kwa moja. Kilichobaki ni ung'ang'anizi wa

kile kituo. Sasa nashauri kwamba, kwa sababu karibu na kituo kile kuna kituo cha utafiti wa kilimo. Yote ni matumizi ya Serikali, kwa hiyo, nashauri kwamba kituo kile basi tukibadilishe matumizi.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya kuweka askari mmoja mmoja pale kutoka Finya akaja akakaa pale asubuhi, nahisi ni usumbufu. Wakati Konde kuna Kituo cha Polisi, karibu tu, hata kilometa moja na nusu sidhani kama inafika, sioni sababu ya kituo kile kibakie kuwa Kituo cha Polisi. Sasa nashauri kituo kile kwa sasa kibadilishwe matumizi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo lipo ni tatizo la ajira. Tatizo la ajira limeshakuwa sugu. Ajira za Polisi na uhamiaji ni kitendawili kwa sababu inaonekana kama ni siri kubwa. Inaonekana kwamba mchakato wote wa ajira unafanyika na wakubwa wa Polisi. Inaonekana hata ule Mkoa kwa mfano, wa Kaskazini Pemba basi hawaelewi. Yaani wanapelekewa majina ya wanaotaka kuajiriwa ikiwa tayari wameshafanyiwa *interview*, kila kitu wameshamaliza. Kwa hiyo, nahisi kwamba tatizo la ajira pia nalo lina matatizo haliko wazi na linahitaji kwa kweli kufuatiliwa ili kuwekwa wazi ili raia wote wajue kwamba kuna ajira hizi ili aliye na sifa aweze kuomba na aweze kuzipata hizo nafasi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kituo cha Uhamiaji kilichopo Bandarini Wete. Kuna kibanda hakieleweki kwamba ni ofisi au ni choo. Lakini kwa kweli kuna kibanda pale bandarini kidogo sana hakieleweki anayekitumia ni nani? Humo humo utakuta askari polisi, humo humo utakuta uhamiaji au wavuvi, humo humo utakuta wasafiri. Kwa hiyo kwa kweli haieleweki. Sasa hilo ni tatizo. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Waziri tunamwomba kwenye bajeti yake hii basi afikirie ujenzi wa ofisi au upatikanaji wa ofisi ya Maafisa Uhamiaji pale bandarini Wete.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa sababu matatizo ni mengi, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, labda ikimalizika bajeti hii basi afanye ziara Pemba, pengine kwa kuungana na Wabunge ili ashuhudie matatizo mengi ambayo yapo Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uwezo wa kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu nami kuchangia machache katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani, lakini pili nikushukuru wewe kwa muda ulionipa ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba Mkoa wa Kaskazini Pemba au Pemba yote basi Jeshi la Polisi linanuka madeni na hili ni kwamba, hawalipi kipaumbele kutokana na mambo muhimu kwa mfano ziara za viongozi, Mheshimiwa Mbarouk ameisemea. Mafuta wanaogawiwa ni kidogo sana kulingana na matumizi wanayohitaji. Kwa hiyo tuondoe hii dhana ya Jeshi la Polisi kufikia *stage* ya kuombaomba maana mwisho wake wataomba na wanataka kukidhi haja ya matumizi. Mheshimiwa Waziri angalia sana Jeshi lako lisiwe ombaomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili nyumba za Askari Polisi. Bunge lililopita tulikwenda kutembelea makazi ya Askari Polisi. Kipya siku zote huwekwa na kikongwe na kama huwezi kukitunza kikongwe na ukakidharau kwa sababu umepata kipya hilo ni tatizo. Tusije tukatumia ule msemu kwamba kipya kinyemi. Nyumba za asili za askari kwa mfano *Police line* Wete ni nyumba muhimu sana, nzuri madhubuti lakini zimekufa na tunaendelea kuziua kwa sababu tumeziacha *total*. Si Wete tu, Konde na nadhani na Wilaya nyingine zote ziko katika hali hiyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri aziangalie zile nyumba tuweze kuzitunza ziweze kuwasaidia askari wetu.

Mheshimiwa Spika, nina taarifa ambazo sina uhakika, lakini naomba niiseme na Mheshimiwa Waziri aichukulie hatua aiangalie kwa umakini. Kamishna wa Uhamiaji pale Zanzibar nasikia ana matatizo na mwaka jana paliundwa Tume na matokeo ya Tume yalipotoka kuna taarifa kwamba, vijana waliotoa taarifa kuhusiana na hali hiyo wamepewa uhamisho. Naomba ufuatilie kwa umakini, kama kuna tatizo lolote basi Bunge lako Tukufu liweze kupata taarifa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Madawa ya Kulevya. Madawa ya Kulevya ni tatizo kubwa sana na ni tishio. Madawa ya kulevya yanaendelea kuingia nchini. Madawa ya kulevya yanapita bandarini, yanapita kwenye viwanja vya ndege, maeneo ambayo tuna ulinzi wa kutosha, tuna usalama wa kutosha, inakuwaje madawa yanaingia kwa nguvu kubwa nchini mwetu. Kuna Kitengo ambacho kinashughulika na madawa ya kulevya, kimeshindwa? Je, tumeshindwa kuwaandalia vijana wetu wa Jeshi la Polisi na Usalama, vifaa vya kisasa wakaweza

kugundua haya madawa ya kulevya jinsi yanavyoingia nchini.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaathirika, Serikali inaathirika mwisho wa siku tumeamua kuandaa nyumba za kuwaweka waathirika wa madawa ya kulevya kule Zanzibar tunaita *Sober House*. Ni tatizo, Serikali inakula hasara, vijana wale wanataka kuhudumiwa, wanataka kulishwa, wanataka madawa. Lakini si hilo tu pale tunapowaweka kuna wanawake na wanaume. Tatizo tunalirudisha palepale, UKIMWI utarudi palepale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale vijana akili zao si barabara hawajui wanachokifanya. Kwa hiyo, ni hatari tuangalie sana, tusikimbilie kutibu tukimbilie zaidi kuingia. Bado tuna tatizo. Wazungu wanasema *prevention is better than cure*. Sisi tatizo hili linatuathiri sana, vijana wanaathirika sana. Naomba niseme kwa ufupi kwa sababu muda haunitoshi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niligusia ni mahabusu. Kule magerezani kuna matatizo. Hatupendelei sana kuongeza Magereza kwa sababu watu wetu wafanye makosa, lakini lazima tuongeze. Kwa sababu makosa yanafanyika, magerezani ni kuchafu, magerezani tunavunja haki za binadamu na hii inasababishwa na mlundikano mkubwa wa mahabusu ambao unachangiwa zaidi na Mahakama. Kuna kesi zingine si za kuweka watu mahabusu. Kuna kijana kwa mfano, kaiba kuku unamkuta mahabusu, kijana kaiba nazi unamkuta mahabusu. Si kesi za kuwalundika watu magerezani. Watu wanalala wanapishana miguu hivi kama jongoo. Ukienda magerezani wewe utalia, wanapishanisha miguu ndiyo waweze kulala.

Mheshimiwa Spika, ni tatizo. Lazima Serikali ihakikishe kwamba tunaondoa tatizo hili. Lakini si hilo tu nina mashaka ule mtindo wa wale mahabusu kujisaidia kwenye ndoo bado nina wasiwasi kwamba unaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunavunja haki za binadamu. Wenyewe kule wanaita mtondoo. Halafu ndoo ile anabebeshwa mmoja anakwenda kumwaga kwa zamu. Ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Afya zao zinaharibika. Ni tatizo lazima tuhakikishe tunajenga vyoo vya kutosha kwenye magereza yetu. Ili wale ambao watapata hatia na kuwekwa kule basi wasiadhibiwe kabla hawajahukumikiwa Sheria hairuhusu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuangalie kwa umakini mkubwa na kwa sababu wanakaa ndani muda mrefu tayari tumewaadhibu. Je, ule muda wao wanaokaa gereza ni wengine wanakaa mahabusu zaidi ya miaka mitatu na hatimaye anakutwa hana hatia inakuwaje, analipwa? Familia yake imeteseka kwa muda mrefu analipwa nini? Analipwa fidia? Lazima Sheria zetu tuziangalie. Kama kuna uwezekano wa kuzirekebisha, tuzirekebisha ili tusivunje haki za binadamu, sisi ni watetezi wakubwa wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo la Askari Polisi vijana ambao wanafanya kazi kwa umakini mkubwa lakini inavyoonekana tutaweza kuwapeleka katika mkondo wa rushwa kwa hivi tunavyokwenda. Kuanzia mwezi Novemba mpaka mwezi wa tano kama sikosei kule Zanzibar kuna vijana wapatao 30 walikosa mishahara miezi yote hii. Ni wafanyakazi wa muda mrefu ilitokezea tu wakakosa mishahara mwezi wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa

tano, hawa walikuwa wanaishije. Je, akitokea mtu keshamkamata akampenyezea chochote si atachukua kwa sababu nyumbani watoto hawana chakula? Tunakaribisha rushwa. Nilivyofuatilia Waziri aliyepita aliniambia kwamba hawa watu hawakupeleka akaunti zao za *NMB*, nikafuatilia sio kweli. Walikuwa na akaunti zao wamepeleka na walishawahi kupokelea mishahara kwenye akaunti imekuwaje wakakatishwa njiani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sio hilo tu baada ya kufuatilia kwa kina wanatoka Zanzibar wanakuja Dar es Salaam wanapoteza nauli ya kuomba au kukopa. Walipofika pale miezi ile sita mpaka leo hawajalipwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini watapewa pesa zao hawa kwa sababu wana madeni. Kama kuna uwezekano basi wapewe na fidia, kwa sababu tumewadhalilishia pamoja na familia zao. Tumewakosesha mambo mengi ya msingi waliyojipangia kufanya katika maisha yao. Lazima tuwe waangalifu sana, hawa askari wana kazi ngumu sana, tunawahitaji ndiyo usalama wa nchi, ndiyo usalama wa raia. Ndiyo usalama wa sisi Wabunge humu ndani na pia Mheshimiwa Waziri usalama wake unawategemea wale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima tuangalie kwa umakini mkubwa. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha leo na kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Pili, naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Tatu, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake safi ingawa kuna matatizo madogo madogo, lakini matatizo kama hayo

hayawezi kuepukika. Muungwana aliyetimia kwanza anashukuru yale yaliyopatikana halafu tena anatoa hoja zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nitakwenda kwenye hoja ya marekebisho ya Jeshi la Polisi juu ya Sheria zao. Kila tukisimama hapa tunaomba Sheria za Polisi zimepitwa na wakati na kila Waziri anayekuja anasema atazirekebisha na ataleta hapa, lakini mpaka leo Sheria zilizopo ni Sheria ambazo zinawakandamiza askari wa chini. Askari wa kawaida ndiyo wanaokandamizwa, lakini vilevile Sheria zile nyingi ni za kikoloni.

Mheshimiwa Spika, Sheria mojawapo, hivi sasa Jeshi la Polisi linafanya kazi utafikiri limekodiwa lina mikataba isiyopungua minne na nina mashaka kuwa Wizara zote au wafanyakazi wote hawana mikataba kama hiyo mkataba wa mwanzo anapoingia ndani ya Jeshi la Polisi, baada ya miaka mitatu wapime mkataba wa tatu ambao unaniuma sana. Akifika miaka 12 anaulizwa je, unataka kiinua mgongo au unataka pensheni, akisema anataka kiinua mgongo basi keshanguka kwa sababu hata akifanya kazi kwa muda wa miaka 30 kama hakuacha katikati analipwa siyo zaidi ya shilingi milioni mbili kwa muda wa miaka 30.

Mheshimiwa Spika kupitia kwako namwomba Waziri kigugumizi hiki kisiweko Askari wa Polisi akishafika miaka 12 anaulizwa mambo mawili kuwa unaendelea, unachukua haki yako au unakwenda penshenia. Mkataba uwe namna hiyo unaendelea au haendelei moja kwa moja aende penshenia. Kwa maisha yetu yalivyo hivi sasa hakuna askari hata mmoja atakayefika miaka 12 akasema nitafikisha miaka 15 halafu aache atafikisha miaka 40 yumo humu

humu na akishafikisha hapati haki, hiyo ni Sheria ya Kikoloni na tunataka iondolewe mara moja kwa sababu askari wengi wanalalamika, nimefanya kazi kwa muda wa miaka 12 nikaacha hapo hapo ndani ya Jeshi la Polisi kiinua mgongo nikachukua na niko huru.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuhusu posho ya chakula. Posho ya chakula iendane na wakati kwa sababu ndugu zetu wanakopa hata wakishapewa posho ya chakula hawana kitu. Kwa hiyo, posho hii ni vizuri ikaenda na wakati yaani wakati ukifika wapewe posho yao na wajue namna ya kuitumia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu magerezani, huu mfumo wa kufanya kazi ndani ya jamii uliopangwa kuanza katika Mikoa mitano au sita uendelezwe, vurugu magerezani ziondoke, wanaofungwa miaka michache wote wafanye kazi ndani ya jamii, itolewe taaluma wananchi wajue kuwa ndugu zetu wana makosa madogo madogo wafanye kazi hizo. Nawaasa Watanzania kazi kubwa ya Polisi ni lazima ahakikishe amani na utulivu nchini vinapatikana. La pili, Polisi wahakikishe mali za wananchi na wananchi wako katika amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, pia kumezuka baadhi ya viongozi kwenda kuhubiri siasa mbaya, siasa za uchochezi, wananchi nawaasa wasiwafuate viongozi hao, wafanye kazi zao, wajue kuwa wakiwafuata Polisi watahakikisha sehemu ile amani ipo na hapo Polisi hatatazama haki za binadamu atahakikisha kuwa mahali pale amani na utulivu unakuwepo na atatumia kila njia ili amani ipatikane.

Mheshimiwa Spika, nimefanya hesabu za haraka haraka hapa nikakuta kama askari 100 wanatoa shilingi 5,000 kila mwezi. Kama kule Zanzibar kuna askari kila mwezi wanatoa shilingi 5,000, kwa hiyo, askari 100 wanatoa shilingi 500,000 na askari 200 watatoa shilingi 1,000,000. Je, kila siku kweli askari wanakufa na kama shilingi 1,000,000 inapatikana nataka kujua inatumikaje? Lakini Jeshi la Polisi ni wajibu wake kuhakikisha kuwa askari kazikwa, kapata vitu vyote na nyumbani kwake kunatazamwa kama kawaida kama vile sisi Wabunge tukifa, nadhani kuna ruzuku fulani inatolewa au ukifiwa kuna ruzuku fulani inatolewa kwa hiyo, shilingi 5000 kwa kila mwezi naona ni ukandamizaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi nasikitika sana, kule Zanzibar utawakuta ndugu zangu Trafiki au Polisi husika wanatumia *vespa* au *Honda* hizi *fifty*. Lakini vijana wote utawaona wana pikipiki kubwa, pikipiki zile zikisimamishwa hata hawajali wanakwenda zao, askari polisi wanabaki wanaadhirika, wanawatazama tu. Sasa wakati umefika lazima tushindane kama wao wana pikipiki kubwa na sisi tuwe nazo.

Mheshimiwa Spika, Polisi anamsimamisha mtu kama mtu huyo hasimami Polisi anasimama tu kumtazama, anazomewa, ni aibu kubwa, sasa wawezesheni vijana wetu waweze kufanya kazi ili wale wanaowatazama Polisi wakati wako kazini mfano watoto wa shule, wawe na moyo wa kuja kuwa mapolisi baadaye. Naomba Polisi wapewe vitendea kazi ili wakiwa kazini wapate raha na starehe, isiwe Polisi yuko kazini anaanza kujjuliza yule anakuja nitamsimamishaje.

Mheshimiwa Spika, Lingine ni kuhusu Sheria zetu za sasa hivi ninatumaini kuwa baadhi ya Sheria hata askari polisi wanazifumbia macho kwa sababu kule Zanzibar ukienda bila taa ndiyo Sheria ukienda na taa unakamatwa Zanzibar wapanda baiskeli wote wanatembea giza bila taa na hata wakikamatwa wanaambiwa *fine* shilingi tano bado ipo Sheria ya shilingi tano lakini wakati huohuo unamlaumu askari polisi kwa nini ile *fine* yake tu akifanya ni zaidi ya shilingi tano kwa hiyo, ninadhani kuwa hizi Sheria ambazo zimepitwa na wakati tuziondoe ili vijana wetu wafanye kazi vizuri na awe na moyo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nadhani sasa hivi tuwe na utamaduni wa kutazama majengo yetu, nyumba zetu zinazovuja zikarabatiwe, tusikimbilie kujenga nyumba mpya tu. Yapo majengo mazuri, lakini yanaachwa, yanaendelea kuvuja kama pale Kituo cha Polisi Fuoni, kuna nyumba chungu nzima, lakini zinavuja na hazitazamwi. Ukienda Mwera halikadhalika, ukienda Makunduchi halikadhalika, utakuta zinatafutwa chungu nzima zijengwe kwa fedha chungu nzima, wakati kama tukikarabati majengo yetu kwa sasa utakuta tutafanikisha na tutatumia fedha kidogo. Kwa hiyo, namshauri Waziri awe na utamaduni wa kuzipitia nyumba kwa maana ya kuzifanyia ukarabati wa haraka ili zifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, natoa pongezi kwa Jeshi la Polisi, lakini pia nazidi kumwambia Inspekta Mwema sifa anazopata.

SPIKA: Haya amesikia.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa namuita Mheshimiwa Faida Bakari atafuatiwa na Mheshimiwa Azzan.

MHE. FAIDA M. BAKARI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali salama. Napenda pia kuishukuru sana Serikali yangu ya Jamhuri Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Daktari Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali ya Zanzibar inayoongozwa na Daktari Shein kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuwaletea wananchi maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Waziri Mheshimiwa Nchimbi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Pereira kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. Nawaambia Daktari Nchimbi na Mheshimiwa Pereira nawaamini, wanaweza kuiweka Wizara hii katika hali ya juu kabisa. Napenda pia kuwapongeza makamanda wote wa Tanzania na Polisi hususani makamanda wa Kisiwa cha Pemba wanavyofanya kazi vizuri. Sasa hivi Pemba imetulia, imenawiri, wanafanya kazi zao usiku na mchana na amani na utulivu umerejea.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchangia katika ajira za Polisi kwa vijana. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa sababu inatoa nafasi hizi kwa sehemu zote za Tanzania na hata Pemba inaleta nafasi hizi, lakini napenda kuuliza labda hawa Mawaziri waliopita wamo humu humu

kila siku tukisimama hapa Bungeni tunatetea sehemu zetu ajira kwa vijana. Mwaka jana nilitetea ajira kwa vijana, ajira za Polisi haziwafikii vijana wa Pemba, vijana wa Pemba ni wazalendo, vijana wa Pemba wamesoma na ni wakakamavu, wana maadili lakini siku ikifika ya kufanyiwa usahili, vijana wa Pemba hawapewi nafasi wanaletwa vijana kutoka sehemu mimi sijui, lakini wanawekwa kama wanatoka Pemba na majina yao eti nakaa Kibirinzi, nakaa Wawi, sijui nakaa wapi, siyo kweli! Vijana wa Kipemba hawapati ajira hizi na kama wanapata wanapata wachache, tunataka vijana wa Pemba wafanye kazi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ajira za Polisi na Jeshi ndiyo ajira ambazo zinatoka kwa wingi, lakini Wizara nyingine tofauti hakuna kuajiri vijana kwa wingi, lakini kama ajira 5000 au 2000 zikiletwa Pemba *Wallah Billah Tallah* wanapata watoto wa Kipemba labda watano. Kama hamnisadiki hawa waliokwishapata miaka iliyopita kawachunguzeni muwaangalie vyeti vyao walivyosoma darasa la kwanza walisoma shule gani za Pemba ile na mwalimu wake wa darasa la kwanza atawaambia ni nani, ndiyo mtapata ushahidi. Wanaletwa watu *from nowhere*, wanaajiriwa kwa majina ya vijana wa Pemba, tumechoka, wanatumiza! Tukiwaona vijana wetu hawapati ajira, wanatumiza. Namwomba sana Mheshimiwa Nchimbi, mara hii naikubali *speech* lakini *Wallah* mwakani siikubali kama itakuwa vijana wa Pemba hawapati ajira, vijana wa Pemba mnanisikia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila anayesimama hapa anasema kuhusu maslahi ya askari. Askari wote ni sawa, hapa wanalinda nchi hii, hakuna ubaguzi kati ya Askari Jeshi na Askari Polisi na askari wengine wowote na Askari Polisi

wanafanya kazi mchana na usiku wanailinda nchi hii na wanatulinda sisi. Bila Askari Polisi hatuwezi kuishi katika dunia hii, lakini kwa nini mnawanyima maslahi yao, posho ya chakula eti 100,000! Je, mtu unaweza kuendesha maisha kwa 100,000? Kama Wabunge hatuwezi na wao hawawezi.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, posho zao za chakula ziongezwe kama wanavyopata askari wengine au zaidi pengine wapate 300,000 baada ya 250,000. Kwa nini wafanyishwe kazi ile kwa sababu hawawezi kusema, kwa sababu hawawezi kuandamana, kwa sababu wao hawawezi kugoma, kwa nini tunawaonea askari. Naomba sana Mheshimiwa Waziri mara nyingine tena sitaikubali hii hotuba.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu ujenzi wa nyumba. Naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, inajitahidi kujenga nyumba za askari, lazima tuseme ukweli jamani. Pesa inayopatikana hiyo hiyo lakini inajenga. Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa naomba aiangalie Wizara hii, naomba afanye kazi Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kukusanya mapato katika nchi hii ili tuweze kuwajengea nyumba askari, Pemba kule watu wanaishi maisha magumu, Mkoani huwa naona huruma.

Mheshimiwa Spika, nikienda Kituo cha Polisi, nikiona zile nyumba, eti zina chumba kimoja, mtu analala na mke wake, watoto na wajukuu, siyo vizuri jamani, ni maadili gani haya? Haiwezekani askari wapatiwe nyumba za kisasa, naomba sana Mheshimiwa Waziri hili alione kwa sababu namjua ni mtendaji wa kazi, namjua na mwakani tukija

hapa tuone mabadiliko na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ananisikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Polisi, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameongelea kituo chetu cha Polisi cha Chake Chake pale ambacho ni cha Mkoa, tunaishukuru sana Serikali, kituo ni kizuri, kina afya, kinang'aa na askari wake ni wazuri kwa maana ni watendaji. Lakini Mheshimiwa amesema kimefikia 100%, nakataa kwa sababu hata shule ukijenga halafu kukawa hakuna madawati, hakuna mbao za kuandikia walimu haitakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara yako iingize vifaa vya kisasa vya kisayansi na teknolojia *computer* na mambo mengine ya kisasa ili askari wetu waweze kufanya kazi vizuri na pale katika jengo lile liwekwe uzio, wajenge ukuta kwa maana jengo lile liko njiani na nyuma kuna nyumba za raia siyo vizuri kwa Kituo cha Polisi kwani kuna mambo ya siri, haiwezekani kila mtu apite hapo anakiona kila kitu wanachofanya polisi. Naomba sana kituo hicho akiangalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile kijengwe tena kituo kingine cha polisi Mkoani. Namshukuru mungu na wenzangu walioko Kaskazini wataniunga mkono, lakini Mkoani hakuna, ni aibu. Mheshimiwa Waziri nakuomba haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu ucheleweshaji wa posho mbalimbali za askari. Kuna posho mbalimbali zinacheleweshwa kama posho za uhamisho, mtu anaweza kuhamishwa leo pesa yake akaja kulipwa mwakani, yule ni binadamu ana watoto, ana mambo mbalimbali ya huduma za kifamilia. Unamhamisha na

kumpeleka mahali hapajui halafu humpi chochote eti unakuja kumpa mwakani, hilo siyo jambo zuri na vile vile fedha hizi ambazo wanapatiwa watu hawa waingiziwe kwenye akaunti zao, lakini kuna wengine wanasainishwa tu baadaye hawapewi chochote, hivi siyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu polisi jamii; kule kwetu katika kituo chetu cha Chakechake ama Pemba Kusini ina polisi jamii ya Wanawake wale ambao nawapenda sana kwa sababu wale wanawake wako *strong* sana, wanapita mashuleni kuelimisha, wanapita kwenye jamii kuelimisha mambo mbalimbali hata ya UKIMWI ya kiaskari na kizalendo, lakini sidhani kama wanatengewa fedha. Kwa sababu wakiwa na *function* zao wanatutafuta sisi ili tuweze kuwasaidia na tunawasaidia sana kwa sababu ni wenzetu, lakini kwa nini wasiwe na bajeti yao? Hawa watu ni muhimu katika jamii na wanasaidia maskini, wanasaidia walemavu, watoto yatima, hiki kikundi kinaongozwa na Kamanda Asha na Kamanda Zuwena nawapongeza sana wanawake wale Maaskari wa Pemba.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee suala la ujambazi. Nashangaa katika nchi yetu hii ya Tanzania na Polisi tulionao wanafanya kazi kwa bidii, lakini ujambazi umezidi. Siku moja Kamati yetu ilisafiri kutoka Kagera kwenda Karagwe, tulivyofika njiani tukaambiwa kuwa sasa shukeni muingie kwenye gari nyingine na Mapolisi na mitutu ya Bunduki. Jamani niliogopa, nikasema mimi niko Tanzania nalindwa, jamani sasa huku ni wapi, nawauliza wenzangu wakaniambia huku ni kwingine lakini ni Tanzania hii hii. Ni aibu Mheshimiwa Waziri amepewa kazi na Mhesahimiwa Rais aifanye, apange jeshi lake vizuri na Mwenyezi Mungu atakusaidia na atatusaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi angalau na mimi nichangie kwenye Wizara hii ya Mambo ya ndani ambayo ni Wizara muhimu sana. Kwanza kabisa leo hii ni karibu miezi saba tangu mafuriko ya kutisha ambayo yamesikitisha nchi yetu yalipotokea pale Dar es Salaam na kusababisha vifo vya watu kadhaa naogopa sana kuwa yale yaliyotokea mwishoni mwa mwaka jana nina hakika yatatokea tena muda siyo mrefu kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, hilo linawezekana kabisa na kwa nchi iliyo makini kama nchi ya Tanzania ninahakika lile ni funzo na tutakuwa tumejiandaa vizuri kukabiliana na hiyo hali pindi itakapotokea, sitarajii yaliyotokea mwezi Desemba ya kukosa vifaa vya kuokoa watu yatatokea tena.

Mheshimiwa Spika, hii ilisababishwa na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, kukosa vifaa vya kuokoa vimeleta athari kubwa sana. Kwa hiyo, naogopa sana kwa sababu kipindi cha mafuriko yale sitaki kuyakumbuka kwa sababu nikiyakumbuka nasikia uchungu sana. Lakini yaliyotokea wakati ule kwa sisi ambao tulikuwepo pale hali ilikuwa inatisha sana. Unapiga simu kuomba msaada kila mahali hakuna anayepokea simu, humpati Kamanda wa Polisi, huwapati watu wa Uokoaji na unaowapata wanakuambia tunangojea kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama cha Mkoa huku watu wanateketea.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mbunge wa Mafia Mheshimiwa Abdulkarim Shah, baada ya kumpigia simu na wote ni mashahidi na baada ya kukosa jinsi ya

kusaidia kuokoa watu ndipo alipoamua kwenda kukodi boti feri na kulileta kuja kuanza kuokoa watu. Tulipata misaada kutoka Jeshi la Wananchi, baada ya kuleta boti za uokoaji na wazamiaji lakini hiyo ilikuwa ni saa tisa za alasiri na mafuriko yalikuwa ni asubuhi, watu wapo juu ya mapaa ya nyumba kuanzia saa mbili asubuhi wanangoja kuokolewa na waokoaji hakuna. Helikopta inapita juu na hakuna helikopta ambayo inaweza kuokoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitarajii kama suala hili litajirudia tena, ni matarajio yangu kwamba Serikali imejifunza, Jeshi limejifunza, tutaanza kununua vifaa vya uokoaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya Uokoaji na Zimamoto, ni hela ndogo sana na ukiangalia magari ambayo yatanunuliwa ya Zimamoto yanayotajwa ni kwa ajili ya *Airport* tu. Dar es Salaam imepanuka sana. Lakini maafa haya siyo lazima iwe moto tu, yanaweza yakawa mafuriko kama ambavyo yalitokea mwezi Disemba. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali katika suala la uokoaji tuache mzaha, tuhakikishe tunapata vifaa, vikae tu kama akiba. Hivi kweli mafuriko yale yanatokea tunashindwa kuwa hata na *fiberboat*, tunashindwa kuwa na hata zile *rubber boat* kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu? Kwa kweli hii ilikuwa ni aibu, lakini hayo yamepita, tugange yajayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafunzo ni muhimu sana katika uokoaji. Kwa hiyo, hili nalo tuliangalie, tusiangalie mafunzo ya askari tu kushika bunduki kwenda kupigana na kulinda mipaka. Hivyo vita vyenyewe hata havipo namna hiyo, lakini tuwaangalie na waokoaji ambao watasaidia

kuwaokoa wananchi wetu yanapotokea maafa kama yale ambayo yalitokea Dar es Salaam maeneo ya Jangwani.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo na wenzangu wamezungumza la ujambazi, ujambazi mkubwa angalau umedhibitiwa, lakini upo ujambazi unaoendelea Dar es Salaam na unatisha na kwa kweli unasikitisha, Jeshi la Polisi limeshindwa kudhibiti hali hiyo hadi sasa. Naomba sana hili tuliangalie tuone ni jinsi gani tutaliwezesha Jeshi la Polisi liweze kupambana na ujambazi wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, upo ujambazi ambao watu wanaokwenda kuiba, au majambazi hawa wanatumia Pikipiki ambazo ni nyingi sana Dar es Salaam, utakuta kwenye pikipiki wana silaha za moto, wanafanya uhalifu wanaondoka na hakuna hatua zinazochukuliwa, kwa maana Jeshi letu limezidiwa.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa kulikuwa na msako, Polisi walifanya msako kwa ajili ya kukamata pikipiki, matarajio yangu na matarajio ya wananchi ni kwamba, Polisi ukisimamisha pikipiki pamoja na kuuliza leseni ya dereva lakini pia mngekuwa mnafanya na utaratibu wa kuwa-*search* wale wanaotumia hizo pikipiki kwa sababu wengi wao wanatumia silaha ama wanakuwa na silaha za moto kwa ajili ya kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuweze kuidhibiti hali hiyo kwa sababu wizi umekithiri. Ni hatari sana mahali ambapo unatoka nyumbani kwenda kazini asubuhi saa kumi na mbili watu wananyang'anywa, watu wanaporwa na maeneo yanayofanyika hayo yanajulikana lakini hadi sasa bado hali haijarekebishwa. Naomba Jeshi la Polisi na

Serikali kwa ujumla tuangalie ni jinsi gani ya kupambana na wimbi hili la ujambazi wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni vitendea kazi, kama Jeshi halina vitendea kazi vinavyokwenda na wakati, hilo siyo Jeshi na siku zote Jeshi hilo litakuwa linazidiwa tu na wahalifu. Kwa mfano, Kituo cha Polisi Magomeni ama Oysterbay vimepandishwa hadhi, Polisi Kinondoni sasa ni Mkoa lakini ukienda kituo cha Polisi cha Magomeni, utastaajabu sana. Kinondoni ambayo inakadiriwa kuwa na watu milioni mbili, ukienda kuangalia kituo ambacho kinatumika ni aibu. Kituo ni kidogo, kituo ukienda pale ni pachafu, magari mabovu yamejazana ambayo wanasema labda ni vithibitisho, sijui vitaisha lini, nafasi hakuna, nyumba za Askari ni aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kituo hicho ambacho ndiyo kinahudumua Wilaya nzima ya Kinondoni kwa maana ya Mkoa wa Kipolisi, lipo gari moja tu ambalo labda anatumia *OCD* hakuna lingine, hakuna pikipiki, sasa hawa askari watafanyaje kazi? Majambazi hawa wana vifaa vya kisasa, wana usafiri unaoaminika, Polisi hawana hata usafiri wa pikipiki. Naomba sana Serikali iangalie kwa umakini mno kwa sababu mahali ambapo kuna watu zaidi ya milioni mbili halafu kuwe na gari moja la Polisi ni aibu. Kwa hiyo, naomba sana tuone tunafanyaje kuhakikisha kwamba vituo hivi vinaimarishwa na siyo kupandisha tu hadhi ya Mkoa, hadhi ya Wilaya halafu huduma nyingine hazipo.

Mheshimiwa Spika, najisikia vibaya mno kusema naiunga mkono hotuba hii, na naweza kufikia mahali nikasema siiungi mkono na nikashawishi na wengine

wasiunge mkono. Unapozungumza Bungeni na ukiahidiwa Bungeni hapa unatarajia kile ulichoahidiwa kitafanyika.

Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia kwenye bajeti ya Wizara hii mwaka jana, nilielezea ubovu wa nyumba za askari Magomeni na Waziri akakubali kuja kutembelea ili aone ni jinsi gani tutaweza kuboresha makazi ya askari wetu. Lakini nasikitika sana kwamba, hilo haikufanyika, pamoja na kufuatilia, lakini hakuna kilichofanyika. Sijui kama ni dharau ama ni kitu gani. Kwa hiyo, inaniwia vigumu sana kusema kwamba nitaiunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho za Askari ambazo wenzangu wamezungumza, ipo posho ya laki moja. Hiyo laki moja inazungumzwa, lakini askari kuipata posho hiyo ni mbinde na anaweza akaipata baada ya miezi miwili au baada ya mwezi na anatakiwa aipate ili aweze kujikimu. Lakini siku za nyuma Askari walikuwa wanapewa vifaa vidogo vidogo kama sabuni, dawa za viatu na kadhalika. Vyote hivyo hivi sasa hakuna, kwa hiyo naomba Serikali ione ni jinsi gani itawasaidia Askari kwa ajili ya vitu vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajali barabarani. Hili nalo limekithiri, kama tunasema UKIMWI unaua watu wengi, basi ajali nazo zinatimaliza sana, naomba sana tuangalie jinsi ya kudhibiti ajali hizi. Kikubwa ambacho kinaweza kikasaidia kudhibiti ni kuwa na vifaa vya kisasa vya ku-*control* mienendo ama safari za magari. Leo Askari anasimama barabarani anapima mwendo wa magari yanayokwenda mwendokasi, anatoka amejificha kichochoroni anakuja na tochi anakumulika, unaweza ukampitia ukamgonga, ama unaweza ukakataa kile

alichokipima kwa sababu hakina ushahidi. Inawezekana alipima kwa mtu mwingine halafu anakuoneshea wewe. Lakini vipo vifaa vya kisasa ambavyo ni lazima sasa tuwapatie Askari wa Jeshi wa Usalama Barabarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zipo kamera maalum ambazo wala huhitaji Askari akae nayo barabarani, ukipita itapiga picha na itarekodi mwendo wako na baadaye utachukua hatua. Hata ukimpeleka mtu Mahakamani ushahidi upo, lakini leo kwa tochi zile tunazotumia ni kiini macho na hazisaidii.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuimarisha Ofisi ya Mkuu wa Usalama barabarani Tanzania. Kama Mheshimiwa Waziri atapata bahati atembelee Ofisi ya Mkuu wa Usalama Barabarani wa Tanzania atashangaa sana. Ofisi ni ndogo, ni aibu, haina vifaa vya kisasa na hakuna dalili yoyote kwamba anaheshimika kwa kazi anayoifanya. Naomba sana hili nalo tuliangalie ili tuweze kumwezesha huyu anayesimamia usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. YUSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako. Nami nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhuhannah Wataala* aliyenipa fursa kusimama katika Bunge hili Tukufu ili kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar kwa kushirikiana nami katika shughuli zangu za maendeleo ambazo zinaendelea

katika Jimbo langu la Nungwi, lakini wakatokea wakorofi ambao hawapendi maendeleo yangu, wakataka kwenda kuzuia, tukamwomba kwenda kutuliza hali ile, akatukubalia na akapeleka Jeshi la Polisi na hali hiyo ikaendelea. Lakini hata hivyo, wametafuta njia nyingine wamestopisha shughuli hizo, lakini naahidi ndani ya Bunge hili, pamoja na mwakilishi wangu makini Haji Mwadini Makame ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi na Nishati, Zanzibar tutapigana na maendeleo ya Jimbo letu la Nungwi mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutanguliza ujumbe huo, sasa nachangia mada ambayo ipo mbele yetu. Naanza na kituo cha Nungwi Zanzibar ambacho kipo ndani ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyopita mwaka jana nilisimama katika kiti hiki, meza hii na nikaelezea matatizo ya kituo cha Nungwi, kwamba Mji wa Nungwi hivi sasa unakua kila siku, unakua kieneo na unakua ki-*population*, kutokana na umuhimu wake wa kuwa na hoteli kubwa na uwekezaji. Kwa hivyo, watu mbalimbali wanapenda kuhamia kule kwa ajili ya kutafuta riziki, lakini pia ifahamike kwamba wote wanaokwenda kule siyo kwamba wanakwenda kwa kutafuta riziki halali, wengine wanakwenda kwa njia za uhalifu, kwa hivyo uhalifu katika Jimbo la Nungwi umeongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kukijitokeza mambo mbalimbali ambayo hayakuwepo kwa zama hizo, lakini siku hizi kuna uhalifu wa madawa ya kulevya, kuna uhalifu wa wizi, uhalifu mbalimbali hata watu kupoteza maisha yao. Kwa hiyo nilisihi sana ndani ya Bunge hili Tukufu kwamba kituo kile kinafanya kazi katika mazingira magumu,

nilimwomba Waziri wa wakati ule kwamba kituo kile kitazamwe kwa jicho la huruma. Kituo kinafanya kazi hata gari la doria hakuna na mji ule unakua kila siku. Askari inabidi wafuatilie shughuli zao kwa miguu, hapa panakuwa hapana utendaji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Rais wa Jamhuri ya Muungano Jakaya Mrisho Kikwete alitembelea Jimbo lile tarehe 24 Januari, 2009 na kwa huruma yake aliwaahidi kuwapatia gari la Polisi kituo kile. Nasikitika mpaka leo gari lile halijapatikana na Rais kaahidi mwenyewe. Kiongozi yeyote wa Kitaifa anapokwenda mahali awe Rais, awe Waziri Mkuu au hata akiwa Waziri basi ataingiwa huruma kutokana na *situation* atakayoiona pale ili asaidie, au watu kwa matatizo yao wamuombe. Sasa ikiwa unaahidi mwenyewe miaka karibu minne na unajua watu wana tatizo hapajatekelezeka, hapa tunawavunja moyo askari wetu.

Mheshimiwa Spika, askari wanavunjika moyo kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu, kwa hivyo, Waziri atakaposimama naomba anielezee kwamba hii ahadi ipo au ime-*expire*. Kama ime-*expire* nijue kwamba hakuna na sitosimamateni kuulizia ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Miji yenye hoteli kubwa kama Nungwi na mingineyo wahamiaji haramu wamekuwa wakiingia kwa wingi sana, Idara ya Uhamiaji sijaona hata siku moja kufanya *patrol* katika maeneo yale ya Pwani kuangalia angalau watu wapo vipi, hili ni tatizo. Kwenye fukwe kumejaa watu wa ajabu. Nilikutana na Mwekezaji mmoja katika Jimbo langu nilipomtembelea alilalamika sana kutokana na watu wanaoingia na biashara mbaya za

unga, lakini pia akinamama ambao wanafanya biashara ya miili yao, hali inakuwa mbaya katika fukwe. Kwa hivyo, Idara hii isibakie kukaa ofisini tu, ni lazima ifanye *patrol* katika maeneo kama yale ili kudhibiti mawimbi haya. Mawimbi haya ndiyo yanayosababisha uhalifu, yanasababisha kila kitu. Kwa hiyo, nakuomba jambo hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha Polisi Mkokotoni, katika bajeti iliyopita niliuliza kama Serikali ina habari kwamba kituo hiki kimeungua, Waziri wakati huo alinijibu kwamba Serikali wanayo habari kwamba kimeungua na kitajengwa kituo kile katika Daraja A ndani ya bajeti iliyopita ya mwaka 2011/12. Nimepata taabu sana kwa sababu mimi ni Mkazi wa Kaskazini, nimekuwa nikienda kutazama kama kile kituo kinajengwa wapi, nimetafuta kabla ya kuja hapa sijaona kinapojengwa kile kituo kwa sababu tuliambiwa kitajengwa katika bajeti iliyopita. Ingawaje Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Tumbatu katika kuchangia kwake alisema anashukuru na kinajengwa, lakini kabla sijaja hapa nilikwenda kukitafuta sana na sikukiona. Kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri kama kituo kile kimejengwa mafichoni akija hapa pia anieleze kimejengwa mahali gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilieleza pia pale Mkokotoni kwa kuwa kituo kile kinacheleweshwa, Askari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanabanda ambalo ukinyanyua mkono unagusa bati na halina *hardboard*. Kipindi cha joto utawakuta Askari wameacha midomo wazi kama ya kuku wanaofugwa kwa taa, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Askari kama hawa ambao wana mazingira magumu hawawezi kuwa jasiri hata siku moja. Kwa sababu utakuta kazi ni ngumu, lakini ukienda majumbani mwao hali ni ngumu, mishahara yao sitaki kusema, lakini kila Mbunge anayesimama anasema hivyo. Watapata wapi ujasiri askari wetu?

Mheshimiwa Spika, askari ni lazima wawekewe mazingira mazuri ili wafanye kazi vizuri, la sivyo rushwa haitaondoka, madawa ya kulevya hayaishi, kila kitu hakiishi kwa sababu askari ana njaa, akipewa chochote anaona *Alhamdulillah*, anatia mfukoni mwake anasahau kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku ya Tarehe 4 Julai, 2012, maeneo ya Msata kutoka Bagamoyo, wamekamatwa Mashekhe na Jeshi la Polisi, kwa kweli kitendo kilichofanyika ni kitendo kibaya na ni kitendo cha udhalilishaji wa Mashekhe wetu. Polisi wanavyodai ni kwamba wamepata ripoti kwamba kuna gari zimechukua wahamiaji haramu. Lakini wamevaa nguo za kiraia na bunduki, sitaki kuingia kwa Ulimboka. Lakini Ulimboka alikamatwa na watu ambao wamevaa kiraia.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, hebu tuachane na mambo kama hayo.

MHE. YUSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nafuta kauli hiyo haraka sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kuonesha kwamba askari anapokuwa amevaa kiraia na Bunduki basi

sijui ni nani anayeweza kuamini kwamba huyu ni askari na hivyo ndivyo walivyokamatwa hao Mashekhe, ndilo lilikuwa kusudi langu. Mashekhe walikamatwa, baada ya kukamatwa wakagaragazwa chini na kanzu zao na kofia zao, hiki ni kitendo cha aibu kwa Jeshi letu la Polisi ambapo tuna Utawala wa Sheria na Haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Mashekhe mashuhuri ndani ya Tanzania, lakini aibu kubwa siyo wao tu Mashekhe walikuwa na Mashekhe wageni kutoka Saudi Arabia, Yemen na Qatar ambao walifanya ziara yao katika Mkoa ya Morogoro, Tanga, walipokuja Dar es Salaam ndiyo wakakumbwa na mkasa huo. Sasa hapa nashangaa sana. Ugeni mkubwa kama huo ambao umeingia ndani ya nchi na *documents* zote halali, halafu unakutwa na mkasa kama huo, wakiwa na wageni tena Mashekhe wenye hadhi ya juu ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa tunaliingiza Taifa letu katika aibu. Lakini pia askari hao wamepata taarifa kwamba kuna wahamiaji haramu, lakini ukishamkamata mtu na wewe umepewa tu habari hajafanya fujo, kwa nini usimwuulize unamdhalilisha, unamgaragaza na vilemba vinavuka, kwa kweli jambo hili linanisonsha sana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri, Askari wetu wafanye kazi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. YUSUF HAJI KHAMIS: Ndiyo kengele ya mwisho hiyo? (*Makofi*)

SPIKA: Ndiyo, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Meshack Opolukwa atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Diana Chilolo naye ajiandae na pia Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ajiandae.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia Bajeti ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, baada tu ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Meatu nilikwenda kutembelea maaskari waliopo pale Meatu kuwezakusikiliza kero zao na matatizo yao ili kuweza kuyafikisha kwenye vyombo vinavyohusika. Baada ya kufika kule kilio kikubwa cha Maaskari ilikuwa ni kutokupandishwa madaraja pamoja na kupandishwa vyeo. Kuna baadhi ya majina machache kwa ruhusa yako ningependa niyasome. Kuna askari E662D anaitwa Fedelisi Mchaka, kuna Askari E7147 PC Christopher sasa huyu Christopher yeye ameajiriwa mwaka 1993 mpaka mwaka 2012 hajawahi kupandishwa cheo hata mara moja miaka 19. Kuna askari WP 3840D anaitwa Asia, kuna Askari anaitwa E8393 PC Kwandu.

Mheshimiwa Spika, tunawakatisha tamaa watumishi wetu wa Jeshi la Polisi, kwa kutowapandisha madaraja yanayostahili. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aweze kuliangalia suala hili kwa makini ili Maskari wote nchini siyo Meatu peke yake ambao wana matatizo na upandishwaji wa vyeo na madaraja waweze kufanyiwa hivyo ili waweze kufanya kazi yenye tija na kuweza kuwasaidia watu wetu kwenye ulinzi wa mali zao pamoja na usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo lipo katika maeneo mengi nchini ni suala la maaskari wetu kuhamishwa vituo vya kazi bila kulipwa stahili zao. Kuna Askari ambao walihamishwa kutoka Meatu Maaskari sita, Maaskari hawa tangu mwaka jana takriban mwaka mzima hawajalipwa fedha zao za uhamisho, wanaishi kwa taabu, hawana fedha, familia zao zinahangaika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ili aliangalie suala hili kwa makini ili kuweza kuhakikisha maaskari hawa sita ambao walihamishiwa vituo mbalimbali, kuna askari anaitwa *SSGT* Joseph, kuna Askari *SGT* Nyamwaja, kuna Askari Koplo anaitwa Renaro walihamishiwa Ushirombo mwaka jana takriban mwaka mzima bado hawajalipwa pamoja na wengineo wanaofuatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Meatu kuna Gereza ambalo halijakamilika, Gereza hili la Meatu linahitaji takriban milioni 50 tu lianze kufanya kazi. Hii milioni 50 inakuja kwamba kuna vitu vya muhimu vinavyotakiwa kufanyika ili Gereza hili lianze kufanya kazi. Kwa mfano, katika Gereza hili miundombinu yote imekwisha kamilika. Maji yameshaingia ndani, umeme umekwishaingia, magodoro yapo na Gereza hili lina uwezo wa kuchukua hadi watu 150 bila kubanana. Lakini shilingi milioni 50 ikipatikana linaanza kufanya kazi, matokeo yake watuhumiwa wote na wafungwa wote wa Meatu wanapelekwa Gereza la Maswa. Hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa kutumia gari la Polisi kufuata aidha, watuhumiwa au ndugu wa watuhumiwa au wafungwa kwenda kuwasalimia zaidi ya kilomita 100 kwenda na kurudi ni kilomita 200.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa Waziri aweze kuliangalia suala hili ili angalau zipatikane hizi milioni 50 kwa ajili ya kuweza kulikamilisha Gereza la Meatu ili kuondoa usumbufu kwa Jeshi la Polisi, lenyewe kufuatilia watuhumiwa, kupeleka wafungwa, lakini pia kuweza kupunguza gharama. Nilikuwa nafanya *calculations*, tutaokoa kiasi gani kama Gereza la Meatu, litakamilika, tutaweza kuokoa shilingi 330,000 kwa wiki kwa kuweka mafuta lita 50 kwenda na kurudi Maswa kurudi Meatu.

Mheshimiwa Spika, tutaweza kuokoa milioni 1,320,000 kwa mwezi mmoja na kwa mwaka tuna uwezo wa kuokoa milioni 68. Milioni 50 kwa milioni 68. Ningeomba kabisa hii fedha ipatikane. Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia katika vifungu vyake aweze kufanya marekebisho, hii fedha ipatikane wananchi wa Meatu waweze kuishi vizuri katika gereza lao na kuweza kufanya kazi yao bila matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niongelee uhaba wa vitendea kazi kwa maaskari wetu, najikita kwa Meatu. Pamoja na kwamba ni suala la Kitaifa, maaskari wa Meatu wote wanajinunulia *uniforms* ikiwa ni pamoja na viatu pamoja na suruali zao na mashati yao. Tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali, ule utaratibu wa zamani kama umefutika sijui hawa maaskari waweze kupata *uniforms*. Nimekutana na maaskari wengine pale Mjini Mwanuzi, katika Wilaya yangu kwenye mitumba wanachagua viatu vya kufanyia kazi, hawa Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa fedha ya walipa kodi iweze kufanya kazi kwa kuwasaidia askari wetu wa Jeshi la Polisi, ili waweze kuwa na *uniforms* wawe *smart* waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ukiachana na suala la *uniforms* kuna suala hili jingine ambalo ni la askari wetu kupanga uraiiani. Lakini katika suala la kupanga uraiiani hawa maaskari, kuna baadhi ya askari 30 ambao wanapanga uraiiani walishaambiwa wajiorodheshe ili angalau majina yao yaende Makao Makuu, waweze kufanyiwa utaratibu wa kuweza kulipwa fedha ya pango. Lakini mpaka leo maaskari zaidi ya 30 wanakaa uraiiani.

Mheshimiwa Spika, jaribu kufikiria leo hii askari anayekaa kwenye nyumba yangu halafu kesho napatikana na kosa atakuja kunikamata kweli mimi *landlord* wake? Hii inakuwa ni ngumu sana. Naomba maaskari hawa ambao kwanza ni wachache, hawa 30, waweze kupatiwa fedha ya pango kama ambavyo Serikali ilikuwa imeahidi mpaka wakajiorodhesha kwa majina, ili waweze kuishi vizuri kama ambavyo wanaishi maaskari wengine wa maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* ya ubabe unaofanywa na Jeshi la Polisi, katika Wilaya ya Meatu. Ubabe huu ni wa kutumia silaha za moto kwenye miili ya binadamu. Tarehe 10 Novemba, mwaka jana kuna ndugu Jisuge Mpemba alipigwa risasi baadaye akapelekwa katika Gereza la Butimba, kufunguliwa mashitaka na hawa waliompiga risasa walikuwa ni askari wa wanyamapori. Lakini Jeshi la Polisi, halikuchukua hatua yoyote kwa ajili ya kufuatilia kwa

nini alikamatwa, kwa nini alipigwa risasi na kwa nini alipelekwa katika Gereza la Butimba.

Mheshimiwa Spika, baadaye kuna bwana mmoja anaitwa Juma Mboje alipigwa risasi ya mguu, baadaye akapelekwa kwenye Hospitali ya Mjini Mwanuzi Wilaya ya Meatu kwa kisingizio cha kuingia maeneo ambayo hayahusiki. Jeshi la Polisi, halijawahi kuchukua hatua kwa watu hawa ambao walimpiga risasi mtu huyu. Tarehe 8 Julai, mwaka huu kuna mtu mmoja anaitwa Mr. Bonyela yeye alipigwa risasi na maaskari wa Kampuni ya Mwiba na akapelekwa kwenye Hospitali ya Seriani Mjini Arusha kwa ajili matibabu na hii inafanywa kuwa ni siri ili isiweze kujulikana. Kama Jeshi la Polisi litaendelea kutumia ubabe huu kwa watu wetu, kwa raia wake, itafikia mahali watu watachoka na itafikia watu watasema sasa liwalo na liwe tusifike huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aligusia suala la mauaji yenye sura ya kisiasa. Akaongelea mauaji yaliyotokea Igunga kwenye kampeni za uchaguzi mdogo. Huyu Kada wa CHADEMA aliyeuawa Igunga mpaka leo Jeshi la Polisi halijatoa taarifa yoyote. Kesi haijakwenda Mahakamani, mtu amekufa, damu inawalilia Jeshi la Polisi. Tunaomba Jeshi la Polisi, litoe sasa tamko ni kwa nini mtu huyu hatendewi haki kama wanavyotendewa watu wa kada nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nakwenda kwa umakini, sitaki kupoteza muda mwingi, nilitaka sasa niongelee suala dogo la jinsi ambavyo kumeanza kutokea uvunjifu wa amani katika maeneo yote yanayolima pamba nchini Tanzania hasa maeneo ya Kanda ya Ziwa.

Kumeanza kutokea uvunjifu wa amani ikiwa ni pamoja na kuchoma moto maghala ya pamba, kuchoma moto magari ambayo yanabeba pamba hiyo.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii. Ahsante kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

MHE. LETECIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia kuhusu ongezeko la uhalifu nchini. Sisi wote ni mashahidi kwamba uhalifu umekuwa ukiongezeka kila kukicha. Mheshimiwa Waziri ametueleza leo kwamba magereza yetu yana wafungwa takribani 37,776. Hili si jambo jema hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunayo magereza kwa ajili ya wafungwa hawa, lakini ni lazima tutambue kwamba kuwa na magereza mengi siyo suluhu ya kupunguza uhalifu nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba nitaje baadhi ya madhara yatokanayo na kumuweka mahabusu au mfungwa gerezani. Hasara ya kwanza mtu huyu huathithirika kisaikolojia. Hasara ya pili, mfungwa huyu hata anapokuwa gerezani huendelea kutenda uhalifu. Hasara nyingine, mfungwa huyu hata anapoondoka nje ya gereza anaporudi uraiiani huendelea kutenda makosa. Hasara nyingine ambayo inatumiza Taifa zima ni kuliongezea Taifa gharama kubwa kwa ajili ya kuhudumia wafungwa magerezani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia takribani milioni 3.6 kumhudumia mfungwa mmoja kwa siku 365. Hili si jambo jema kwa Taifa linaloendelea kama kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa suluhu ni nini, wenzetu Marekani wametumia sana *crime prevention program* ambazo zimekuwa zikiwaelimisha raia kuhusu madhara ya kutenda uhalifu. *Program* hizi husaidia raia kwa sababu wengi huepuka kutenda makosa kabla ya kuanza kukamatwa kwa ajili ya makosa. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwekeza zaidi kwenye *crime prevention program* ili tuweze kupunguza uhalifu nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *crime prevention programs* zina faida nyingi. Raia huelewa athari za kutenda makosa, hivyo huogopa kutenda makosa. Vile vile *programs* hizi huokoa fedha nyingi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika iangalie uwezekano wa kuwekeza kwenye hizi *program za crime prevention*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nizungumzie tatizo la wafungwa ambao huwekwa magerezani kwa sababu ya kukosa faini ndogo. Magereza yetu nchini yana wafungwa wengi ambao wamefungwa kwa sababu walikosa faini ambayo walikuwa wanatakiwa kulipa. Wengine utakuta wamefungwa kwa kukosa shilingi 50,000 tu. Hili si jambo jema ni jambo la aibu kwa Taifa kama letu. Ni jambo la aibu kumfungia raia gerezani eti kwa sababu amekosa shilingi 50,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa Bunge lako Tukufu, kwamba ni wajibu wetu wote Wabunge kwa kuwasiliana na *DPP (Director of Prosecution)* tuweze kuona uwezekano wa kwenda kuwatoa wafungwa hawa Majimboni kwa kuwalipia hizo faini ambazo walishindwa kuzilipa matokeo yake wakafungwa magerezani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba Wabunge waliomo humu ndani wamelisikia hili na kwa kushirikiana na Wizara husika tuwasaidie wenzetu ambao wako magerezani kwa makosa madogo tu na vile vile wamo magerezani kwa sababu wamekosa malipo ya faini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nina ombi, ndugu zangu, naomba sana wote kwa pamoja tushirikiane kuondoa rushwa nchini. Rushwa imekithiri kwa sababu tumewaachia TAKUKURU na TAKUKURU hawana uwezo mkubwa wa kuweza kudhibiti rushwa. Ningeomba Serikali iweke utaratibu wa kuwashirikisha Watanzania wote kwa kuwapatia motisha ili wote wawe askari wa kupambana na rushwa. Ningeomba Wizara husika itenge fungu ambalo litakuwa linawalipa wale wote ambao watatoa taarifa za kweli kuhusu rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na naomba kuwasilisha hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Hakuna hoja iliyowasilishwa hapa. Umechangia tu. Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Diana Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kupitia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya

Nchi. Nianze mchango wangu kwa kutoa masikitiko makubwa na kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha kijana wetu Yohana Mpinga.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nadhani ulikuwa haupo, ni katika zile kesi ambazo ziko Mahakamani, tunaomba tafadhali usiendelee kuchangia hilo, ni mojawapo katika hizo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante nilidhani kutoa pole nayo ni jambo tu zuri.

SPIKA: Endelea.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naomba niingie kwenye mada ambazo nilikuwa nimeziandaa. Kwanza kabisa napenda nizungumzie kuhusu nyumba za maaskari wa Singida. Napongeza sana Wizara yangu, Jeshi langu kwa jinsi ambavyo linajitahidi kuwajengea Maaskari nyumba za kuishi, lakini nataka nijue Singida kulikoni! Mji wetu wa Singida, sasa hivi Manispaa kwa kweli imejengeka vizuri mno, lakini nyumba za polisi zinatia aibu. Nyumba za karne moja iliyopita, mpaka leo bado zinaonekana Mjini Singida. Chumba kimoja na sebule inakaa familia yenye watoto watano wa kike na wa kiume. Nataka nijue Wizara hii inawafikiriaje askari wa Singida? Ndio mambo haya haya inawafanya maaskari washindwe kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia bajeti hii nielewe nyumba za maaskari wa Singida Mjini zinafikiriaje, naomba nyumba hizo jamani zitoke, zinatutia aibu, zinadhalilisha Mji wetu, zinawakatisha tamaa maaskari wetu. Nashukuru maeneo mengine nyumba zimejengwa nyingi za kisasa

tena za ghorofa, kwa Singida kuna tatizo gani? Jamani mnapoona wengine tunajitahidi, hebu tushikeni mkono, waoneni hawa maaskari, watieni moyo kwa kuwajengea nyumba za kuishi ambazo zina hadhi na binaadamu wengine wanavyoishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika ukifika pale utasikitika wewe mwenyewe, tena Mheshimiwa *IGP* ameshafika Singida na nyumba ameziona, nakuomba sana Mheshimiwa *IGP*, najua unanisikia, hebu wahurumie maaskari hawa, wajengee nyumba hizo. Zinatia aibu, zinawakatisha tamaa kwa kiwango kikubwa. Naomba niishie hapo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea suala la nyumba, naomba niongelee suala la gari la *patrol* la Polisi, Mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida ni mmojawapo wa Mikoa ambayo bado inakumbwa na suala la kutekwa magari, ujambazi na matukio kadha wa kadha, lakini Jeshi hili la Polisi linapata shida sana kufanya kazi zake kwa sababu hata gari la *patrol* la Mkoa hamna. Tukio lolote likitokea, gari limetekwa, gari hamna, linachukuliwa gari la *RPC* ili maaskari wakimbie kwenye tukio, ndugu zangu, hivi tunawatendea haki maaskari wa Singida kweli? Tunalitendea haki Jeshi la Polisi la Singida? Naomba tukitaka kuwafanya wafanye kazi, hebu wapeni vitendea kazi. Kitendea kazi kikubwa ni gari, ndiyo mguu wa askari kwa tukio lolote la haraka linapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Kituo cha Polisi cha Shelui. Kituo hiki ni kituo kikubwa sana katika Tarafa ya Shelui, lakini kituo hakina usafiri, kina pikipiki, ni kati ya kituo chenye matukio makubwa makubwa ya wizi, ujambazi

ndiyo uko pale, utekwaji wa magari pale Mlimani Sekenke ndiyo uko pale, lakini askari hawana gari. Nawaombea hawa maaskari kwa huruma ya pekee muwatazame kwa jicho la huruma, muwape gari la kufanyia kazi ili waweze kupambana na matukio makubwa yanayotekea katika eneo la Tarafa ya Shelui. Tena wanamsumbua kweli Mbunge wa Jimbo, kila akifanya mkutano pale agenda ni hiyo. Wananchi wanapiga kelele kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu mafunzo ya askari kazini. Tunashukuru kwamba askari wetu wanapelekwa kozi na wanapomaliza mafunzo yao wanapandishwa vyeo aliyekuwa *Constable* anakuwa Koplo na kuendelea. Lakini nataka nijue kulikoni vijana hawa wenye sifa ya kufanana, wameingia kazini mwaka mmoja, wametumikia miaka ya kulingana, wana elimu ya kulingana kama ni diploma wana diploma, mmoja anapelekwa kuchukua kozi ya ukoplo, mwingine anapelekwa kuchukua kozi ya *u-sergeant*, huu ubaguzi unatoka wapi?

Ukifuatilia hata kosa alilofanya huyu ambaye ameambiwa achukue ukoplo hamna, watu wanakwenda kozi moja, wote wanachukua ukoplo, unakuta anaanza kunyofolewa mtu mmoja mmoja, wewe hamia kituo fulani, wewe unachukua *u-sergeant*, wewe hamia sijui wapi, mnawakatisha tama askari. Naomba sana ndugu zangu Afande *IGP* hebu wapeni haki zinazofanana hawa maaskari. Kama wanastahili kupata ukoplo, wapate ukoplo wote, kama wanastahili *u-sergeant* wapate *u-sergeant* wote. Hii kuwafanyia matabaka yasiyokuwa na sababu zozote za msingi kweli unawanyong'onyeza, wananyong'onyea, wanakata tamaa na pia unawajengea

tabia ya kuchukiana wao kwa wao kwamba huyu ni bora na huyu sio bora.

Mheshimiwa Spika, naomba wale walioachwa kuchukua ukoplo, wenzao wakachukua u-*sergeant* na wao sasa wapelekwe wachukue u-*sergeant*, walingane vyeo na wenzao kwa sababu kama ni kutumikia, wametumikia miaka ya kulingana na elimu wana elimu za kulingana. Naomba sana tuwatendee haki hawa vijana ili tuwatie moyo ili na wenyewe wajijue kwamba wana thamani inayolingana katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu maslahi na mishahara ya maaskari. Ndugu zangu, ukiona maaskari wanazembea kazi, wanafanya kazi wanavyotaka, matukio yanakosa usimamizi unaostahili ni kutokana na maslahi. Hawa watu kwa kweli hatuwatazamani kwa macho ya huruma. Mishahara yao ni duni, posho zao ndiyo hizo ndogo na zinapatikana kwa tabu hizo safari za kikazi ndiyo kabisa wanalimbikiza madeni kila siku wanaikopa Serikali, wataikopa Serikali mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa maaskari hawa, tusiendeleo na tabia ya kuwakopa, mnapowapa kazi hebu wapeni na stahili zao. Hii mtakuwa mmefanya jambo zuri tena jambo la kiungwana na mtawatia moyo na watafanya kazi zao vizuri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, wanapata shida askari, wanafanya kazi katika mazingira magumu, wana-*risk*, wako maaskari wanakufa kwa ajili ya kazi zao tu, lakini unakuta mahitaji yale ya msingi hawapati, anatumwa porini, anakaa porini wiki nzima, lakini hana senti tano

mfukoni, anaishi kwa kamshahara kale kale alikokapata wiki tatu zilizopita na bado familia inahitaji na bado wanasomesha, ndugu zangu hawa maaskari hatuwahurumii? Kazi wanayo- *risk* wenzetu, sisi tunakaa ndani, wenzetu wanakaa nje wanatulinda, naomba sana tuwapeni haki zao za msingi wanazostahili, tuache tabia ya kuwakopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tena inashangaza kweli kweli. Mimi kila siku nikipita naliangalia jengo la Makao Makuu ya Polisi pale, naangalia na kitengo cha Uhamiaji pale, jengo hilo kwa Dar es Salaam jamani limeshapitwa na wakati, hata ukarabati haupo? Hivi kweli inawezekana Waziri asahau hata Makao Makuu yake, je, nikimwomba msaada wa kunijengea huko, ndiyo ataniona kweli? Hebu aanze kwake. Lile jengo sisi tumeshachoka kuliona katika mazingira hayo, tunaomba jengo hilo likarabatiwe, liwe na hadhi ya Kidar es Salaam ndiyo Mji mkuu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli halina *standard* kabisa, ukiingia kwenye *lift* mara ukwame, mara sijui vipi, mpaka huwa naogopa. Nikienda kwa *IGP* huwa natembea pole pole mpaka ghorofa ya sita, naogopa kukwama humo. Naomba jengo hilo mlifikirie kulikarabati ni jengo la Serikali, wala sidhani kama kuna Mbunge atapiga kelele katika hilo, tutaona ni kazi tu ya kiungwana pale inafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu askari wa zimamoto. Hawa askari wa zimamoto kwa kweli wamesomeshwa kwa gharama na wanaipenda kazi yao na wanaiheshimu, lakini hawana majukumu kwa sababu hawana vitendea kazi. Huwa wanaangalia hivi hivi nyumba inaungua moto, inateketea, wanaitazama tu kwa macho,

wanashindwa wafanye nini kwa sababu hawana vitendea kazi. Naomba kuwepo na mpango mkakati kuhakikisha angalau kila Wilaya inakuwa na gari la zimamoto ili tukio lolote la moto linapopatikana kuwe na gari ya kusaidia. Hivi kweli moto uzuke Iramba, tsubiri gari ya Singida Mjini iende kuzima Iramba, hiyo nyumba tutainusuru? Itawezekana kweli?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa kweli nitaunga mkono baadaye. (*Makofi*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote niwapongeze na jitihada za watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Mbaraka Abdulwakil pia nipongeze Mkuu wa Polisi, Mkuu wa Uhamiaji, Makamishna wote akiwemo Ndugu Mussa Ali Mussa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nitazungumza juu ya ajira. Hii ajira kwa Zanzibar tunakirimiwa au tuna haki? Kwa nini nasema hivyo, kwa mwaka mzima niliuliza swali hapa katika askari 3,264 Zanzibar walijiririwa 168. Ni suala ambalo linatupa mshangao mkubwa sana wakati tunasema kwamba chombo hiki ni cha Muungano. Hii ni asilimia tano. Ni kitendo cha kusikitisha sana na kitendo ambacho kinaleta kutosikilizana, kuleta ubaguzi. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu wakati askari wanaochukuliwa ni kidogo, tujjalie hata Maofisa wakiwa na jamaa zao, wana ndugu zao, wakimalizika hao, hawa wa chini nafasi hiyo wataipata wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, utaona kwamba hapa panaingia kitu ambacho katika ajira ile itaingia kitu tabaka. Kwa wale wenye vyeo, ndiyo watapata nafasi kwa jamaa

zao, lakini wengine itakuwa haki hawana. Kwa hivyo, Jeshi lile ina maana litajenga tabaka. Kwa hivyo, nahisi sasa imefikia wakati kuhakikisha kwamba tunatenga nafasi za Zanzibar. Kwa nini nasema hivyo, niliuliza swali hapa na nikajibiwa kwamba hatuchukui kwamba huyu Mzanzibari au huyu Mtanzania Bara. Haiwezi kuwa, tumeungana nchi mbili ndiyo ahadi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ukasema kwamba, unachanganya tu mchele na choroko haiwezi kuwa. Lazima tuelewane mwenendo wetu na taratibu zetu na tujue kwamba Zanzibar tunapata wangapi na fursa ambayo wenzetu mnayo zaidi. Huwezi kuajiri Zanzibar usipate vijana wazawa wa Tanzania Bara, huwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo hatuna tatizo nalo, tatizo letu tunataka kujua kwamba, tunachukua Zanzibar vijana 200 au 300 tuelewe sio kusema kwamba hatuwezi kuajiri hawa Wazanzibar hawa Tanzania haiwezi kuwa, haiyumkiniki wenzetu tunamaliza shule kwa maelfu na wenzetu kwa malaki, haiyumkiniki. Kwa hivyo, tunasema suala hili lazima lifuatiliwe na ukweli ujulikane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na hivi sasa alisema kwamba ataajiri 3,000 hata kama mkachukua 2,000 sisi mkatupa 1,000, kuna ubaya gani? Kuna kasoro gani kuchukua 2,000 sisi mkatupa 1,000? Wenzetu tunajua kwamba wengi, wenzetu tunajua kwamba Taifa kubwa zaidi, kwa nini tusigawe kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, lakini lingine tunasema kwamba tunachukua vijana hata kutoka vyuoni, lakini tunahisi kuna vikwazo vya kujijendeleza kwa Jeshi letu la Polisi. Vijana

wapewe fursa, sisi tunahitaji vijana waliosoma, lakini kuna vikwazo vikubwa hata ukipata nafasi nenda kusoma na hata ukasema kwamba mimi nikasome nje ya nchi, basi ndiyo matatizo zaidi na wengine wanakuwa muda wao ni karibu kutokana na taaluma yao, sasa wanataka kwenda mbele zaidi, inabidi lazima aongeze taaluma yake ili afikie ule muda na apate kile kipato zaidi hata wakati wa kustaafu. Sasa kwa nini tunawazuia hawa? Kwa sababu gani? Tusijenge imani kwamba labda kwa sababu niko mimi tena labda mwenzangu nimbane, hatuwezi kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kwenda kwa shabby wewe hujui utaishi kwa muda gani. Kuna wakati unaweza ukaondoka ikiwa ni kwa njia yoyote ile, kwa hiyo tuwape fursa na hawa wenzetu wafanikishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine tunakuja kuhusu maslahi. Natumai wenzangu wameweza kuzungumza kwa muda mrefu kuhusu hili. Jamani niliuliza swali ndani ya Bunge hili mnamo tarehe 18, nikaambiwa Sheria ndiyo inayowabana Jeshi la Polisi hata kupata kima kile cha chini. Sheria hizi jamani, tuliondoa ukoloni ili tujitawale na kupanga mipango yetu, yale yenye maslahi ya Taifa letu ndiyo madhumuni yake. Tusipangiwe, tupange wenyewe. Hivi imekuwaje miaka yote toka tulivyojitawala mpaka leo Sheria hizi hazijaondolewa kwa nini? Hivi wewe unafikiri dharau pia inapita, utaona kwamba Mwanajeshi anaweza kumdharau Polisi na hiyo iko. Kipato kinajenga kiburi na ndiyo sababu kubwa hiyo, Polisi anaweza akamkamata Mwanajeshi, matokeo yake ikiwa ugomvi, kiburi. Tunaomba Sheria hii imewabana, imewagandamiza Polisi, iondolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi Wanajeshi wanalipwa na Serikali gani? Hii Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa nini hatuwezi kubadili na hawa wakalingana na wenzi wao? Kitu gani cha kufanya choyo na hawa wana kazi kubwa zaidi, kama mnasema vita, nani asiyepigana? Hapa paingie mtiti nani asiyepigana? Unafikiri anakwenda Jeshi peke yake? Tunachukua mpaka madereva wa nje nao wanakwenda kwenye msitari wa mbele na hiyo ilishatokezea kwa Iddi Amini. Kwa hivyo, usitegemee na Polisi atakwenda msitari wa mbele, kama ni kisa hicho.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wengine hata malipo hayatambuliki, anakwenda mstari wa mbele, labda ndiyo sababu yenu iliyokubaneni. Kwa hivyo, nasema Sheria hii Waziri mhusika utuletee katika Bunge hili Tukufu, tuondoe Sheria ile tulete Sheria ambayo itawanufaisha Polisi na wao walingane na wenzi wao kwa Serikali hii hii moja. Hao wanalipwa na Serikali hii. Kwa hivyo na wenzetu tuhakikishe kwamba Serikali hii ndiyo inawasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine. Kuna rambirambi, hakuna mfumo maalum unaoeleweka. Kuna askari anaweza kufiwa hapa au kufa akalipwa laki tano, pengine akalipwa milioni. Huu si mpango. Kiwango kinachangiwa sawa, pesa zinazopatikana, zipatikane sawa. Haiwezi kuwa huyu awe na umuhimu, maiti hii ina umuhimu, maiti hii haina umuhimu, kufa ni kufa tu. Kwa hivyo, hili tunataka lieleweke na askari wanasikitika kwa suala hili. Kwa hivyo, mfanye utaratibu suala hili mlirekebishe ili mafanikio yapatikane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, *radio call*. Kule Zanzibar mara nyingi wanatumia visimu vyao, vimeo vyao. Mkipita huku unaona kila kituo unachopita kama utasimamishwa

radio call wenzetu wanazo inakuwaje? Hivi hawa askari wamejigawa kuna Wazanzibari mbali na wa Bara mbali? Mbona tunaonesha tofauti ambazo hazina maana? Mbona tuna tofauti ambazo hazileti mantiki? Vitu vidogo kama hivi kwa nini vitutofautishe? Usione kile Kisiwa kidogo, kina mengi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, na ile tunasema ni nchi ndiyo tulivyokubaliana. Au wako wengine wana matatizo hapo au wanasema vingine? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, *radio call* tuhakikishe zinapatikana kwa sababu wanatumia simu zao, lakini pia hawalipwi, sio kwamba wanalipwa, hawalipwi. Atatia vocha, halipwi. Kwa hivyo, tuhakikishe kwamba radio call zinakuwepo na hivyo vimeo unaweza kupiga pia usipate mawasiliano, matokeo yake hali inakuwa hairidhishi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mategemeo yangu niliyoyasema yote yatachukuliwa hatua ipasavyo. Kutokana na hali hiyo nasema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mie kidogo nizungumzie kuhusu Wizara hii na naomba mie niangalie saa ile ya ukutani. Naona saa hii kidogo inatupotezea dakika baadhi ya wakati.

SPIKA: Haya hiyo hiyo. (*Kicheko*)

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara kama hizi za Muungano hasa kama hii ya

Mambo ya Ndani inatakiwa ichangiwe si chini ya siku tatu. Sisi Wabunge tuko tayari tusichukue hiyo posho ya siku moja lakini tuelezee tuliyokuwanayo kutokana na matatizo ya Jeshi la Polisi. Ni Wizara ambayo ina Uhamiaji, ina Polisi, ina Magereza, utachukua wapi uache wapi? Na wote ni majeruhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini acha niendeleee. Hakuna kitu hatari duniani kama njaa. Njaa imegawanyika katika makundi matatu, kuna njaa kwamba, una fedha, lakini chakula cha kununua kwa hizo fedha hakipo, hilo ni janga. Kuna njaa kwamba, fedha huna, lakini chakula kipo na kuna njaa ya tatu kwamba, unakula chakula, lakini hakina manufaa katika mwili wako.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nikasema hivyo? Hivi Askari Polisi, unampa mshahara, huu mshahara uliotajwa hapa, maana naona aibu hata kuutaja na *inflation* hii tuliyokuwanayo na *calories* ambazo zinatakiwa awe anakula Polisi au Jeshi au Magereza, atakula chakula kweli kinachomfaa katika mwili wake? Hatuoni kwamba, sasa angalau kwa kuanzia mshahara wa chini wa Polisi, *net*, uwe shilingi 350,000/= mpaka 400,000/= ? Sikwambii posho, ambayo unampa 100,000/= ni 3,333.33/= kwa siku, atakula nini kwa 3,000/= ? Utamfanya awe na afya kweli ya kufanya hizi kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Polisi tunawaona wanavyotaabika barabarani, wao ndio wa mwanzo kwenda kuzuia maandamano, wanaingia mpaka Misikitini na viatu na wanasema haya, ni amri. Wanalinda Makanisa, wanasema haya, ni amri, lakini kwa nini sisi, wao tusiwajengee mazingira ya kwamba, wanapochukua hizi hatua kwa

mujibu wa Jeshi lao, angalau na wao wakawa na kipato kinachoweza kuwaingizia kipato cha kula wao na watoto wao?

Mheshimiwa Spika, Polisi, anakaa mpaka miaka 20 hajapandishwa cheo, yuko kwenye Polisi Konstebo, hakuna Koplo, hakuna Sajenti, kiko kikundi benchi ya 1995 ya 74, mpaka leo hawajapandishwa vyeo. Hawapewi nafasi ya kwenda kwenye mafunzo kila baada ya miaka mitatu wakapanda cheo na cheo kikampandishia mshahara wake, anaachwa pale pale. Hizi si taratibu za Jeshi la Polisi, ni kwa nini tufanye hivi? Lakini wenzao wa Magereza inasemekana kwamba, wanapanda vyeo kila baada ya miaka mitatu, bila ya kwenda mafunzo; ni kwa nini, hawa wasiende wakati wanatumikia Jeshi moja au Wizara moja? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Pensheni ni haki yake Polisi kupata. Ningeshauri hasa, hii *gratuity* iondoshwe, wanaadhirika baada ya muda. Kwa sababu, *gratuity* yenyewe ni mkia wa mbuzi. Bora aingie kwenye pensheni, ili pensheni yake imsaidie katika *life time* yake, kuliko kumjengea mazingira ya kumpa pesa Sh. 5,000,000/= au Sh. 10,000,000/= baada ya mwaka pesa haipo, biashara haifanyiki, hali ya nchi tunaijua inavyokwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna fedha wanachangishana za Sh. 5,000/= kwa kila mwezi, ili wanapofikwa na maafa ya kufiwa, kama mtu amefiwa na mkewe, watoto, wazee wake, anapewa fedha. Anazika maiti, baada ya miezi mitatu, amesahau msiba, labda ndio anapewa hiyo pesa ambayo ilikuwa apewe. Nasema hapa, ufanywe utaratibu wa *database* ya hizi fedha wanazochangisha, iwapo Polisi

atastaafu, atamaliza muda wake na kwa bahati nzuri yeye hakufiwa, basi 50% ya mchango wake arejeshewe, eeh. Kuna nchi watu wanapata *benefits* kama hizi bila hata kuchangishwa, kwa nini, Polisi tuwachangishe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la likizo. Likizo kama fedha hazipo, wazuiliwe likizo. Unampa likizo unamwambia haya nenda kwenu, katembea halafu urudi na watoto wako, anakwenda na nauli ipi? Mpaka anarudi ndio a-*claim* apewe hizo fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanapolinda mabanki wanalipwa 10,000/=, lakini hatujaambiwa hizo benki zinalipa kiasi gani kwa Wizara. Kwa nini, alipwe 10,000/= ? Kwa hivyo, mambo mengi tu yapo ya kuwasaidia hawa ndugu zetu wakaweza kuwa na imani zaidi ya kulitumikia hili Jeshi. Hali zao ni mbaya, mishahara ni midogo, posho hazilingani na hali ya *inflation* ya nchi, nyumba hawana, umeme hawalipiwi kwa wakati, wengine wanakuwa na *LUKU* wengine hawana *LUKU*. Hata aanze ku-*claim* apate pesa zake za umeme, kwa nini, isiwekwe *percent* kwenye mishahara tu kwamba, kila mwezi awe anapata 30,000/= ya umeme, basi imekwisha. Tena akilala na kandili, akilala na umeme, hiyari yake, pesa umeshampa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, ili Jeshi la Polisi liweze kufanya kazi vizuri na liweze kuwa na zana za kisasa, Wizara kwanza, iwe tayari kuwajengea mazingira mazuri ya maisha yao ya kila siku. Maisha jamani ni magumu sana, unamlipa posho ya 100,000/=, 3,000/= kwa siku anakwenda kula nini? Hii sio *chock-stick* ya Bakhresa? Yaani Polisi, unamlipa kwa kutwa *chock-stick* ya Bakhresa? Ndio maana yake. Kwa hivyo Polisi tuwahurumie. Wenye vyeo wabakie na vyeo

vyao, lakini mshahara wa chini tena uwe unapandishwa kila baada ya miaka mitatu angalau kwa 25%, basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo nasema, Serikali hii kama iko makini, hii gesi tunayochimba sasa hivi, hebu kaichukulieni mkopo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yuko hapa ananisikia, nchi za wenzetu ndivyo wanavyofanya; ukishapata kitu kama hicho unakwenda kukichukulia mkopo, ukishachukua mkopo anzisha viwanda vya ndani, watu 16,000,000 wanalima pamba, peleka viwanda vitatu vikubwa, tuanzishe biashara ya kutengeneza nyuzi na vitambaa tusafirisha nchi za nje. Wakati gesi inatoka, fedha tunalipa kidogo kidogo, tuna viwanda tumetoa ajira, wakulima wa pamba wanainuka, nchi inakuwa na *revenue* zaidi, ndivyo itakavyoweza kujenga mazingira mazuri ya hawa Polisi, Jeshi, Magereza, *Immigration* na wengineo, ndivyo nchi zinavyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Qatar ile pale ina gesi, tazama hiyoo inakwenda zake. Algeria wana gesi, Iran wana bomba wanasafirisha mpaka Russia. Sisi tuna gesi o, mpaka leo ndio kwanza watu wanaangalia mikataba, wanaangalia 10% zao, kwa nini tusiyatafute makampuni tukayaambia *this area has gas*, wewe chukua *investment* hii, tunataka fedha tujenge viwanda, vijana wetu wapate kazi; wala vijana hawana haja ya kugombana hapa, kuwaajiri katika Polisi peke yake, tunaweza tukawaajiri katika hivi viwanda.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda, tukatengeneza pamba, tukatengeneza viwanda vya kusindika samaki, tukaagiza meli tukavua samaki, fedha zinazoingia ndizo zitakazoweza kuendesha

katika shughuli za Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi kwa sababu, hili sio Jeshi la kuzalisha, hili ni jeshi la kutulinda sisi na mali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ni dogo nataka nilizungumzie, ni *Immigration* ya Zanzibar. Mheshimiwa Waziri, kuna tatizo la mwaka jana kumeundwa Tume kufuatilia tatizo hili na tatizo hili limekuwa kubwa na limewagawa hata Watendaji na Wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar; Mheshimiwa Waziri, nataka ulitolee ufumbuzi hapa ndani ya Bunge, kesho, Tume ile imetoa ripoti gani? Kuna matatizo baina ya viongozi wa juu na Watendaji wa chini.

Mheshimiwa Spika, ukisema kweli na ukazungumza inaonekana wewe ni mhalifu na wewe unakwenda kinyume na mabwana wakubwa, unapewa *transfer* unapelekwa Pemba. Kama kupewa *transfer*, apewe huyo mkubwa ambaye anasababisha vurugu hizi. Idara ya Uhamiaji ya Zanzibar, sio shamba la bibi, ni Idara ya uhamiaji inayoendesha na chombo cha Muungano...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Haya, nakushukuru sana, lakini saa ndio hiyo hiyo uliyokuwa unaiangalia.

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Spika, imekwisha?

SPIKA: Ndiyo. Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Mbilinyi, atakayefuatia ni Mheshimiwa Kidawa Salehe na Mheshimiwa Sabrina, ajiandae.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani. Kabla sijaanza naomba, kama kawaida nimshukuru Mungu; namshukuru Mungu, kwa kila jambo, nawashukuru sana Wanambeya kwa *support* yao na nawashukuru sana Wachungaji wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa sala zao na maombi, ndio zinatuweka fiti, tunaendelea kuwawakilisha kama hivi.

Mheshimiwa Spika, leo nitajikita zaidi kwenye ushauri, nitamshauri Mheshimiwa Waziri, nitamshauri *IGP*, nitawashauri Makamishna na *RPCs* wote, kuhusu namna gani mtazamo uliopo kwa nje kwa wananchi, kuhusu taswira ya Jeshi la Polisi sasa hivi na wanaitazama vipi. Lakini kwanza, kabla sijakwenda huko kwenye kulishauri Jeshi la Polisi na Wizara kwa ujumla, naomba nianze na kitu ambacho nimetumwa na Mbeya Mjini, kuja kusema kwenye Wizara hii leo.

Mheshimiwa Spika, watu wa Mbeya Mjini, wamenituma tena kama walivyonituma mwaka jana kuja kudai Tume Huru, kwa ajili ya vurugu za Wamachinga zilizokuwa kati ya Wamachinga na askari, zilizofanyika Novemba 11, mwaka jana. Wako *serious* na hili kwa sababu, Novemba 11, kwetu sisi kule Mbeya, ndio Septemba 11 yetu na hatutaweza kuisahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu walipata madhara, watu walipoteza mali zao, wananchi walipigwa kwa risasi za

moto, wengine mpaka leo hii wana vilema na hii haiko Mahakamani kwa hiyo, ndio nataka iende Mahakamani sasa baada ya Tume. Watu walipoteza viungo, watu walipoteza maisha; mpaka leo Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini, bado anaendelea kuuguza. Kule Mbeya bado tunauguzana kwa lile tukio, bado tunapeleka watu Peramiho na naomba niwataje kwa majina wahanga ambao ninawasimamia hapa baadhi. Kuna bwana Abel Mwalukali wa Soweto, tulimpeleka Peramiho. Kuna Frank John wa Kata ya Manga, kuna Moses Mwakalukwa wa Kata ya Ruanda, ambaye mpaka leo hii ninavyoongea hapa, yuko kitandani akisubiri apatiwe nyonga bandia. Haya yote ni matokeo ya zile vurugu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zile vurugu kovu lake halijakwisha na Wanambeya, wanataka kujua hatima. Kwa sababu, inachekesha, mpaka juzi napokea *message* kutoka kwa Askari Polisi na yeye ananiuliza Mheshimiwa Tume Huru vipi? Mimi nilipoteza pikipiki yangu. Sasa wananchi wanalalamika, Polisi wanalalamika, *RPC* ameondoka tayari, *DC* ameondoka, mwisho wake kutakuwa hakuna mtu wa kumuuliza maswali, hii Tume itakapokuja. Lakini wananchi wa kutoa ushirikiano wapo na tunaitaka hii Tume kwa sababu, hawa watu niliowataja Mbeya nzima iko nyuma yao na Mbeya wamesema hivi, *this is very serious*, kama hakuna Tume huru na tujue hatima ya hawa; huyu bwana Mwakalukwa Moses, anawekewa vipi nyonga na Serikali, ili apone arudi kwenye shughuli zake?

Mheshimiwa Spika, mke wake ni mwalimu, hana kitu maskini, mshahara hauendi, wanakaa nyumbani wanatazamana mpaka Mbunge aende apeleke hela ndio waende Peramiho. Sasa hivi, Mbeya yote iko nyuma na

Mbeya wamesema niseme na nitasema hili kwamba, isipoeleweka mwaka huu hatutapokea tena Viongozi wa Serikali Mbeya, wa ngazi zote, watakapokuja kutembelea Mbeya mpaka hili suala lipatiwe ufumbuzi wa hawa watu ambao ni wahanga wa risasi za moto kwenye zile fujo za Wamachinga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niende kwenye ushauri. Juzi tu nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, nikampongeza na nikamwambia sijui ni vigezo gani vimetumika kukupeleka Mambo ya Ndani ndugu yangu, maana tulikuwa wote huku, tulikuwa tunakwenda vizuri kwenye Michezo na Utamaduni na *Bongo Fleva* na kila kitu, lakini wamekuppeleka huko. Nikamwambia hivi, Wizara ya Mambo ya Ndani, ni Wizara nyeti kwa Taifa lolote duniani. Ndio inabeba nchi, ndio inabeba Taifa, nikampa mfano Irak, baada ya Saddam Hussein, walikwenda wakaunda Serikali ya Utaifa, sijui Wakurdi, sijui Wassuni na Washia, waliunda Wizara zote. Wizara ya Fedha mpaka Wizara ya Mafuta, ambayo ndio tegemeo la uchumi wa ile nchi, lakini Wizara ya Mambo ya Ndani, ilikaa takribani mwaka mmoja wanabishana wampe nani kutokana na unyeti wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara ya Mambo ya Ndani ni muhimu sana. Ndio maana utaona Tawala zinapoanguka, kama ilivyotokea Misri, watu wanaokwenda na Mtawala ni watu wa Mambo ya Ndani; Mapolisi, Waziri wa Mambo ya Ndani, Majenerali, Makanali, Mabrigedia, huwakuti. *Field Marshal* Mohamed Kantawi, Mkuu wa Majeshi aliyekuwa wa Mubarak, mpaka leo hii ndio Mkuu

wa Majeshi. Hata Hilary Clinton, juzi ameenda *Egypt* na amekutana na yeye kama sehemu ya Serikali, hajaguswa.

Mheshimiwa Spika, Mambo ya Ndani ni nyeti sana na ndio maana nikasema leo nitajikita kwenye ushauri na nawashauri nini ndugu zangu? Kuweni makini, msikubali kutumika kwa maslahi binafsi kwenye mfumo wowote ule kwa sababu, mara nyingi mwisho wake unakuwa mbaya. Waziri wa Mambo ya Ndani, Habib Alhadli, wa Mubarak, amepigwa maisha pamoja na Mubarak, lakini pengine hajafanya kitu. Wakati waliokuwa wanamsaidia kuongoza kwa mabavu muda wote ni Wanajeshi. Kwa hiyo, hili, mtaliangalia jinsi Wizara za Mambo ya Ndani, zinavyotumika vibaya halafu mwisho zinakwenda kuishia kwenye *disarray* na muitumie kama changamoto ya kufanya mambo yaliyo sahihi kwa Taifa na kwa wananchi, ndugu zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani, tumieni weledi wenu kuboresha na kurudisha heshima na imani ya Jeshi la Polisi kwa wananchi, ambayo kiukweli imeshatoweka. Wananchi hawaamini tena hizi hadithi za mambo ya Ndani. *RPC* anatokea sijui Mkuu wa Kanda Maalum, anatokea kwenye *TV* sijui, Mchungaji, hivi vitu kama hivi vyote, eeh. Mchungaji sijui kaja, kaungama sijui nani kakamatwa, kafanya nini, ukweli unavurugwa vurugwa tu, Makamanda wanatumika kisiasa, sijui kwa kutumwa au kwa utashi wao au kwa kutaka kuwafurahisha wateuzi, hiki ni kitu kibaya sana na kitakuja kuwa-*cost* siku moja.

Mheshimiwa Spika, warudi kwenye weledi, wajenge Jeshi la Polisi, waweke mambo sawa, waboreshe usalama barabarani, Wizara ya Mambo ya Ndani, waboreshe *Traffic*.

Waangalie *Traffic* ilivyokaa sasa hivi; mimi sasa hivi nasafiri sana bahati nzuri, nakwenda njiani, kutoka Mbeya mpaka nanihii ni kilometa 800, kila kilometa 10 unakutana na Askari *Traffic* nane, sita au saba, sasa hivi tena sio na *uniform* tu, mpaka wale wenye makofia ya chuma wanatoka siku hizi nao wanashika pochi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Polisi Kata, tena *credit* ziende kwa Mheshimiwa Mrema, kwa sababu, ndio mtu pekee katika nchi hii katika kumbukumbu yangu, aliyeifanyia haki Wizara ya Mambo ya Ndani, akaipa heshima. Igeni mfano wa Mrema. Kwa hili, nitakaa tofauti na itikadi za Kisiasa, nendeni kwa Mzee Mrema, mkajifunze alifanyaje kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, ili mrudi sasa kwenye mstari mboreshe *Traffic*; huna haja ya kujaza Maaskari kutoka Dar-es-Salaam mpaka Mbeya Askari 200? Hiyo *Manpower* yote unaiweka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anzisha *trooper*, anzisha *High Way trooper*, wape magari vijana wa Polisi, kila mtu unampa kilometa 50, kutoka hapa mpaka Mbeya kilometa 800, ni magari 16 vijana 16, anapanda anashuka, anapanda anashuka, vijana wengine sasa hivi wana Digrii za Sheria, wako wanalinda Benki. Hawa wote wangekwenda huko, gari, *Computer*, anazunguka, hii itasaidia kwamba, wale madereva hawawezi kufanya makosa kwa sababu, hawajui huyu mtu atakutana naye wapi. Hajui atakutana na *trooper* wapi, tofauti na sasa unatoka Mbeya, unajua sehemu fulani kuna *Traffic* 10, sehemu fulani kuna *Traffic* 12. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inabidi waboreshe mapato ya hawa watu. Hawa vijana, tena nasikia huku *Traffic*, sasa hivi ndio wanajaa watoto wa wakubwa. Dawa sio kiuwajaza watoto wa wakubwa kule, dawa, njooni na mipango mboreshe Jeshi zima, ili kuwe na mapato mazuri kwa wote, *FFU*, sijui Askari wa Farasi, sijui wa nini, watu wake sambamba kwenye mstari mmoja, hapo ndipo itakuwa kila kitu kitakaa sawa.

Mheshimiwa Spika, sasa wewe Askari, leo hii doria unaambiwa wameletewa magari sijui 150, doria magari yanapewa lita tano, lita 10, lazima utaua pampu kwenye yale magari mapya na Jeshi haliwezi kwenda. Jeshi linaletewa vifaa, ripoti hamna, mlifunga kamera Dar-es-Salaam pale kwa mbwembwe, ooh, sijui kamera kwa ajili ya wizi wa magari, ziko wapi zile kamera? Mbona hatusikii tena? Kimya kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, meli za Polisi, *MV Mamba* na ile nyingine, tukasikia ndio zitaleta ulinzi baharini, mpaka leo yaani hamna kitu, meli zinaungua baharini huko hamna msaada kwa sababu, zile meli hazifanyi kazi, ninazo taarifa. Kama zinafanya kazi tunaomba mtupe taarifa sahihi basi, kuhusiana na hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa vijana wanasindikiza hela kwenye haya magari ya makampuni binafsi, wanasindikiza hela Mkoa hadi Mkoa, gari limebeba maboksi ya mamilioni, maboksi 20, maboksi mangapi; anakwenda mpaka Mkoani analipwa 15,000/= kwa siku. Wakifanya kama Kasusura, chukua hela yote, ingia mitini? Mtamlaumu nani? Haya ni mazingira ambayo mnawawekea ndugu zangu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, hiyo ya kwanza?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo yote...

SPIKA: Ahsante kwa ushauri. sasa...

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ni ya kwanza hiyo.

SPIKA: Ni ya pili.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, imeshafika ya pili?

SPIKA: Ndio, si tunaangalia saa.

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, ya kwanza.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ok. Salamu tu kwa Kova, kwamba filamu yake ya...

SPIKA: Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe? Mheshimiwa Kidawa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ...ya Mchungaji kumteka Ulimboka, haijaeleweka kwa wananchi, inabidi arudi studio. *(Kicheko)*

SPIKA: Kwa nini, nyie mnataka fujo? Eeh? Msimfanye mtu kuongea hovyoy, haina busara hiyo. (*Kicheko*)

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi nichangie hoja iliyokuwepo mezani hivi sasa. Naanza kwa kulipongeza Jeshi letu la Polisi kwa kufanya kazi nzuri ya kutulinda sisi raia na mali zetu. Ni kweli Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa katika mazingira magumu. Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa kilio chao kwa Serikali kuhusiana na vitendea kazi duni visivyotosheleza na ambavyo siyo vya kisasa, wengine wamefika kusema hadi silaha zao ni rungu na filimbi.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia habari ya nyumba za Polisi, maslahi yao, mishahara na mambo mengine, tunaomba Serikali, ichukue kilio hiki cha Wabunge ifanyie kazi kwa maslahi ya Jeshi la Polisi na wao wapate ile *job satisfaction*, wasifanye kazi kwa kuwa ni wajibu wao tu kufanya kazi hii ya kutulinda, kama ni majukumu yao lakini na wao kama binadamu kama ni Watanzania wanataka wafanye kazi wafurahie kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, madawa ya kulevya, katika ripoti iliyotolewa *World Drugs Report, 2012* inaonesha kuwa bado tatizo hili ni kubwa ulimwenguni, watu karibu milioni 27 wanahusika na tatizo hili na karibu laki mbili wanakufa kila mwaka. Nchi zilizopo Afrika Mashariki taarifa zinaonesha nazo zinahusika katika suala la kusafirisha haya madawa ya kulevya kutokana *border* zetu kukosa mitandao ya kiutaalam, hazina miundombinu mizuri ya kuzuia tatizo hili na takwimu zinaonesha Watanzania wengi au wanaongezeka katika kusafirisha madawa ya kulevya

kutoka nchi za Pakstani na Iran kupitisha katika nchi yetu na kuelekea sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa pamoja na Tume ya Madawa ya Kulevya, lakini bado tuna kazi kubwa ya kufanya, jambo la kusikitisha ni kuwa, wanawake sasa wanageuzwa makontena ya kusafirishia madawa ya kulevya, wanawake wa Kitanzania wanapendeza, wazuri, wana sifa nzuri lakini wanaoneshwa kwenye TV kuwa na wao ni makontena. Wito wangu kwa akinamama tukatae kubebeshwa madawa ya kulevya, tufanye kazi halali tusitumiwe kwa manufaa ya watu wengine, tukajiingiza katika biashara hizi haramu haipendezi kwa mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo hili tukikosa ushirikiano wa nchi jirani hatutaweza kupambana nalo, kwa hiyo, ni ushauri wangu kwa Serikali iendeleze mashirikiano na nchi nyingine, ipange mikakati madhubuti ya kupambana nalo kwa pamoja. Lakini na miundombinu yetu ya kwenye bandari hasa hizi za maji na nchi kavu, *airport* wamejitahidi kidogo, kuna mambo na mengine yanasaidia. Lakini nikitoka hapa nikienda Zanzibar, bandari yetu naiona ilivyokuwa wazi, kwa hiyo tufanyie kazi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kuna *NGOs* zinazofanya kazi katika mapambano haya kwa kutoa elimu kwa walio athirika na madawa ya kulevya. Serikali ishirikiane na hizi *NGOs* kuona programu zao zinakwenda vizuri kwa sababu wanaoshughulikiwa ni vijana wetu ambao wameathirika na tatizo hili. Lakini juzi niliona kwenye TV watoto wa nchini Uganda wanaanza kutumiwa katika

biashara hii. Kwa hiyo, tuandae programu za elimu mashuleni kwenye *primary schools* tueleze tatizo hili na ubaya wake na ukubwa wake ili vijana wanapokua waone na wajue kabisa kama hili ni tatizo kubwa na haifai kushiriki katika jambo hili. Elimu itolewe tangu wakiwa wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika upande wa Polisi Zanzibar. Changamoto zilizotajwa nyingi wanazo vile vile katika Jeshi letu la Polisi kule Zanzibar, nyumba za Polisi katika Mkoa wangu wa Kaskazini hakuna askari karibu 99.999 wanaishi uraiani si jambo zuri, athari ya jambo hili wengi wameieleza, siwezi kulirudia. Lakini kinachoshangaza nimepitia tabu letu hili la maendeleo, nimeangalia Vituo vya Polisi bajeti ya ujenzi na ukarabati imewekwa sifuri sifuri, sasa tunapiga kelele hapa, lakini pesa hamna, labda Mheshimiwa Waziri atakuja kutueleza. Je, hiyo bajeti ya ujenzi na ukarabati zimewekwa katika kasma gani ili nasi tuzione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la magari, magari ya viongozi ikiwemo yale tunayoita vimulimuli vimeshapitwa na wakati, vingine vina umri wa miaka kumi na tano na zaidi. Lakini nimefarijika alivyozungumza Mheshimiwa Waziri kusema kuna magari kama 34 hivi yatanunuliwa katika mwaka huu, nataka kuuliza je, katika magari hayo yamo ya kule Zanzibar? Kama yamo nitafurahi na nitashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, niliuliza swali hapa kuhusiana na mbwa wa kipolisi yule ambaye alikuwa anafuatilia masuala ya madawa ya kulevya amefariki, nikaambiwa bado hajanunuliwa, lakini nashukuru Kamishna

wetu na Maofisa wake wamejitahidi wanatumia mbwa wa kienyeji wa mitaani wanawakusanya kwa wana jamii wanawapa *training*, ndiyo mbwa hao wanaowatumia kufanyia shughuli zao za kiaskari. Lakini wanapambana na tatizo lile lile, hawana gari la kusafirishia mbwa hao, ikitokea tukio labda mbwa wakodiwe *taxi* haiwezekani! Unachukua *taxi* na mazingira ya kwetu, mbwa ukimpandisha kwenye ile *taxi* wananchi hawatakodi tena *taxi* milele mpaka ile gari i isafishwe kwa sabuni mara saba, hivyo inakuwa vigumu. Kwa hiyo, tuandae utaratibu, mbwa wale wapatiwe gari zao maalum za kufanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mafuta, kwa kweli ni ndogo, wenzangu wamezungumza hapa, hawa watu watafanya kazi namna gani? Kila muda wanapigiwa simu, nenda hapa rudi hapa, lakini hakuna mafuta watafanyaje kazi, tutawalaumu Jeshi letu la Polisi hawafanyi kazi ipasavyo kumbe hawana mafuta ya kutosha. Lita tano unasafiri kwenda wapi yaani upewe lita tano kwa siku, wanasafiri kwenda wapi, haiwezekani suala hili ni lazima liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuhusu majenereta. Kwenye vituo vyetu, hakuna hata majenereta, umeme wetu ni umeme wa kusuasua, zima washa, zima washa, Vituo vya Polisi vinatakiwa vifanye kazi masaa 24, bila hata majenereta watafanya nini? Hawawezi kufanya kazi kwa vibatari, wawakamate wahalifu, wawaweke mahabusu, wafanye shughuli nyingine kwa vibatari haiwezekani. Mambo mengine ni aibu hata kuyazungumza katika Bunge hili, lakini ni *reality*, lazima yazungumzwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni lile la ahadi ya Rais, mwenzangu Mbunge wa Nungwi amelizungumzia, ahadi imetolewa tangu 2009, kwa hiyo Waziri sasa aifanyie kazi ile ahadi, siyo watu wanalalamika tu. Yeye kiongozi mkubwa ametoa ahadi, ninyi ni wajibu wenu kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, Polisi Jamii, wanafanya kazi na kwa kiasi kikubwa uhalifu katika mitaa umepungua kwa sababu ya polisi jamii. Kule Zanzibar vikundi vile vilivyokuwa vinavuta sijui bangi, sijui vinanusa unga hadharani sasa vimepungua kutokana na kazi ya Polisi jamii. Kwa hiyo, tunapongeza utaratibu huu na uendeleo na tunaomba wale katika Kata zao na katika Shehia zao, wanafanya kazi nzuri wapewe motisha ili waendeleo kupambana, wafanye kazi nzuri na ikiwezekana wapandishwe hata vyeo kwa sababu wanafanya kazi nzuri ya kulinda amani katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni huu utaratibu wa ajira ya vijana wetu Polisi, ilikuwa mwanzo wanagawiwa katika kila mkoa, kila mkoa unapewa kiasi fulani cha watu wa kupatiwa ajira. Hii ilikuwa inajenga Utaifa kwa kila Mkoa kutoa Askari Polisi. Kwa hivyo, inakuwa siyo mkoa mmoja tu au miwili inayotoa watu. Lakini sasa utaratibu umebadilisha ajira zinapelekwa makambini, JKT na pengine JKU, lakini je, kule utaratibu wa ajira unakuwaje? Yawezekana wakatoka watu fulani tu au wa mkoa fulani au wengi zaidi inawezekana wakatoka Mkoa mmoja tu. Kwa hiyo, ujenzi wa Utaifa na uzalendo unakuwa unapotea na kwa jeshi kuwa lina watu wengi kutoka mkoa mmoja, nadhani *revisit* utaratibu mzima, muone mtafanya nini ili kila Mtanzania mwenye sifa stahiki na kila mkoa upate ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

SPIKA: Msemaji wetu wa mwisho atakuwa Sabreena Sungura.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mungu kwa kunipa fursa hii adhimu kuliona Bunge hili la bajeti nikiwa hai na mwenye afya njema. Namshukuru Mungu kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa kwenda moja kwa moja kwenye kuchangia, Polisi wamekuwa na changamoto nyingi. Changamoto ya kwanza ni makazi, Polisi wetu wanakaa kwenye nyumba ambazo ni hafifu, nyumba ambazo ukuta wa Polisi na vijana wake kama ni mabinti na vijana wadogo ni panzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuzitendei haki familia zao kwa sababu tunawakomaza kwa sababu ya umri wao, ni lazima Serikali sasa ichukue hatua madhubuti ya kujenga nyumba imara za Polisi.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni suala la posho. Tumeambiwa hapa mwaka jana na Waziri aliyepita, bahati nzuri sasa hivi Waziri Nchimbi ni Waziri mpya, lakini mwaka jana tumeambiwa posho za Polisi zitapanda kutoka sh. 100,000/= mpaka 150,000/=, lakini mpaka sasa hivi hali si shwari, bado wanapewa kiwango kile kile. Sasa kama imefikia hatua Wabunge tunadanganywa humu na hakuna utekelezaji Serikalini kwa kweli hii inakatisha wananchi tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ningependa kuongelea kuhusu malipo, mafao ya Polisi ambao wamemaliza muda wao. Leo hii ukakutana na Polisi ambaye amemaliza kutumikia nchi hii, ukiona mafao anayopewa kama wewe ni kijana unataka kujiunga na Jeshi la Polisi unakata tamaa, hali hii ni mbaya na haikubaliki kwa sababu nchi hii ina rasilimali za kutosha, kwa nini tusitumie rasilimali hizi kama gesi, madini na nyinginezo kuwawezesha Polisi wetu waweze kupata mafao ya kutosha na mishahara mizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda niende kwenye suala la pili la matukio mbalimbali ambayo yametokea nchini kwenye uchaguzi mdogo wa Jimbo la Igunga, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Wilson Mkama, alitoa kauli kwamba imeleta magaidi kutoka Afghanistan, lakini napenda nisikitike kwamba hatukuona vyombo vya usalama vikimhoji Katibu Mkuu juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu uliopita wa Maswa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Shibuda, yalitokea mauaji, Mheshimiwa Shibuda akawekwa ndani kwa muda kadhaa, lakini baadaye akaachiwa, juzi Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, katoa tamko juu ya kuhatarishiwa maisha yake akiwemo na Mheshimiwa Mnyika hapa na Mheshimiwa Lema, wameitwa mara moja kuhojiwa. Sasa tunasema hii Serikali inaendeshaje mambo yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanahoji, kwa nini watu wengine wahojiwe kwa nini watu wengine wasihojiwe, tumekuwa na uzoefu wa kuhudhuria chaguzi ndogo nyingi

tulikwenda kwenye Uchaguzi wa Igunga, tumekwenda kwenye uchaguzi wa Tarime, tumekwenda kwenye uchaguzi wa Busanda, tumekwenda kwenye uchaguzi wa Tunduru, kote huko ambako tumepita kulikuwa hakuna mauaji lakini kwenye chaguzi mbili tu, chaguzi ya Igunga na chaguzi ya Arumeru Mashariki, ambapo meneja wa kampeni alikuwa ni Mwigulu Mchemba, maeneo hayo mauaji yametokea. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge naomba, kanuni zetu zinakataza kutaja taja majina kwa sababu mkishaanza kutajana majina, naomba mnisikilize hii sisemi yangu nasema kanuni tabia ya kutaja majina inasababisha ugomvi kati yetu, wewe kama una pointi eleza, lakini acha kutaja majina nakuomba uendelee lakini majina sipendi uyataje.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nilikuwa nataka tu kuweka mambo sawa ili kuwawezesha wenzetu wa Jeshi la Polisi waweze kufanya *equal justice* kwa vyama vyote na wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa sababu haki ya kuishi ni haki ambayo ipo kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kila mtu anatakiwa aishi. Pale ambapo tunaona kuna *circumstantial evidence* ambazo zinaweza zikamhusisha Mtanzania yeyote yule licha ya cheo chake, ni lazima tuwaambie wenzetu wa *investigation department* kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani tuweze kuwa-*alert* waweze kuangalia pande zote za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haraka haraka sasa nihamie kwenye suala la wahamiaji haramu. Mkoa wa

Kigoma tumekuwa na changamoto nyingi, wavuvi wetu wanafariki, vyombo vyao vinaporwa kwenye maji. Tunasikitika kusema kwamba, mpaka dakika hii ninavyoongea uchumi wa Mkoa wa Kigoma unazidi kudidimia kwa sababu wavuvi hawaingii ziwani na wakiingia wanavua kwa kusuasua kwa sababu wanaogopa kuhatarishiwa maisha yao. Hali kama hii haikubaliki, tunaona hapa askari wengi mnawaacha mijini, kwa nini maeneo ya mipakani hamuwapeleki askari hawa?

Mheshimiwa Spika, tukiangalia juzi hapa Kongwa wameletwa wenzetu hawa wa Ethiopia, maiti zimemwagwa, nchi hii tunasema miaka 50 ya uhuru tuna ulinzi shirikishi, tuna ulinzi salama, wananchi hawa ambao wanaingia nchini kinyume na sheria na taratibu wanaingiaje mpaka wanafika katikati ya Makao Makuu ya nchi Dodoma? Hii ni aibu kwa miaka 50 ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali itafsiri, kwa nini mnaacha askari wengi maeneo ya mijini, kulinda maandamano ya wanafunzi, kupambana na maandamano ya Madaktari, kupambana na maandamano ya Vyama vya Siasa kama CHADEMA, kwa nini mnashindwa kuweka askari wetu kwenye mipaka kuangalia usalama wa raia, kuangalia usalama wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya hatulielewi Jeshi la Polisi na tunaweza kuona kabisa kwamba watu hawa wanafanya kazi kwa maelekezo ya Chama cha Mapinduzi, wakati walipa kodi wa Tanzania ni watu wote. Lazima Jeshi la Polisi lifanye kazi kwa mujibu wa Katiba na

kuhakikisha kwamba maslahi ya Watanzania wengi yanaangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatari ya hili ni kwamba, kama inafikia hatua linaingia lori na watu zaidi ya 120 nchini hapo hapo kuna uwezekano mkubwa wa kusafirishwa nyara za Taifa ikiwemo tembo, pundamilia na vitu vingine. Lakini kuna uwezekano mkubwa wa kuingizwa madawa ya kulevya, wa kuingizwa silaha ambazo ni mbaya, ambazo zitahatarisha amani ya nchi yetu, ni lazima sasa Jeshi la Polisi liweze kufanya kazi inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitakuwa mchoyo kama sitompa pongezi za dhati *RPC* na *OCD* wa Mkoa wa Dodoma mbona wao wameweza, Dodoma sasa hivi kwa kweli wamejitahidi sana na ningependa kutoa wito kwa viongozi wengine wa Polisi, mamlaka za Polisi Mikoani na Wilayani waje kwa viongozi wa Dodoma, wajifunze, wenzao wamewezaje ku-*control* hali hii ya uhalifu katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani tunaona hapa kuna idadi ya wanaume 16,700, ambao wamepewa kifungo cha kunyongwa, lakini kuna wanawake 308, adhabu hii tunavyosikia kwamba kwa mujibu wa mikataba ya Kimataifa, Tanzania tunataka tuifute. Lakini kama tunataka kufuta adhabu ya kunyongwa, ni kwa nini tuwaweke watu kwenye *desperate condition*, watu wamekaa mtu hajui kesho yake inakuwaje, *psychologically* wanaathirika kwa sababu mtu anajua anategemea kunyongwa, lakini adhabu ya kunyongwa haioni. Hili ni tatizo na tunataka Serikali itoe majibu aidha,

inawanyonga watu hawa ama ndiyo inaridhia hiyo mikataba na kusema kwamba haki za binadamu wasinyongwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi napendekeza wanyongwe kwa sababu katika *Quran* sisi tunaamini atakayemuua mwenzake basi na yeye auliwe na tunapenda Waziri kesho akija ku-*windup* aje atuambie watu hawa wananyongwa ama hawanyongwi. La sivyo mtakuwa hamuwatendii haki Watanzania ambao wanauawa kila siku kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, nataka kauli ya Mheshimiwa Waziri kuhusu wakimbizi, tumepata taarifa hapa kwenye ripoti kwamba kuna wakimbizi kadhaa ambao wameanza kurejea Burundi na Rwanda, lakini kulikuwa na wakimbizi wengi katika kambi ya Katumba na Mshamu huko Rukwa. Tilitaka tujue mwaka jana tuliambiwa kwamba wakimbizi hawa watagawanywa katika Wilaya mbalimbali nchini mwetu. Lakini baadaye kelele za Wabunge kuwa nyingi zoezi hili lilisitishwa. Sasa tunataka Waziri atakapokuja kesho kuhitimisha atuambie *position* ya wakimbizi hawa je, wanarudishwa nchini kwao ama wanatawanywa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa na kwa umuhimu wa kipekee nataka kuzungumzia kuhusu mwendo wa kuendesha mashtaka katika nchi yetu, kuna Watanzania wengi ambao wako magerezani wengine wako lokapu wanasubiri kesi zao kuitwa mahakamani. Lakini tumeangalia kesi mbalimbali hapa za mauaji, kuna kesi kama ya Mheshimiwa Chenge ilipelekwa kwa muda mfupi tu ikaisha, ikaja kesi ya muigizaji maarufu Lulu, tunaona na yenyewe kila siku inaletwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, wakati kuna Watanzania wana miaka zaidi ya mitano mbona kesi zao haziendi na hapa napo tulitaka majibu, Idara ya Mashtaka watuambie nchi hii kuna watu ambao ni *special* kwamba wenyewe wakishtakiwa kesi zao zishughulikiwe kwa uharaka na kuna watu ambao wenyewe tu katika Taifa ni wasindikazaji kwamba hawana umuhimu wowote, hili ni janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kuhusu askari wetu ambao wanakwenda katika maeneo mbalimbali hususan kwenye mikutano ya hadhara kulinda askari hawa wamekuwa hawana vifaa vya kutosha, *bullet proof* hazitoshi, *helmet* hazitoshi na ndiyo maana inafikia hatua kwamba likitokea lolote askari wanaingia mitini, lazima wajilinde kwa sababu wanajua hawana vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka Waziri aje atuambie hapa katika mwaka huu wa fedha anashughulikia kero ya vifaa. Hivyo ili pale ambapo zinatokea vurugu hususan kwenye mikutano ya hadhara, askari hawa waweze kupatikana kwa urahisi na kufika maeneo husika na kuzuia mauaji ambayo yangeweza kutokea kama yalivyotokea katika maeneo mengine mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nasubiri kesho Mheshimiwa Waziri aniletee majibu kwa mambo hayo niliyoyahoji. Nashukuru sana na ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge dakika zilizobaki kabla ya kuahirisha kikao kama nilivyosema hazitoshi. Mtu yeyote ambaye ana hoja nzito, hataji watu, ukiwataja watu

unatafuta maneno ya kujibu, aliyeko humu ndani atakujibu, aliyeko nje kifungu cha 71 atakitumia na ninazo kesi nyingi sana, Waheshimiwa Wabunge mnashtakiwa na watu na bahati nzuri zinaingia kwenye Kamati ya Maadili, nitakuja hapa nitawaambieni wewe ulisema uwongo humu ndani.

Sasa naona mtu yeyote mwenye fikira nzuri sana katika kujadili, anajadili *issue*, hajadili watu, maana ukianza kutaja watu hata busara ile ya kusema inapotea na ndizo fujo zinatokana na hili, kwa sababu mtu anaamua kumtaja mtu mwingine katika majadiliano yao. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, naomba kabisa staha, tusizungumze kama ujanja ujanja tu, hivi tuwe na staha katika kuongea, jenga hoja yako sisi tukusikilize na wananchi wokusikilize.

Waheshimiwa Wabunge, msidhani vituko vyenu mnavyofanya watu hawawaoni, wanawaona. Simu zangu zimejaa kabisa wanavyokuwa na manung'uniko juu ya tabia zetu humu ndani. Tafadhali kila mtu ajistahi mwenyewe, wewe Mheshimiwa jamani, siyo mhuni tu, umekaa unaruka ruka humu ndani, sasa wengine wanasema mpaka utafikiri wanataka kubomoa na viti vyenyewe, halafu hata hoja yenyewe hatusikii sasa! (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa nasema daima ukumbuke wewe ni Mheshimiwa uliyepata kura za watu na wanakutegemea, jenga hoja yako mimi sijali ukubwa wa hoja, lakini jenga basi na sisi wenzio tukusikilize, lakini usiwe na tabia ya kuleta ugomvi. Kwa hiyo, ningepomba sana tuzingatie na tutafanya kazi yetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, niwashukuru sana kwa siku ya leo na kesho nitakachokifanya kwa sababu bado orodha ni kubwa kidogo, tutaendelea kifungu cha asubuhi, ingawa ukisikiliza hoja zinakuwa ni pale pale, ni kama yale yamejirudia mara kumi na Mbunge mmoja kwa busara yake akasema mbona wanarudia rudia. Nikasema ikifika mahali wengine hoja hazipo, inakuwa ni kurudia rudia. Kwa hiyo, hata Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kweli hatakuwa na kazi, maana yake zitakuwa hizo hizo za kurudia rudia. Kwa hiyo, naomba niahirishe kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.54 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, tarehe 18 Julai, 2012, Saa tatu kamili Asubuhi)